# Nipashe

Jumanne Machi 31, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580193

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Wajawazito wahamasika kwenda kliniki baada ya kupatiwa kipande cha sabuni

UKURASA 10


Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ufundi stadi mwarobaini kufungua fursa za kujiajiri

Virusi matata, tishio duniani?

CORONA WIKI ILIYOPITA Wamarekani 100,000 waambukizwa

TEKNOLOJIA

Grace na Nancy wabunifu wanaofanya maajabu ujenzi

UKURASA 13

## TISHIO CORONA

# WAGONJWA WAONGEZEKA

**WADAIWA** ni maambukizi ya ndani, Bunge labadili utaratibu wa vikao, Mahakama yaweka msimamo, kanisa lachukua uamuzi mgumu...*Endelea ukurasa 2, 3, 4, 8, 23*



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas (katikati), akiwatia moyo askari wa kikosi maalum cha kupambana na uhalifu, kilichowasili mkoani Mtwara jana, kwa ajili ya kuimarisha doria katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, baada ya kutokea kwa uvamizi wa vituo vya polisi, kambi za jeshi na benki Msumbiji. **PICHA: JESHI LA POLISI**



## BAA LA CORONA

IDADI ya vifo vilivyotokana na ugonjwa wa corona imeendelea kuongezeka katika nchi mbalimbali duniani na hadi jana Machi 30, vilivyothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ni 30,039 kutoka 26,654 vilivyothibitishwa juzi.

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## SALUM SHAMTE AFARIKI DUNIA

UKURASA 3

## ... Wadau sekta ya utalii waanika walivyoathirika

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAONYWA USAJILI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6



Mwonekano wa daraja la juu la Ubungo (Ubungo interchange), linaloendelea kujengwa katika makutano ya barabara ya Morogoro, Sam Nujoma na Mandela, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wagonjwa wa corona wafikia 19

**Na Waandishi Wetu**

WATANZANIA watatu zaidi wamebainika kuwa na maambukizo mapya ya COVID-19, yanayosababisha ugonjwa wa corona kati ya wagonjwa wapya watano waliothibitishwa jana.

Idadi hiyo mpya, imefanya wagonjwa waliobainika kuwa na maambukizi ya virusi hivyo vya corona nchini kufika 19.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alitoa taarifa hiyo jana kupitia vyombo vya habari na kusema kati ya wagonjwa hao watano, watatu wanatoka Dar es Salaam na wawili Zanzibar.

"Hivyo sasa jumla ya wagonjwa wa COVID-19 nchini ni 19 akiwamo mgonjwa mmoja aliyetolewa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar Machi 28, mwaka huu," alisema Ummy.

Alifafanua zaidi kuwa taarifa za wagonjwa hao wapya wa jijini Dar es Salaam zinawahusu wanaume wawili na mwanamke mmoja.

Alisema watu hao walibainika kupitia vipimo vilivyofanywa na Maabara Kuu ya Taifa akiwamo mwanamume mwenye umri wa miaka 49 aliyekutana na raia wa kigeni kutoka miongoni mwa nchi zilizoathirika.

Waziri Ummy alimtaja mwingine kuwa ni mwanamke mwenye umri wa miaka 21 ambaye ni miongoni mwa watu waliokuwa wakifuatiliwa.

"Kazi ya kufuatilia watu wote wa karibu waliokutana na wagonjwa hawa inaendelea. Tunawataka wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na ugonjwa huu," alisema Ummy.

Ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na homa ya mapafu, ulianza kubainika kuwapo nchini kuanzia Machi 17, mwaka huu, baada ya kubainika kwa mgonjwa mmoja mkoani Arusha aliyetokea nje ya nchi, ambaye kwa sasa ameshathibitishwa kupona.

Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa za kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo, ikiwamo kuzifunga shule zote nchini kuanzia za msingi hadi kidato cha sita na vyuo vikuu na vya ufundi kwa siku 30 kuanzia Machi 17, mwaka huu.

**KAMPUNI YAJITOSA**

Kampuni ya Grumeti Reserves kwa kushirikiana na Grumeti Fund, imefadhili mafunzo ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona katika vijiji 31 wilayani Serengeti na Bunda mkoani Mara.

Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, David Mwakipesile, alisema jana mjini hapa kuwa kwa kushirikisha wataalamu wa afya kutoka halmashauri za wilaya hizo, wamevifikia vijiji hivyo kupitia makundi mbalimbali ya vijana, wanawake na wazee.

Alisema njia zilizotumika kusambaza elimu ya kinga dhidi ya ugonjwa huo unaosambazwa na virusi vya Covid-19 ni pamoja na vipeperushi na matangazo vilivyosheheni ujumbe wa njia bora za kujikinga na kuepuka maambukizo.

"Kunawa mikono mara kwa mara kwa maji yaliyotiwa dawa, kuepuka misongamano na kukwepa kushikana mikono sambamba na kukumbatiana ni masuala muhimu ambayo wataalamu kutoka ofisi za waganga wakuu wa wilaya hizo wamefundisha wananchi katika vijiji hivyo," alisema.

Alisema kampuni hiyo inayojihusisha na utalii na uhifadhi, imetoa kipaumbele katika mapambano dhidi ya corona ili kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha taifa na wananchi wake wanapata uelewa juu ya kujikinga na ugonjwa huo ambao Shirika la Afya Duniani (WHO) limeutangaza kuwa janga la dunia.

Mwakipesile alisema kwa sasa kampuni hiyo imeazimia pia kufadhili matangazo ya moja kwa moja kupitia vyombo mbalimbali vya habari yatakayobeba maudhui ya elimu ya kinga dhidi ya kusambaa maambukizo ya ugonjwa huo katika mkoa wa Mara.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, alisema kwa sasa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo inaendesha operesheni katika maeneo ya Mugumu na vituo vya kibiashara yakiwamo maeneo ya kupokea na kuhifadhi watalii ili kuhakikisha maagizo ya hatua za tahadhari yanafuatwa.

"Tunawashukuru wadau mbalimbali ikiwamo kampuni ya Grumeti ambao wanaendelea kusambaza elimu ya uhamasishaji kwa wananchi juu ya njia bora za kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona," alisema Babu.

Kwa mujibu wa Babu huenda maambukizo haya yaliyokumba dunia yote yakaathiri biashara ya utalii hususan katika mbuga kuu ya Serengeti, kutokana na ukweli kwamba biashara hiyo inategemea wageni kutoka mataifa ya Ulaya na Marekani ambazo kwa sasa zimepiga marufuku na kufunga mipaka yao.

***Imeandikwa na Mary Geofrey, DAR, na Ambrose Wantaigwa, SERENGETI***

# Wadau utalii waanika walivyoathirika corona

**Na Salome Kitomari**

WATOA huduma kwenye sekta ya utalii nchini, wameeleza uwepo wa ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vua corona, ulivyoathiri biashara hiyo na huenda hali ikawa mbaya zaidi kwenye nyakati za kilele cha sekta hiyo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wadau hao walisema kipindi cha biashara kuu huwa ni kuanzia mwishoni mwa Juni hadi mwanzoni mwa Novemba ambapo wageni huanza kutoa oda zao kwa njia ya mtandao.

Kwa mujibu wa watoa huduma hao, kwa sasa wamefunga hoteli na huduma nyinginezo kisha kuwarejesha wafanyakazi nyumbani kutokana na kukosekana kwa kazi.

Mkurugenzi wa Burudika Limited, Erastus Lufungilo, mmoja wa wamiliki wa hoteli za kitalii, alisema alikuwa na wageni wengi walioweka oda mtandaoni lakini waliahirisha huku wengine wakisogeza mbele.

Alisema kwa sasa wamefunga biashara na wafanyakazi wameondolewa na kubaki walinzi kwa kuwa hakuna kazi za kufanya.

Aidha, aliiomba serikali kuangalia suala hilo na kukaa na watoa huduma hao ili kuondoa baadhi ya kodi ambazo kwa sasa hakuna mapato yoyote na haijulikani ugonjwa huo utakwisha lini.

Katibu Mtendaji wa wenye ndege zilizosajiliwa Tanzania (TAOA), Lawrence Miku, alisema usafiri wa ndege wa Tanzania kwa asilimia kubwa unaleta watalii kwa kuwa ni wachache wanaokwenda kwenye biashara au mikutano.

Alisema kutokana na corona asilimia kubwa wameacha kuja na kwamba abiria waliowategemea kwa ajili ya ndege za ndani kuwapeleka maeneo mbalimbali.

"Kama watalii hawapo hatuwezi kwenda ndege zetu kwa asilimia 90 zimeegeshwa haziruki. Kwa sasa hatupati mapato yoyote. Pia wauza mafuta ya ndege hawauzi, kampuni za mizigo hakuna mizigo nao hawana kazi ya kufanya na hawapati chochote huku wakiendelea kuwa na wafanyakazi, watoa huduma kwenye ndege nao wameathirika," alibainisha.

"Tuko njia panda, wenye ndege hata kama haikuruka inatakiwa kulipiwa ada ya kuegesha kulingana na aina, uzito wa ndege na muda. Tatizo kubwa kuna vitu lazima ulipe hata kama hujarudi kufundisha marubani na mainjinia ambayo ni Dola 20,000 (sawa na Sh. milioni 46.2) kwa mwaka ambayo lazima ilipwe," alisema.

Naye, Katibu Mtendaji wa Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania (TCT), Richard Rugimbana, alisema ugonjwa huo ni janga la dunia huku sekta ya utalii ikitegemea wageni wengi kutoka mataifa ya Marekani, Italia, Uingereza na kwingineko ambako wamefunga mipaka na kuzia ndege kuruka.

"Utalii wetu wa juu huanza Juni hadi Otoba na baadaye katikati ya Desemba hadi Machi. Kama hali haitabadilika maana yake msimu hautakuwa mzuri. Tunajua serikali imeunda kamati ya kufuatilia Aprili, Mei na Juni tutajua," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Safari AM Guide Service, Ally Mtemvu, anayemilikia magari ya kubeba watalii, alisema athari ni kubwa kwa sasa kwa kuwa soko kubwa la utalii kutoka Ulaya na China.

Alisema mataifa mengine yanawasaidia watu wao kukabiliana na hali hiyo na kwamba wafanyakazi wengi wako nyumbani kwa sasa na kwamba hali ikiendelea, hivyo sekta ya utalii kurudi kwenye hali yake itachukua muda mrefu.

"Juzi nilikuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kulipia mapato nikawaeleza nalipa mapato, nalipia nini maana biashara imefungwa. Wakaniambia si ulifanya biashara mwaka huu, mwaka huu nakadiriwa nini, lakini hupewi majibu sahihi unaambiwa ulipe sehemu baadaye uandike barua. Serikali iliangalie hili tunalipa kodi katika kipindi ambacho hakuna biashara," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kilimanjaro Guides Association (KGA), Alex John, alisema hata ugonjwa huo ukimalizika athari kwenye sekta ya utalii itaonekana na si rahisi kurudi katika hali yake ya ukuaji kwa haraka.

"Wahanga (waathirika) wakubwa wa corona nchini ni sekta ya utalii ambao hutegemea watalii ambao kwa sasa wamepata misuko suko mikubwa, wakiyumba kiuchumi nasi tunawategemea kutoka kwao."

Alisema Mlima Kilimanjaro peke kuwa na waongoza watalii 2,400 kati yake 1,300 ni wanachama wao, huku wabeba mizigo wako zaidi ya 5,000 ambao wote kwa sasa hawana kazi za kufanya na miezi mingine ijayo hawatakuwa na kazi.

TISHIO CORONA

# Idadi ya wabunge kwenye vikao sasa yapunguzwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKUTANO wa 19 wa Bunge la Bajeti, unaanza vikao vyake leo, huku kukiwa na mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa shughuli zake.

Miongoni mwa mabadiliko ni kupunguzwa kwa idadi ya wabunge kutoka 393 hadi 150 kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Kadhalika, vikao hivyo vitafanyika kuanzia mchana hadi jioni tofauti na awali ambapo vilikuwa vikianza saa tatu asubuhi hadi saa mbili usiku.

Akitangaza mabadiliko hayo jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema bunge hilo litaanza leo hadi Juni 30, mwaka huu na muda wa kukutana umepunguzwa kutoka saa tisa hadi nne kwa siku.

"Kutakuwa na mabadiliko ya hapa na pale kadri siku zinavyoenda, lakini tumedhamiria kuhakikisha tunafanya kazi na usalama wa wabunge ni mkubwa wakati wote wakiwa hapa, tumezuia wageni wasiokuwa muhimu kwa kiwango kikubwa," alisema.

Pia, alisema vitakasa mikono na hatua nyingine zimechukuliwa.

"Kutokana na ugonjwa huu ni rahisi kuambukizwa hasa kwenye mkusanyiko wa watu na mkutano wowote wa Bunge una mkusanyiko wa watu kwa kawaida huwa kuna wabunge 393, watumishi wa bunge, pia wageni kwenye kumbi, hivyo kwa wakati mmoja huwa kuna watu zaidi ya 700," alisema.

Alieleza kuwa kutakuwa na utaratibu wa tofauti na ilivyokuwa nyakati zilizopita.

Alibainisha kuwa awali walikuwa wakikutana kwa saa tisa au zaidi, lakini kwa mkutano huo watakutana kwa saa zisizozidi nne.

"Siku zote za mkutano zitakuwa 92 siku za kazi zitakuwa 64, nyaraka zote zitakazotumika zitawafikia wabunge na waandishi kwa njia ya mtandao hakuna karatasi itakayokuwapo ndani labda aingie nayo mwenyewe, nyaraka zitatumwa asubuhi siku ya bajeti husika," alisema.

Kadhalika, Ndugai alisema vikao vitaanza saa nane mchana hadi saa 12 jioni kila siku isipokuwa leo kikao kitaanza asubuhi.

"Kesho (leo) tutakutana kwa muda ule, asubuhi watapata mambo yote yanayotakiwa ikiwamo randama, na wabunge watapata nzuri ya kujiandaa na kuchangia... na kwa kweli mabunge mengi ya Jumuiya ya madola yanautaratibu huo," alisema.

Aliongeza: "Ndani ya ukumbi kutakuwa na wabunge 150 watakaa kwa nafasi na mawaziri wote watazungumza kutokea kwenye nafasi zao walipo tofauti na awali kusogea kwenye kipaza sauti kimoja, Mbunge akiingia tu ndani ya viwanja vya bunge ataonekana kwa njia ya mtandao.

"Wabunge watakuwa kwenye kumbi zingine ambapo watafuatilia kwa utaratibu wa 'video conference' watafuatilia kinachoendelea na kuchangia hoja kwa kupitia mfumo tulioweka, kupiga kura watapiga kwenye tablets zao na tutapata orodha kwa jina utaratibu ambao ni wa uhakika zaidi."

Kuhusu maswali, Ndugai alisema maswali yote yataingizwa kwenye vishkwambi vya wabunge na mwenye swali la nyongeza atauliza kupitia mfumo wa bunge na majibu yake.

"Hatutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu kabisa kwenye mkutano huu, na maswali ya kawaida yatakuwa 500,"alisema.

Akizungumzia siku ya bajeti ya serikali, alisema Katiba inamtaka mbunge kupiga kura ya wazi, hivyo utawekwa utaratibu ambapo wataingia wachache kuingia na kutoka.

## Wafanyabiashara Mkuyuni wachukua tahadhari ya corona

**Na Abdul Kingo, MOROGORO**

WAFANYABIASHARA katika soko la Mkuyuni mkoani Morogoro wameitikia wito wa serikali wa kujikinga na ugonjwa wa corona kwa kuweka vifaa vya kunawia mikono mbele ya maduka yao.

Akiongea na Nipashe, mfanyabiashara Reginard Silayo, alisema wamelazimika kuchukua hatua hiyo kutokana na kupata elimu ya kujikinga na ugonjwa huo unavyoweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine ambaye hana maambukizi.

Mfanyabiashara wa mitumba katika soko hilo, Ramadhani Pengo, alisema, licha ya kuwawekea vifaa vya kunawia mikono wateja wao, bado kuna changamoto ya baadhi ya watu kukosa elimu ya kujikinga na maambukizi kutoka vijiji wanavyotoka.

Diwani wa Kata ya Mkuyuni, Wilaya ya Morogoro vijijini, Mwinyi Bui, amesema wanaendelea na mkakati wa kutoa elimu kwa wanakijiji na wafanyabiashara wote kujikinga dhidi ya ugojwa wa corona.

Alisema, soko la Mkuyuni ni miongoni mwa yenye mkusanyiko mkubwa ya watu hasa siku za gulio ambazo hufanyika kila Ijumaa na Jumapili.

Wakulima na wafanyabiashara pamoja na wageni kutoka maeneo mengine hukusanyika kwa wingi kuendesha shughuli za kujipatia kipato na mahitaji muhimu.

Mwandishi wa habari hii aliyekuwapo sokoni hapo alishuhudia uwapo wa vifaa vya kunawia mikono mbele ya maduka, biashara ndogo ndogo, migahawa na kituo cha basi.

Mbali na kuwapo kwa vifaas hivyo, wahusika walikuwa wakitoa maelekezo kwa wateja wao kunawa mikono kabla ya kuwahudumia.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Uchukuzi), Dk. Leonard Chamuriho (katikati), akitoa maelekezo kwa uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa meli mpya, chelezo na ukarabati wa meli ya MV Victoria, jijini Mwanza, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Eric Hamissi. **PICHA: WUUM**

# Shamte afariki dunia, kuzikwa leo

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Salum Shamte (67), alifariki dunia jana asubuhi katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) jijini Dar es Salaam baada ya kulazwa kwa siku nane.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MOI, Patrick Mvungi, alithibitisha jana kutokea kwa kifo hicho na kueleza kuwa walimpokea Shamte Jumatatu iliyopita na hali yake ilibadilika baada ya siku tatu.

"Siku ya Alhamisi (Machi 26) hali yake ilibadilika na kuhamishiwa chumba cha wagonjwa wa uangalizi maalum (ICU) na leo (jana) saa 12:44 asubuhi alifariki dunia," alisema.

**TPSF WAMLILIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, amesema wamempoteza mwenyekiti wao ambaye ndiye mmoja wa waanzilishi wa taasisi hiyo iliyoanza miaka 22 iliyopita.

"Hadi umauti unamkuta Shamte alikuwa ni Mwenyekiti wa TPSF. Shamte alikuwa anapenda kusikiliza kila mtu, alikuwa mtu mwenye mawazo mpaka umuone ana hasira itachukua muda mrefu."

"Kuna watu wamejitoa kufanikisha kitu kifanyike, Shamte alikuwa mmoja wapo, wajumbe wa bodi wa sekta binafsi hawalipwi hata senti moja, Shamte alijitolea bila kujali. Amefanya mambo makubwa ya kuendeleza sekta hii."

Simbeye alisema alikuwa mkulima, mfugaji na wakati wote alipenda kujiita mkulima.

"Alikuwa anatetea maslahi mapana ya sekta hii, mwaka 2007/8 alikuwa mmoja wa wana kamati ya Kilimo Kwanza na alisukuma uanzishaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Mpaka anafariki alikuwa anapigania kuwe na Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi Tanzania. Suala hili lipo kwenye mchakato."

Simbaye alisema Mwenyekiti Shamte alikuwa jela na baada ya kuzidiwa alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga, Bombo na hali yake ilipozidi kubadilika alihamishiwa Moi, Dar es Salaam.

"Alikuwa akisumbuliwa na mgongo kabla ya kwenda jela na alipooza kwenda chini," Mkurugenzi TPSF alisema.

**MAZISHI**

Simbeye alisema Shamte anatarajia kuzikwa leo alasiri katika makaburi ya Kisutu na msiba upo nyumbani kwake Mbweni, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam.

**WASIFU WAKE**

Kwa miaka 44, Shamte amekuwa akijihusisha na kilimo cha biashara na miaka 10 kati ya hiyo alikuwa Uingereza akiuza bidhaa za kilimo.

Mwishoni mwa mwaka 2017 alistaafu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Katani.

Amewahi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) ambayo ndiyo taasisi inayosimamia kilimo sekta binafsi.

ACT ndiyo iliyojihusisha na uandaaji wa sera ya Kilimo Kwanza (Agriculture First) iliyowezesha sekta ya kilimo kuwa juu ya mipango ya kiuchumi Tanzania.

Amewahi kuwa Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi ya Shirikisho la Vyama vya masuala ya Kilimo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SACAU) iliyowaleta pamoja wakulima wa nchi Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Mwezi Agosti mwaka 2018, aliteuliwa kuwa mwenyekiti mpya wa TPSF baada ya aliyekuwa Dk. Reginald Mengi (marehemu), kumaliza muda wake kwa kuitumikia kwa kipindi cha miaka mitano.

# Maeneo hatarishi Dar yapuliziwa dawa

**Na Elizabeth Zaya**

MKOA wa Dar es Salaam umeanza kupuliza dawa katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo, ikiwa ni miongoni mwa hatua zinazochukuliwa kupambana na tishio la ugonjwa wa corona.

Akizungumza katika kipindi cha kumekucha kinachorushwa na Televisheni ya ITV kuhusu hatua mbalimbali ambazo Jiji la Dar es Salaam zinachukua kudhibiti ugonjwa huo, daktari kutoka ofisi ya Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Ford Chisongela, alisema wamepuliza dawa hiyo katika maeneo makubwa hatarishi na kazi hiyo inaendelea.

Alisema wameshapuliza maeneo hatarishi 12 kuanzia katika stendi ya mabasi yaendayo mikoani ya Ubungo na nchi jirani ya Ubungo, katika vituo vya mabasi ya mwendokasi kuanzia Kimara, Mkwajuni, Magomeni, Feri na Kariakoo.

Alisema pia wanapita katika maeneo mbalimbali kukagua namna tahadhari mbalimbali za ugonjwa huo zinavyochukuliwa.

"Mfano tumepita katika eneo la Airport pia tumeshuhudia wanachukua tahadhari za kupuliza dawa zaidi ya mara tatu kwa siku hususani yale maeneo ambayo abiria wanapita," alisema Dk. Chisongela na kuongeza:

"Airport wako vizuri na wamejipanga kuhakikisha kwamba maambukizi hayasambai, kila sehemu kuna vitakasa mikono."

Pia alisema wanaangalia njia bora zaidi ambazo zitatumika kutengeneza vifaa vya kuwekea maji tiririka ambavyo vitakuwa na usalama zaidi badala ya kutumia vile ambavyo kila mtu lazima aguse.

"Hizi koki za kufungulia maji tiririka ambazo kila mtu lazima afungue ili anawe nazo ni changamoto na ndiyo maana tunaona kwenye mitandao ya kijamii watu wanajaribu kutengeneza njia za kuleta teknolojia ya mtu kukanyaga na kunawa badala ya kugusa koki," alisema na Dk. Chisongela.

"Na ndiyo maana tunajaribu kushawishi watu kwamba hiyo teknolojia isambae haraka ili kuzuia maambukizi ambayo yanaweza kusambaa kutokana na kugusagusa koki wakati wa kunawa, lakini kwa maeneo ambayo yana watu wengi tunashauri awapo mtu mmoja ambaye atakuwa anawafungulia watu kwa ajili ya kunawa na si kila mtu kugusa."

"Lakini kuna aina fulani ya bomba zinaitwa elbow ambazo zinatumika hospitali, ambazo kufungua au kufunga kwake kunatumia kiwiko, hizo ndizo tunazoshauri zitumike zaidi ili kuzuia maambukizi."



Mafundi wa kampuni ya Mabibo Construction Ltd, wakiendelea na ukarabati wa barabara ya Mwai Kibaki, eneo la Mikocheni Chama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Lowassa ashiriki ibada ya mazishi mtoto wa Sokoine

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu mstaafu na Mbunge wa zamani wa Monduli, Edward Lowassa, jana ameshiriki ibada ya kumuaga mtoto wa kwanza, Lazaro Sokione wa aliyekuwa Waziri Mkuu na mbunge wa jimbo hilo, marehemu Edward Sokoine, iliyofanya Kanisa la Mtakatifu Petro, jijini Dar es Salaam.

Lowassa pia ni kiongozi mkuu wa kimila wa Masai Laigwanan.

Mwili wa Lazaro aliyefariki juzi katika Hospitali ya Muhimbili, ulisafirishwa jana kwa ajili ya mazishi yanayotarajiwa kufanyika leo Monduli Juu.

Marehemu Lazaro ni mtoto wa kwanza kati ya 11 wa marehemu Sokoine.

Lowassa aliyeambatana na mkewe Regina kwenye ibada hiyo, anachukuliwa kama mtu kutoka jamii ya Kimasai aliyevaa vyema viatu vya marehemu Sokoine kuanzia ubunge hadi uwaziri mkuu.

# DC aagiza wafanyabiashara wakamatwe madai kughushi

**Na Ambrose Wantaigwa, TARIME**

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Msafiri Mtemi, ameagiza kukamatwa wafanyabiashara wawili katika eneo la Nyamongo kwa madai ya kughushi nyaraka na kujipatia mamilioni ya fedha kutoka mgodi wa dhahabu wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya Barrick.

Ameliagiza Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya, kuanzisha uchunguzi mara moja na kuwachukulia hatua baadhi ya watu wakiwamo wafanyabiashara maarufu wilayani hapa wanaodaiwa kujenga majengo na miundombinu katika maeneo ambayo yamefanyiwa tathmini na kulipwa fidia.

Wafanyabiashara hao, John Mwita na Paul Masabo, wakazi wa Nyamongo wanadaiwa kuwasilisha madai yasiyo halali na kufanikiwa kushawishi mgodi huo kulipa zaidi ya Sh. milioni 80 katika maeneo ambayo tayari yalikwisha fanyiwa tathmini na malipo siku za nyuma.

Jana Mtemi alisema kwamba serikali itawachukulia hatua kali ikiwamo kuwafungulia mashtaka ya uhujumu uchumi wote ambao kwa nia ovu walifanikiwa kughushi nyaraka na maeneo yaliyokwisha lipwa fidia kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

Siku za hivi karibuni kumekuwapo wimbi la wananchi pamoja na wafanyabiashara ambao wameingia katika mji mdogo wa Nyamongo na kuamua kujenga majengo mapya kwa kasi kwa kushirikiana na wamiliki wa awali katika maeneo yaliyokwisha lipwa fidia maarufu kama 'Tegesha' na kufanikiwa kuchota mamilioni ya fedha.

"Huu ni uhalifu kama mwingine, kitendo chochote cha kujipatia fedha tena kiasi kikubwa kama ilivyotokea hivi karibuni kwa wananchi hao wawili ni kosa la jinai na kusababisha serikali wilayani hapa kuagiza uchunguzi mkali kuhakiki madai na malipo yaliyofanyika kwa wakazi kwa miaka miwili iliyopita," alisema Msafiri.

Kwa muda mrefu suala la malipo ya fidia kwa ardhi inayochukuliwa na mgodi huo kwa ajili ya uchimbaji mkubwa limekuwa kero na wamiliki wa mgodi huo wamelalamika mara nyingi kuhusu madai hewa na wakazi wanaolipwa kuamua kurejea tena katika maeneo hayo na kudai fidia upya baada ya kujenga tena.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya wakazi kulazimika kuendelea kuishi mita chache kutoka hifadhi ya mgodi na hivyo kuhatarisha maisha yao kiafya na makabiliano na vyombo vya dola wananchi wanapolazimika kuingia katika mgodini kutafuta mawe ya dhahabu.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa wilaya amewaagiza watendaji wa kata na vijiji katika maeneo hayo ya mgodini yenye idadi kubwa ya vijana kutoka maeneo mengine ya ukanda huo, wanafuata kanuni za afya kuepuka maambukizi ya virusi vya corona.

"Wakati wananchi wakiendelea na shughuli zao za ujenzi wa taifa katika mji mdogo wa Nyamongo wanapaswa kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kunawa mikono mara kwa mara na sabuni na kuwahi katika vituo vya afya vilivyo karibu mara wakihisi dalili za homa kali na kupanda joto la mwili.

HABARI KITAIFA

# Mabasi hayaruhusiwi kuondoka Kagera mpaka abiria wanawe

Na Lilian Lugakingira, BUKOBA

ABIRIA wanaosafiri na mabasi yanayoanza safari saa 12 asubuhi kutoka mkoani Kagera kuelekea katika mikoa mingine, wametakiwa kufika kituo kikuu cha mabasi cha Bukoba saa 11 alfajiri, ili unawaji mikono na kupimwa joto la mwili uweze kufanyika mapema na kuruhusu mabasi hayo kuondoka kwa muda uliopangwa.

Agizo hilo lilitolewa na Ofisa Mfawidhi wa Mamkala ya Kudhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), mkoa wa Kagera, Shadrack Mahale, ikiwa imethibitika kuwapo kwa mgonjwa mmoja wa corona mkoani Kagera, huku raia mwingine wa China aliyeingia mkoani hapa akitokea nchini Uganda kupitia mpaka wa Mutukula, akiwa amewekwa karantini kutokana na kuwa na baadhi ya dalili za virusi vya ugonjwa huo.

Mahale alisema hakuna basi lolote litakaloruhusiwa kuondoka katika kituo kikuu cha mabasi bila abiria wake kunawa mikono na kupimwa joto la mwili, na kuwa abiria watakaochelewa kufika watasababisha basi lao kuchelewa kuondoka.

"Mapokeo ni makubwa maana elimu tumeanza kutoa kwa muda mrefu, mwitikio ni mkubwa kwa wasafirishaji wameweka vifaa kwa ajili ya kuwawezesha abiria wao kunawa mikono, na sisi kama viongozi tunapita kukagua kila mara ili kujiridhisha," alisema Mahale.

Kwa upande wake Ofisa Afya Mkoa wa Kagera, Nelson Rumbeli, alisema wanaendelea kusimamia afua walizojiwekea ili kuhakikisha ugonjwa huo hauenei zaidi, kwa kuwasimamia abiria kunawa mikono na kuwapima joto la mwili kabla ya kupanda mabasi.

"Hili zoezi la kuwapima abiria joto la mwili ni endelevu, lakini tutahakikisha mabasi yote yanapuliziwa dawa ili magari yote yanayosafirisha abiria yanakuwa safi na salama kwa afya za abiria," alisema.

Mmoja wa madereva wa mabasi hayo Joseph Mushi, alisema wanajitahidi kufuata maelekezo ya wataalamu ikiwamo abiria ananawa mikono kabla ya kupanda basi.

"Mlangoni kabla ya kupanda basi kuna kifaa kwa ajili ya kunawa, tumeweka maji yenye tiba, hii ni moja ya tahadhari," alisema.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakijiandaa kuvuka barabara, huku bajaj 'zikitanua', pembeni na kusababisha foleni isiyo ya lazima na usumbufu kwa waenda kwa miguu katika eneo la Mbezi Mwisho, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Usafiri wa treni wasimamishwa reli yafunikwa maji

Na Neema Hussein, KATAVI

USAFIRI wa treni kutoka mkoani Katavi kwenda Tabora umezuiwa kwa muda kutokana na daraja linalopita katikati ya mto Ugala kusombwa na maji na reli kufunikwa.

Hali hiyo imesababishwa na mvua inayoendelea kunyesha katika mkoa huo na kusababisha mto huo kujaa maji.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi wa Mkoa wa Katavi walisema usafiri wa treni ndiyo uliyokuwa umebaki kwa wananchi wa kipato cha chini, pia ulikuwa ukitegemewa baada ya barabara ya kutoka Katavi kwenda Tabora kufungwa kutokana na daraja la Koga kujaa maji.

"Kipindi hiki usafiri umekuwa shida sana, usafiri tuliokuwa tunautegemea ni wa treni pia nauli yake ilikuwa ndogo sasa hivi nayo imezuiliwa," walisema wakazi hao.

Mkuu wa kituo cha treni Ugala, Abubakari Juma, alikiri kuzuiwa kwa usafiri huo kwa muda usiojulikana na kuwa tayari mafundi wapo eneo la tukio kutatua tatizo hilo.

"Ni kweli usafiri wa treni umezuiwa kwa muda kutokana na mto Ugala kufurika maji na kusababisha daraja kusombwa, mafundi wapo eneo la tukio wakitatua tatizo hilo," alisema.

Njia pekee ya usafiri kwa wananchi wa Katavi kwa sasa ni wa anga au kwa basi kupita wilayani Uvinza mkoani Kigoma.

## Jela miaka 30, viboko 10 kwa unyang'anyi

Na Daniel Limbe, CHATO

WAKAZI wawili wilayani Serengeti mkoani Mara, wamehukumiwa kifungo cha jumla ya miaka 60 jela pamoja na kuchapwa viboko 20 baada ya kupatikana na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Pia, wametakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni mbili kwa kumsababishia madhara mwathirika wa tukio hilo watakapomaliza kifungo chao.

Kesi hiyo ilikuwa ikimkabili, Juma Kunzu na Peter Sahani, wote wakazi wa Wilaya ya Serengeti, baada ya kudaiwa kufanya kitendo cha unyang'anyi wa pikipiki kwenye kijiji cha Musasa, wilayani Chato, mkoani Geita na kufikishwa mahakamani Novemba 22, 2019.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Chato, Erick Kagimbo, baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa na pande zote mbili.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Anosisye Erasto, akishirikiana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Semen Nzigo, walidai mahakamani hapo kuwa, washtakiwa kwa pamoja walitenda kosa hilo Novemba 12, mwaka jana, kwenye Kijiji cha Musasa, wilayani Chato baada ya kumkodi mwendesha bodaboda, Maneno Selemani.

Ilidaiwa kuwa bila kujua kuwa abiria hao wana nia ovu, walimteka Selemani, kisha kumpiga na kitu chenye ncha kali kichwani na kusababisha kuzirai na kumpora pikipiki na kutokomea nayo huku majeruhi wakimtelekeza pembezoni mwa njia.

Baada ya kutekeleza unyang'anyi huo, washtakiwa kwa pamoja waliisafirisha pikipiki hiyo hadi wilayani Serengeti mkoani Mara ambako walikamatwa na polisi na kurejeshwa eneo walikofanya uhalifu huo.

Waendesha mashtaka hao, walidai kitendo cha unyang'anyi wa kutumia silaha ni kinyume na kifungu cha 287 A cha kanuni ya adhabu sura ya 16.

Baada ya mahakama kuwakuta na hatia washtakiwa, upande wa Jamhuri uliiomba kutoa adhabu kali kwa watu hao, kutokana na kukithiri kwa matukio ya unyang'anyi wa bodaboda kila siku.

Wakijitetea, waliomba kupunguziwa adhabu kwa madai ya kuwa na familia na watoto wanao wategemea kuwatunza.

Kutokana na maelezo hayo, mahakama hiyo iliamuru washtakiwa wote kutumikia kifungo cha miaka 30 kila mmoja, kupigwa viboko 10 kila mmoja, pamoja na kulipa fidia ya shilingi milioni moja kila mmoja kipindi watakapo maliza kifungo chao gerezani.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wa dini wachukue hatua zaidi hadhari Pasaka

**WAKATI** waumini wa madhehebu ya kikristo wakijiandaa na sikukuu ya Pasaka nchini, baadhi ya makanisa yametangaza hatua kadhaa za kuchukua kwa lengo la kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Makanisa hayo yametangaza utaratibu huo kwa kuwa kabla ya Pasaka kufanyika ibada kadhaa ambazo uhusisha mikusanyiko ya waumini kuanzia Alhamisi Kuu, Ijumaa Kuu, mkesha wa Pasaka (Jumamosi) na Pasaka yenyewe (Jumapili) na Jumatatu ya Pasaka.

Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar jana lilitangaza kuwa litatumia sehemu kubwa ya ibada ya Pasaka kwa ajili ya kuliombea Taifa kupambana na janga la corona, huku likibadili baadhi ya taratibu kama sehemu ya tahadhari dhidi ya maambukizo.

Askofu wa kanisa hilo, Dk. Michael Hafidh, alizitaja baadhi ya hatua hizo kuwa ni kupunguza mikusanyiko mikubwa inayowakutanisha watu mbali mbali kwa wakati mmoja, na kwamba ibada zote zitafupishwa na mahubiri yasizidi dakika kumi, ambapo pia ibada hazitakuwa na kwaya.

Baadhi ya shughuli zimesitishwa kabisa katika kipindi hichi kuelekea Pasaka ikiwamo mazoezi ya kwaya, madarasa ya kipaimara pamoja na mikesha ya aina zote na tafrija.

Ibada ya Ijumaa Kuu hakutakuwa na njia ya msalaba pamoja na utaratibu wa kubusu msalaba.

Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT), limesema maadhimisho ya Pasaka mwaka huu yataadhimishwa katika makanisa ya mitaa ili kuepuka mikusanyiko.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Kanisa hilo Makao Makuu, Mchungaji Josephales Mtebe, alisema pia hakutakuwapo safari ya kwaya na mialiko ya wahubiri kutoka kanisa moja kwenda lingine.

Nalo Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), limesema wakati wowote kuanzia sasa, litachukua hatua za ziada katika kukabiliana na kasi ya maambukizi ya corona.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa kanisa hilo, Askofu Dk. Frederick Shoo, juzi, na kuwa katika kukabiliana na corona, huenda kanisa likachukua hatua za ziada katika taratibu zake za ibada.

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), lilieleza kwamba Alhamisi Kuu hakutakuwa na kuoshwa miguu wala maandamano ya Ekaristi Takatifu na badala yake Sakramenti Takatifu itahifadhiwa katika tabernakö.

Pia hakutakuwa na utaratibu wa kubusu msalaba na badala yake waumini watainamia msalaba kwa mbali bila kuugusa wala kuushika pamoja na kusitishwa kuwekwa maji ya baraka ya kuchovya katika milango, na waumini hawatakiwi kupeana mikono badala yake wafumbe mikono na kuinamiana waumini watakominika kwa mikono tu.

Aidha, kila muumini kutumia kitabu chake cha ibada na wanaohesabu fedha za matoleo watatumia vitakasa mikono (maji tiba) kujisafisha.

Kadhalika, sakramenti ya kitubio, Padri anayeungamisha asiangaliane na waumini uso kwa uso katika kiti cha kitubio bali maungamo yafanyike sehemu za wazi.


Viongozi wa makanisa haya wamefanya maamuzi mazuri, ingawa ni magumu kwa kuwa lengo ni kuepusha maafa dhidi ya binadamu.

Tunaamini kuwa makanisa yote ya kikristo yataweka na kutangaza kwa umma hatua za tahadhari za kukabiliana na janga la corona lililoitikisa dunia wakati wote wa ibada za kabla na wakati wa Pasaka.

Ni matarajio yetu kuwa waumini wao wataziheshimu taratibu hizo na kuzifuata, kwa lengo la kuepukana na maambukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Likizo ya virusi vya corona iongeze kasi ya kujisomea

SHULE za awali, msingi hadi vyuo vikuu zimefungwa na sasa wanafunzi wako likizo ya ghafla iliyotangazwa na serikali kama njia ya kuepusha maambukizi zaidi ya virusi vya corona nchini.

Shule zilifungwa kuanzia Machi 17, mwaka huu, ikiwa ni maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa Watanzani, huku mikusanyiko mikubwa ya watu nayo ikipigwa marufuku.

Kutokana na likizo hiyo ya dharura, wizara husika iliagizwa kufanya marekebisho ya ratiba ya kidato cha sita ambao wanatarajiwa kufanya mitihani Mei 4 mwaka huu, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanasoma kama ilivyo ada.

Kamba wanafunzi watakuwa na muda mfupi, hivyo itasogezwa mbele kadiri ya matokeo ya kuenea ugojwa huo yatakavyokuwa ili nao wapate nafasi ya kusoma kwa kipindi kile kile kilichokubalika kwa mujibu wa ratiba hiyo.

Hatua hizo zimechukuliwa na serikali baada ya kuwapo kwa wagonjwa wa corona nchini, na hivyo kulazimika kufunga shule kwa muda wa siku 30 ili wanafunzi wawe nyumbani kwao kwa kipindi hicho chote.

Nikirejea katika kile ambacho ninataka kukijadili, ni kwamba ni vyema wanafunzi wakatumia nafasi hii kujisomea, kwa kutambua kwamba hiyo ni likizo ya dharura ambayo haikutarajiwa.

Inawezekana katika mazingira ya udharura, zipo baadhi ya shule ambazo hazikuwapa wanafunzi kazi za kufanyia nyumbani, hivyo wenyewe hawana budi kujiongeza kwa kutumia likizo hiyo kujiongezea maarifa.

Ikumbukwe hata vituo vya masomo ya ziada vilivyopo mitaani ambavyo baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakienda kusoma, navyo vimefungwa, kwa sababu ya tishio la virusi vya corona.

Njia mojawapo iliyobaki ni wanafunzi wenyewe kutumia dharura hiyo kutulia nyumbani na kujisomea kwa bidii na wale ambao wamepewa kazi za nyumbani nao wazifanyie kazi inavyotakiwa.

Ninaamini kwamba wanafunzi wanaojitambua na hasa madarasa ya juu watakuwa wanajua maana ya kujisomea, hivyo likizo hiyo ya dharura nao waitumie kujiongozea kitu kichwani.

Bila kufanya hivyo, likizo hiyo inaweza kiumaliza wakarudi shuleni wakiwa hawana kitu kichwani na bado hali ya hewa kuhusu virusi hivyo vinavyozidi kusambaa nchi mbalimbali haijatulia.

Yawezekana muda uliowekwa na serikali ukaongezwa iwapo hali itakuwa si ya kuridhisha, hivyo suala wanafunzi kutenga muda kujisomea ni la muhimu badala ya kudhani kwamba wamepata muda wa kupumzika.

Kwa wanaotambua umuhimu wa elimu watakuwa wanaumia kutokana na virusi hivyo kusababisha warudi nyumbani, lakini pia inawezekana wapo wanaofurahia kukaa nyumbani badala ya kuwa shuleni wakisoma.

Lakini kwa ujumla ni kwamba suala la kujisomea kwa ajili ya kujiongezea uelewa ni la msingi na ndivyo wanafunzi wanatakiwa kufanya wakati wa likizo rasmi na isiyo rasmi kama ya sasa.

Huu siyo wakati wa kwenda vijiweni kupiga soga, si wakati wa kukaa nyumbani na kuangalia filamu na si wakati wa kuzunguka kwenda kutembelea marafiki, bali ni wa kutulia na kujisomea.

Ni kweli wanafunzi wanatakiwa kufanya shughuli za nyumbani, lakini kutenga muda wa kujisomea ni jambo la muhimu ikiwamo mijadala kuhusu mada zinazotokana na masomo yao.

Mara nyingi ufaulu wa wanafunzi huchangiwa kulingana na jinsi wanavyoipa elimu kipaumbele kwa kuitengea muda wa kutosha wa kujisomea kuliko mambo mengine yasiyo na umuhimu.

Vilevle ufaulu wa wanafunzi unachangiwa na vitu vingi kama mazingira ya mwanafunzi, namna ya ufundishwaji, mundombinu, walimu wa kutosha, ratiba na uhuru wa mwanafunzi katika kujifunza.

Lakini pia wanafunzi wenyewe wanatakiwa kujiongeza kwa kujitengea muda wa kujisomea na siyo kutegemea kufundishwa masomo ya ziada tu au kupoteza muda kwa kufanya mambo yasiyoendana na elimu.

Kwa mfano wapo baadhi ya wanafunzi ambao muda wao mwingi wanautumia kwa kungalia filamu au tamthilia, kuchati au mambo mengine ambayo hayahusiani na elimu.

Hayo yote ni adui wa maendeleo ya elimu, ndiyo maana ninashauri wale ambao kwa sasa wako kwenye likizo ya dharura, waitumie inavyotakiwa na hasa kwa kutenga muda wa kujisomea.

Wanafunzi ambao wamejengewa utaratibu wa kusikiliza maelekezo ya walimu yanayoeleza kwa undani wanachofundishwa na kisha wanauliza maswali na kujadili mada, watakuwa wanaelewa umuhimu wa kujisomea.

## BARUA / MJADALA

# *Corona umetufunza mengi wanadamu*

***MHARIRI***

*Nawapa pole Watanzania kutokana na hofu ya corona ambayo imemfikia kila mmoja.*

*Napenda nisema kuwa dunia ni moja na zile habari kuwa nchi maskini zipo kwenye hatari ya kudhurika na majanga yanayotokea duniani wakati mwingine kisiwe kigezo na madai ya nchi tajiri kuikandamiza Afrika hasa zinapojadili masuala ya maendeleo.*

*Tatizo la corona limedhihirisha kuwa si maskini wala tajiri wote wanakufa na kwamba bila mshikamano na kufanyakazi kwa pamoja hakuna atakayeshinda mtihani wa corona.*

*Kwa hiyo, tunaiomba jumuiya ya nchi zilizoendelea ziachane na dhana kuwa zimefikia kiwango cha juu cha kupevuka kimaendeleo kwa hiyo masuala ya umaskini na shida za Afrika haziwahusu.*

*Ukweli ni kwamba maradhi ya corona yameirudisha dunia kwenye zama za kuwa pamoja na kudumisha mshikamano bila kujali kuwa fulani ni tajiri au maskini.*

*Walioendelea wakumbuke kuwa wamefanya mengi kuidhuru dunia pamoja na Afrika, lakini methali ya mchuma janga hula na wenzake inawahusu pia.*

*Wenzetu hawa wamekuwa wagumu kukubaliana na masuala ya kupunguza joto duniani, wamekuwa wakitupa taka za sumu kwa nchi maskini, lakini pia hata kuifanya Afrika kuwa jalala la vitu wasivyovihitaji hasa vifaa vya kiteknolojia.*

*Corona inaifunza dunia kuwa kila mmoja ni lazima awe raia mwema bila kujali anaishi Afrika au ughaibuni. Umoja na kuujali ubinadamu ndilo funzo wanalolipata wanadamu wakati huu wa corona.*

***Maimuna Mdee***
***Kighare Usangi***
***SLP Mwanga***

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Chunga simu, kompyuta visikuambukize corona

**Na Gwamaka Alipipi**




WAKATI huu dunia nzima ipo katika mapambano ya kuutokomeza ugonjwa wa virusi vya corona na mataifa karibu yote yameathiriwa na maradhi.

Matangazo mbalimbali yamekuwa yakitolewa yanayoelezea namna ya kujikinga ikiwamo kunawa kwa kutumia vitakasa mikono kwa jina maarufu 'sanitizers'.

Lakini wengi wetu tumesahau ana kutojua kwamba simu yako ya mkononi inaweza kuwa hatari katika maambukizi ya ugonjwa huo pindi unapoiweka juu ya meza, ama sehemu yoyote ambayo watu wengi wanakuwa wameshika.

Simu ya mkononi kama kifaa mojawapo cha mawasiliano, kwa sasa ni wakati ambao inatumika sana kupata taarifa zaidi kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona, lakini je, tunahakikisha simu zetu ni safi? Na tunazitunza vizuri ili tusipate maambukizi?

Kitengo cha Serikali ya Marekani kinachoshughulikia masuala la milipuko ya magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention) kinatambua simu kama moja ya kitu kinachoweza kusambaza virusi kwa urahisi.

Ikumbukwe kuwa simu yako ya mkononi unaiweka sehemu mbalimbali, hata ukisalimiana na mtu au kushika vitu mbalimbali mwisho wa siku utaishika simu yako.

Hata wakati wa kuongea na mtu uwe umepiga au umepigiwa kumbuka utaiweka simu kwenye sikio jambo ambalo litakuweka katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Hivyo, wakati wa kipindi hiki kuna mambo unayotakiwa kuyafanya dhidi ya simu yako ya mkononi katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo hatari.

Kwanza, unapaswa kuwa na kitambaa maalumu utakachokuwa unakitumia katika kuifuta simu yako mara kwa mara, kabla na baada ya kuitumia.

Kitambaa hicho hakikisha kinakuwa na unyevunyevu wa dawa ya kuua vijidudu, kisiwe kimelowa sana kwani unaweza kuhatarisha simu yako kufa.

Kiweke katika hali ya usafi muda wote kitambaa hicho, uwe unaifuta simu yako sehemu zote ndani na nje, iache ikauke kidogo ndipo uendelee kuitumia tena, kwa kufanya hivyo utakuwa salama kwa asilimia 90.

Pili, tumia sabuni ya kawaida ya kuogea yenye sifa na uwezo wa kuua virusi na bakteria (zipo nyingi dukani) na zingine za kijamii zenye uwezo wa kuua vijidudu.

Wakati wa kuanza kusafisha simu yako hakikisha mikono yako iko safi ndipo uanze kuchanganya sabuni na maji kidogo.

Chukua kitambaa laini au vile vitambaa vya kusafishia miwani. Kilainishe kidogo na kisha safisha simu yako katika maeneo yote ya nje kwa utaratibu, usitumie nguvu za kusugua.

Kitu muhimu cha kuzingatia sana ni kuepuka kushika simu/kifaa cha kidigitali ambacho siyo chako, hata kama simu ni ya mpenzi wake ama mke wako au mume wake achana nayo kwa kipindi hiki, ikimbie kama ukoma.

Ule msemo kuwa huyu ni mwenza wangu niko tayari kufa naye, kwa sasa uweke kando kwani ugonjwa huu ni hatari kwa watu wote, mnaweza kufa nyie lakini mkaacha balaa kwa wengine mliowahi kuchangamana nao.

Wakati huu si wa kuaminiana kuwa mwenzangu hana virusi vya corona basi itakuwa si vibaya nikitumia simu yake au kifaa kingine cha kidigitali kwa lengo la kufanya mawasiliano ama kwa sababu nyingine kwani haujui kifaa hicho ni kisafi kiasi gani kutokuwa na vrusi hivyo.

Tumia simu yako ya mkononi katika kufanya miamala kwa njia ya kielektroniki, lipa bili mbalimbali kwa kutumia simu yako kuliko kulipa kwa 'cash'.

Ni vyema tukawa wapenzi wa kutumia mitandao yetu ya simu au hata benki mtandao kuweza kufanya manunuzi/malipo ya vitu mbalimbali jambo ambalo linafanya kitendo cha kufanya malipo kwa pesa mkononi ili kupata huduma hivyo kuepuka watu kugusana.

Kwa wafanyakazi wa maofisini ni wakati wa kuhakikisha vifaa vya kidijitali kama vile kompyuta mpakato 'laptop' au kompyuta za kawaida ukakitumia peke yako, usiruhusu kuchangia kwani ushikaji wa kipanya au 'mouse' na 'keyboard' kwa watu wengi kunaweza kuchangia kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo hatari.

Huu ni wakati wa wafanyakazi katika maofisi kutumia kadi kufungulia mlango katika maofisi kuliko kutumia milango ya kusukuma, hiyo itasaidia kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Mwisho, kila Mtanzania anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzake katika mapambano ya ugonjwa huu, kufuata masharti ya wataalamu wa afya yanayotolewa.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Mahakama yatoa mbinu za kuepukana na corona

**Mwandishi Wetu**

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amewataka mahakimu kusikiliza kesi za jinai kwa mfululizo ili kupunguza msongamano wa mahabusi ikiwa njia mojawapo ya kuepukana na maambukizo ya virusi vya corona.

Dk. Feleshi alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea mahakama mbalimbali za Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi maalum.

"Anzeni kusikiliza kesi za jinia mfululizo. Hii itasaidia tusiwe na msongamano wa mahabusi na wale wanaostahili dhamana wapewe. Hatua hii itatuwezesha kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona," alisema Jaji Kiongozi.

Pia Jaji Kiongozi amewataka watumishi wa mahakama kuendelea kuepukana na vitendo vya rushwa na kuzingatia maadili ya kazi zao.

Kadhalika Dk. Feleshi alizipongeza Mahakama za Mwanzo kutokuwa na mrundikano wa mashauri.

Jaji Kiongozi ameanza ziara ya ukaguzi maalum katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ambayo inatarajiwa kumalizika Aprili 3, mwaka huu.

Katika ziara hiyo, Jaji Kiongozi alikagua ujenzi wa jengo la Kituo cha Mahakama Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC) kilichoko Kinondoni.

Pia alikagua Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Mahakama ya Wilaya Kinondoni na Mahakama za Mwanzo za Sinza, Kinondoni,Kawe, Kimara, Magomeni na Kariakoo.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wakinunua mahitaji katika gulio la Jumatatu, eneo la Msikiti Mkuu wa Ijumaa, Muheza mjini jana, ambapo wakulima kutoka vijijini hupeleka mazao yao na kuyauza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Takukuru yamsafisha Prof. Kitila Mkumbo

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imekanusha kusambaratisha mkutano unaodaiwa kuitishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo wilayani Iramba mkoani Singida.

Inadaiwa kuwa mkutano wake huo, ulihusisha wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa lengo la kutoa rushwa ya kushawishi kuungwa mkono katika mbio za kuwania ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, taarifa hiyo ya uongo ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii juzi kuwa Takukuru ilisambaratisha mkutano huo.

"Takukuru inapenda kuufahamisha umma kuwa yaliyoandikwa katika taarifa hiyo ambayo ilikuwa ikisambazwa katika mtandao wa kijamii wa Facebook siyo ya kweli," alisema na kuongeza:

"Takukuru inapenda kukanusha taarifa ambayo ilikuwa ikieleza kuwa tumesambaratisha mkutano wa Prof. Mkumbo na wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM Wilaya ya Iramba, mkoani Singida."

Alisema taarifa hiyo ambayo siyo ya kweli na wanaendelea kuchunguza chanzo chake ili kubaini aliyehusika na uhalifu huo. Alisema taarifa hiyo ilidai kuwa katika mkutano huo Prof. Mkumbo alitoa hongo ya Sh. 50,000 kwa kila mjumbe kwa lengo la kuwashawishi wamchague muda wa uchaguzi utakapofika, na kwamba mkutano huo ulisambaratishwa na Takukuru mkoani humo.

"Tunapenda wananchi wote wafahamu kuwa Takukuru ni chombo kinachotambua majukumu yake na kinafanya majukumu hayo kwa mujibu wa sheria. Tunatoa rai kwa wananchi wote kutojihusisha na kusambaza taarifa ambazo siyo za kweli kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Mitandao ya mwaka 2015," alisema Jenerali Mbungo.

# Maombi kutaifishwa bil. 16/- Aprili 3

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi maarufu 'Mahakama ya Mafisadi', imepanga kutoa uamuzi Aprili 3, mwaka huu dhidi ya maombi ya kutaifisha zaidi ya Sh. bilioni 16 yaliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Amri hiyo ilitolewa jana na Jaji Elinaza Luvanda, baada ya kusikiliza maombi yaliyowasilishwa na DPP chini ya kiapo cha Wakili wa Serikali, Esterzia Wilson na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, (SSP), Fadhili.

Jopo la Mawakili wa Serikali likiongozwa na DPP akisaidiana na Mawakili wa Serikali Wakuu, Shadrack Kimaro na Christopher Msigwa.

Katika maombi ya msingi, DPP amefungua kesi Mahakama ya Mafisadi akiomba akaunti za washtakiwa Rais wa Ujerumani Manon Huebenthal, Rais wa Uingereza, Frank Rickeltis na Kampuni ya IMS Marketing Tanzania Ltd zilizopo katika Benki ya Boa zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Kwa mujibu wa hati ya maombi hayo, DPP, Februari 11, 2019 alifungua kesi ya jinai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam dhidi ya washtakiwa wa kwanza na wa pili, wakikabiliwa na mashtaka ya kula njama, kuendesha upatu na kutakatisha fedha.

Hata hivyo, kesi hiyo ya jinai Machi 15, 2019 Mahakama ya Kisutu ilitoa amri ya kukamatwa washtakiwa.

Katika hati ya maombi hayo, ilidaiwa washtakiwa walifika nchini na kuanzisha kampuni ya IMS Marketing Tanzania Ltd Novemba 19, 2014 na kupewa usajili namba 113132.

Mshtakiwa wa kwanza na wa pili walikuwa wakurugenzi na wanahisa, lakini kuendesha upatu haikuwa mojawapo ya shughuli za kampuni hiyo.

Ilidaiwa washtakiwa walianza kutia saini nyaraka mbalimbali kwa wanasheria na kwamba Aprili 23, 2015 walifungua akaunti za Dola za Marekani mbili tofauti na Machi 3, 2016 akaunti ya Euro katika Benki ya Boa.

Washtakiwa walipata leseni ya biashara iliyotolewa na Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya masoko.

Kampuni hiyo ina mahusiano na Kampuni ya IMS International Marketing Services imesajiliwa na inafanya kazi zake Singapore.

Ilidaiwa kampuni hizo mbili zina mahusiano ya karibu na ni sehemu ya Kampuni ya Onecoin Ltd ambayo ilianzishwa Aprili, 2014 huko Gibraltar na ilianzishwa ofisi nchini Bulgaria, Falme za Kiarabu na Hong Kong.

DPP alidai kuwa Onecoin Ltd inajihusisha na masuala ya upatu kwa kushirikiana na Kampuni za IMS ambalo ni kosa tangulizi la kutakatisha fedha. Ilidaiwa mahali tofauti kampuni ya Onecoin na kampuni zake tanzu na akaunti zilizokuwa hazijaingizwa fedha za upatu zilikamatwa kwa sababu zilihusishwa na kutakatisha fedha.

Ilidaiwa katika akaunti za mitandao ya jamii za Kampuni ya Onecoin ilitangazwa kwamba wateja wake wanaweza kuendelea kutoa michango yake kupitia akaunti zilizopo benki ya Boa.

Ilidaiwa kwa nyakati tofauti akaunti mbili zilizopo benki ya Boa za Dola za Marekani ziliingizwa Dola 1,337,965.90 na 15,631.97 na Euro 5, 442,020.05.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa wa kwanza na wa pili walianza kulipwa. Kati ya Novemba 18,2015 na Juni 31,2016 zililipwa Dola za Marekani 61,643.84 kwa Kampuni ya IMS International.

HABARI KITAIFA

## Benki ya UBA yaipatia serikali mil. 230/- corona

**Na Romana Mallya**

BENKI ya UBA Tanzania, imetoa Sh. milioni 230 kwa serikali ili zisaidie juhudi za kupambana na virusi vya corona.

Msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na UBA Tanzania ambayo ni kampuni tanzu ya UBA Group na kuukabidhi kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa UBA Tanzania, Usman Isiaka, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuiwezesha serikali katika juhudi zake za kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa vifaa vya kukabiliana na ugonjwa huo.

"Ukweli ni kwamba serikali zote duniani hivi sasa zimebebeshwa mzigo mkubwa wa uhitaji wa vifaa muhimu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona," alisema.

Alisema UBA Tanzania imejipanga kuhakikisha inachangia pakubwa katika kuchangia juhudi za serikali zenye lengo la kuboresha mazingira ya biashara nchini kwa faida ya uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla.

Alisema mchango walioutoa ni sehemu ya jumla ya Dola za Kimarekani milioni 14 ambazo UBA Group itatoa kwa jumla ya nchi 14 za Afrika.

"Fedha hizi hutolewa kupitia Mfuko wa UBA (UBA Foundation), benki yetu inaamini kuna kila sababu ya kushiriki katika mapambano dhidi ya janga hili ili kila mtu awe salama," alisisitiza.

Alisema wanapongeza juhudi ambazo tayari serikali imezichukua mpaka hivi sasa.

"Tumeamua kuongeza juhudi zetu kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunalimaliza tatizo hili," alisema.

Mkurugenzi asiye Mtendaji wa UBA, Farhiya Warsame, alisema corona ni janga la dunia na hivyo ni lazima wadau waungane na serikali katika juhudi za kulitokomeza.

Waziri Mkuu Majaliwa, ambaye ndiye mwenyekiti wa kamati ya kitaifa ya kupambana na Covid- 19, aliishukuru UBA Tanzania kwa msaada huo.

Alisema serikali itahakikisha unatumika kwa kazi iliyolengwa ili kuongeza juhudi za kupambana na janga hilo.

UBA Group inafanya biashara katika nchi 20 za Afrika na inapatikana katika nchi za Uingereza, Marekani na Ufaransa.

# Diwani ahofia mlipuko kipindupindu Shinyanga

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

DIWANI wa Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, amesema anahofia kutokea mlipuko wa kipindupindu katika manispaa hiyo kutokana na kukithiri kwa mrundikano wa uchafu.

Alibainisha hayo kwenye kikao cha Baraza la Maalumu la Madiwani Manispaa ya Shinyanga, lililokuwa na ajenda ya kujadili taarifa ya maandalizi ya miradi mitatu itakayo fadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), ambayo ni ujenzi wa soko, stendi ya mabasi na ujenzi wa kilomita 18 za barabara ya kiwango cha lami.

Alisema Manispaa ya Shinyanga ipo katika hatari ya mlipuko wa kipindupindu kutoka na uchafu kikithiri kwenye maghuba, huku mwingine ukianza kutoa funza, hivyo kuhatarisha afya za wananchi.

"Manispaa ya Shinyanga kwa sasa hali ni mbaya sana, uchafu umekithiri sana kwenye maghuba na sasa hivi tunapambana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, huku kipindupindu nacho kinapiga hodi," alisema.

"Hili litakuja kutugharimu, nadhani mnakumbuka kipindi cha nyuma tulishatumia milioni 30 kwa ajili ya kipindupindu," alisema Nkulila.

"Mimi nimekagua baadhi ya maghuba na yameanza kutoa funza kabisa, nimepiga hadi na picha kama ushahidi wangu, hali ni mbaya sana," alisema na kuongeza:

"Na watoto wanakwenda kuchezea uchafu huo, hivyo naomba uongozi wa Manispaa muutoe uchafu ili kunusuru afya za wananchi."

Naye Diwani wa Kambarage, Hassani Mwendapole, alisema hali ya uchafu ni mbaya, na kwamba mzabuni aliyepewa kazi ya kusomba uchafu kwenye makazi ya watu na kuupeleka kwenye maghuba ameizidi Manispaa ya Shinyanga ambayo inapaswa kuutoa uchafu huo na kuupeleka dampo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geofley Mwangulumbi, alikiri uchafu kujaa kwenye maghuba, na kutolea ufafanuzi tatizo limetokana na mtambo wa kuzolea uchafu kuharibika, na wanachokifanya kwa sasa ni kutumia watu kuuzoa uchafu huo kwa kutumia makoleo, na ndio maana kasi imekuwa ndogo ya uzoaji taka.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, akiwaonyesha waandishi wa habari jijini humo jana, gari aina ya BMW ambayo inadaiwa kuingizwa nchini kinyume cha sheria na kukwepa kulipa kodi zaidi ya Sh. milioni 10, watuhumiwa wawili wanashikiliwa na jeshi hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 7/- zahitajika Tarura kujenga daraja la Berega

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI ya Mkoa wa Morogoro kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), inahitaji zaidi ya Sh. bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Berega wilayani Kilosa, ambalo lilikatika kufuatia mafuriko.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alisema hayo wakati akikagua ujenzi wa daraja hilo ambalo linaunganisha na vijiji kadhaa na Hospitali ya Berega, wilayani Kilosa.

Alisema hayo wakati akitekeleza agizo la Rais Dk. John Magufuli, alilolitoa Machi 16, mwaka huu, ambalo anapaswa kusimamia ujenzi wa daraja hilo ndani ya siku saba ili magari na wananchi waweze kuendelea kulitumia.

Mhandisi Kalobelo alisema, zinahitajika Sh.i bilioni saba ili kuwezesha kujengwa daraja kubwa jipya hapo baadaye fedha hizo zitakapopatikana.

Alisema, kwa sasa daraja lililojengwa ni kuwawezesha wananchi wa vijiji vya kata ya Barega na vingine wawe na mawasiliano ya barabara kutoka upande mmoja kwenda mwingine kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii.

"Ili daraja hasa linatumiwa na watembea kwa miguu na pikipiki na linaendelea kuimarishwa ili kupitisha magari yenye uwezo wa tani tatu hadi 3.5 kuanzia Machi 28, mwaka huu," alisema Mhandisi Kalobelo.

Aliwataka wataalamu wa Tarura wa mkoa huo, kufanya ukaguzi wa madaraja mara kwa mara ili kuepuka changamoto ya ukosefu wa mawasiliano baina ya sehemu moja na kwenda nyingine.

Naye Meneja wa Tarura Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Benjamin Maziku, alisema daraja la Barega lilipojengwa mwaka 2013 lilikuwa ni la muda baada ya lililokuwapo awali kusombwa na maji.

Alisema daraja hilo lina historia ya maji ya mafuriko kusomba magogo na hivyo katika ujenzi wake daraja litajengwa kwa nguzo nne na litanyanyuka juu zaidi ili kupitisha magogo na kuepusha kuziba wakati wa mvua.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi waliokuwapo katika daraja hilo kwa nyakati tofauti wamepongeza hatua za serikali kusaidia ujenzi wa daraja hilo, ambalo limekuwa kero kwa muda mrefu na wakati mwingine kushindwa kuvusha wagonjwa kwenda Hospitali ya Berega.

Machi 16, mwaka huu wananchi waliofika eneo la daraja la Kiyegeya, ambalo Rais alitembelea, walipewa fursa kutoa hoja na changamoto zao na mmoja alieleza kero ya muda mrefu ya kukosekana daraja la kuwaunganisha na hospitali tegemeo kwao ya Berega.

Kutokana na hoja ya mwananchi huyo Rais alimpa siku saba Meneja wa Tarura Wilaya ya Kilosa kujengwa kwa daraja hilo ndani ya siku hizo na pia Katibu Tawala wa mkoa huo kusimamia ujenzi.

# Takukuru yachunguza viongozi Mvomero tuhuma za ubadhirifu

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Mvomero, inafanya uchunguzi kwa viongozi watatu wa kata ya Mlali kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za wananchi zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa vibanda vya biashara katika soko la Mlali.

Mkuu wa Takukuru Wilaya ya Mvomero, Eufrasia Kayombo, alisema hayo wakati akitoa taarifa fupi kwenye mkutano wa hadhara wa wananchi wa kijiji cha Mlali mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Mohamed Utaly, aliyeambatana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

Mkutano huo ulitumika pia kwa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo kufanikisha urejeshwaji wa fedha kwa wananchi waliodhulumiwa haki zao Sh. milioni 3. 4 na kukabidhiwa kwa mwenyekiti wa kijiji hicho yakiwa ni malipo ya vibanda.

Alisema uchunguzi wa Takukuru umegundua kuwa viongozi ambao ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mlali, Hussein Mtogole, Ofisa Mtendaji kata hiyo, Annuciatha Mpina na Ofisa Ugani Paul Kato walikiuka maelekezo yaliyotolewa na Baraza la Maendeleo la Kata.

Kayombo alisema, uchunguzi huo ulibaini viongozi hao waliamua kuuza maeneo hayo kwa baadhi ya wananchi kinyume na utaratibu.

Alisema, viongozi kupitia kikao cha Baraza la Maendeleo la Kata walikubaliana kuwa wananchi wasichangishwe fedha za kujenga vibanda vya biashara bali mwananchi mwenye nia ya kujenga apewe vibanda bure na kuvijenga kwa lengo la kuboresha mazingira ya soko.

"Uchunguzi umethibitisha kuwa Sh. 3,400,000 zilitolewa kutoka kwa wananchi na kukabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji Hussein Mtogole ikiwa ni malipo ya vibanda," alisema Kayombo.

Pia, alisema katika uchunguzi huo imethibitika kuwa fedha hizo hazikuingizwa katika akaunti ya halmashauri ya kijiji wala akaunti ya kata.

Alisema, uchunguzi umethibitisha pasipo shaka kuwa watuhumiwa walikiuka utaratibu na kutenda kosa la ubadhirifu wa fedha za wananchi kinyume na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mkuu wa Takukuru Wilaya ya Mvomero, alisema uchunguzi umethibitisha pasipo shaka na Takukuru ilifanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha kutoka kwa watuhumiwa hao na kurejesha kwa wananchi waliodhulumiwa haki zao.

Alisema, wananchi saba wamerejeshewa fedha zao mbele ya mkuu wa wilaya na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya kulingana na viwango walivyotoa kwa viongozi wa kata hiyo.

Mkuu wa wilaya hiyo akizungumza na wananchi katika mkutano huo, aliipongeza Takukuru kwa kazi nzuri waliyofanya ya uchunguzi na kuleta matokea chanya kwa wananchi.

Utaly, aliwataka wananchi waendelee kuiunga mkono serikali katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kukataa kutoa na kupokea rushwa na pia kuwafichua wote wanaoendekeza vitendo vya rushwa.

Pia, aliwataka wananchi kuwa tayari kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili kuviwezesha kufanya kazi nzuri na kuleta matokeo chanya kwa jamii.

"Nashukuru wananchi wote ambao mlitoa ushirikiano kwa Takukuru na kuwezesha kuokoa kiasi hiki cha fedha ambacho kilikuwa tayari kimefanyiwa ubadhirifu na viongozi," alisema Utaly.

Aliwataka wananchi waliorejeshewa fedha kuwa mstari wa mbele kufichua viongozi wala rushwa kwa kutoa taarifa kwa Takukuru kwa wakati.

Nao miongoni mwa wananchi saba waliorejeshewa fedha zao, Magdalena Fabian, aliyepokea Sh. 300,000 na John Vincent, aliyepata Sh. 800,000, kwa nyakati tofauti waliipongeza Takukuru kwa kuwajali watu wanyonge hadi kufikia kurejeshewa tena fedha zao.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kulia), akikagua ubora wa kifaa cha kutenganishia mifereji ya kupitishia maji ili kuepusha upasukaji, wakati alipofanya ziara katika skimu ya umwagiliaji wa Kigugu, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, juzi. **PICHA: WK**

## Wakazi wa Magu wapewa angalizo athari za corona

**Na Anthony Gervas, MAGU**

HOSPITALI ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, imewatahadharisha wananchi na watendaji wa serikali, kuacha kuchukulia mzaha suala la kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Mganga Mkuu Mfawidhi wa Wilaya wa hospitali hiyo, Dk. Benard Maduhu, alitoa tahadhari hiyo juzi kwenye kikao cha baraza la madiwani katika halmashauri ya wilaya hiyo.

"Ugonjwa wa corona ni hatari na tishio, hivyo wananchi na watendaji wa serikali msichukulie mzaha katika kuchukua hatua za kujikinga, kunawa mikono kila mara na sabuni ya maji yenye vimiminika vya dawa kwenye maeneo yote ya huduma za kijamii, ikiwamo migahawa, hoteli na maduka," alisema Dk. Maduhu.

Dk. Maduhu alisema watu wanatakiwa kujiepusha na kushikana mikono, kushika vitu kama milango, meza, nguo, na kuwataka kutoa taarifa kwenye idara ya afya wanapoona kuna dalili za mgonjwa wa aina hiyo.

Alisema hospitali hiyo imetenga vyumba maalum vinne vya kuwahudumia washukiwa wa ugonjwa huo, hivyo wasihofu huduma zinaendelea kama kawaida.

Alisema watu wenye urahisi wa kuambukizwa na virusi hivyo ni wazee na watoto wadogo, lakini kubwa zaidi ni wale wenye ugonjwa wa moyo, kifua kikuu, magonjwa sugu ya mapafu na mapafu yenye nyuzinyuzi.

Magonjwa mengine ni presha, ugonjwa wa saratani ambao asilimia 11 wanafariki dunia, huku asilimia tisa ya wagonjwa wa kisukari wanafariki dunia kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

**Dk. Maduhu alisema watu wanatakiwa kujiepusha na kushikana mikono, kushika vitu kama milango, meza, nguo, na kuwataka kutoa taarifa kwenye idara ya afya wanapoona kuna dalili za mgonjwa wa aina hiyo.**

# Vipande vya sabuni vyahamasisha wajawazito kuhudhuria kliniki

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAJAWAZITO katika kijiji na kata ya Mapamba, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, hawahudhurii kliniki mpaka wapatiwe kipande cha sabuni cha kufulia nguo zao.

Muuguzi wa Zahanati ya Mapamba, Jesca Ibrahimu, alisema hayo wakati alipotembelewa na maofisa wa shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Red Cross Society, walipofika kutoa elimu na vipeperushi vyenye ujumbe wa namna ya kupambana na corona.

Alisema, hapo awali walikuwa wakiwapatia wajawazito kipande kimoja cha sabuni ya kufulia na walikuwa wakihudhuria kliniki kwa wakati na kwa wingi, lakini baada ya kusitisha utoaji wa vipande hivyo, wanaohudhuria ni wachache ikilinganishwa na idadi ya wajawazito.

Alisema wanawake wanaofika katika zahanati hiyo kujifungua wengi hawana kadi za kliniki na wengine huja siku moja kuchukua kadi na siku inayofuata hujifungua hali ambayo inawawia vigumu kutambua maendeleo ya mtoto anapokuwa tumboni.

"Mwanzo tulikuwa tunawapatia kila mmoja kipande kimoja cha sabuni ya kufulia, baada ya kusitisha utoaji wa vipande hivyo, mahudhurio ya kliniki yalishuka kwa kasi na mpaka sasa wanahudhuria siku moja kabla ya kujifungua au wakija kujifungua," alisema Ibrahimu.

"Ili tudhibiti vifo vya wajawazito kwa kata hii, mashirika kwa kushirikiana na halmashauri kuangalia namna ya kuendelea kugawia vipande vya sabuni kwa wajawazito ambavyo vinawatia hamasa ya kuendelea kuhudhuria kliniki kwa ajili ya usalama wa mtoto tumboni.

Hata hivyo, alisema wanatoa elimu kwa umuhimu wa kuhudhuria kliniki na kujifungulia zahanati au vituo vya afya vilivyo jirani yao hasa wakati wa utoaji wa chanjo au kwenye vikao vya chama vinapoitishwa.

Pia alisema, wanatumia wenyeviti wa serikali za mitaani kuanzia ngazi za vijiji hadi kata kuwahamasisha kinamama wanapojigundua kuwa na dalili za ujauzito kuanza kliniki mara moja kwa ajili ya usalama wake na mtoto.

# Wafanyabiashara wa madini wakwepa jela

Na Allan Isack, ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imewatia hatiani wafanyabiashara wawili wa madini ya tanzanite kwenda jela miezi 24 au kulipa faini jumla ya Sh. milioni 163, kwa kosa la kufanya biashara bila leseni na kuuza madini nje ya soko lililotengwa na serikali.

Hata hivyo, wafanyabiashara hao, Sanare Saireku (43) maarufu kwa jina la Muller mkazi wa Kata ya Moita Bwawani wilayani Monduli na Lanaito Loiko (51), mkazi wa Nadosoito wilayani Simanjiro, walilipa fedha hizo hivyo kukwepa kwenda jela.

Muller ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Muller Gems Stone na mwenzake Loiko, ambao ni ndugu, walikutwa na hatia baada ya kukiri makosa mbele ya Hakimu Mfawidhi Martha Mahumbuga, aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo.

Katika shtaka la kwanza lililosomwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Innocent Njau, Muller alidaiwa kuwa Machi 14, mwaka huu, maofisa wa Wizara ya Madini, walifika ofisini kwake Kaloleni, katika jengo na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na hakuwa na kumbukumbu cha kiasi cha madini aliyo nayo na pia kushindwa kuwasilisha nyaraka hizo wizarani.

Shitaka la pili, Muller alidaiwa kuwa Machi 15, mwaka huu, katika ofisi yake alishindwa kutunza madini ya tanzanite kilogramu 45.3 na kareti 19.3 yenye thamani ya dola za Kimarekeni 751 sawa na Sh. milioni 1.7) katika kisha maalumu kinyume cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2018.

Mshtakiwa wa pili, Laitoi Loiko, alidaiwa kukutwa na madini ya tanzanite yenye uzito wa kilogramu 269.5 yenye thamani ya dola za kimarekani 20,500 sawa na zaidi ya Sh. milioni 47, akiuza nje ya soko la madini katika bar ya Uzunguni City Park katikati ya Jiji la Arusha, wakati akijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Kutokana na kukiri makosa hayo, katika shtaka la kwanza, Muller alihukumiwa kwenda jela miezi sita au kulipa faini ya Sh. milioni 10 na shtaka la pili kwenda jela miezi sita au kulipa faini ya Sh. milioni 10 kama sheria inavyoelekeza.

Pia hakimu alimtia hatiani mshtakiwa, kwenda jela miezi 12 au kulipa faini ya Sh. milioni 143 kwa makosa mawili, moja kufanya biashara bila ya kuwa na leseni, la pili kufanya biashara nje ya soko la madini lililotengwa na serikali.

Washtakiwa walilipa faini mahakamani hapo kwa 'code' namba maalumu ya benki inayotumika kulipia faini na walilipa jumla ya Sh. milioni 163 na kuachiwa huru.



Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Zakia Mohamed, akitoa mada kuhusu ugonjwa wa corona kwa maofisa ustawi na maendeleo ya jamii wa Mkoa wa Arusha, juzi. **PICHA: WAMJW**

## Vijana kunufaika uvuvi na mifugo

Na Allan Isack, ARUSHA

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania watanufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo ili kujikwamua kiuchumi.

Lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo ni kutawasaidia vijana kujiajiri kupitia shughuli za uvuvi na mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo uliofanyika jijini hapa, Rais wa Mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya umri wa miaka 35 kutoka mikoa hiyo, watanufaika na mtandao huo, kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji na uvuvi.

Boaz alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo ni kuhamasisha vijana kujiajiri katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kutumia njia za kisasa ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Rais huyo alisema walianzisha mtandao huo baada ya kuona kuwa kuna mwanya wa kimaendeleo kati ya wazee na vijana .

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa vijana namna ya kufuga kisasa, na vijana waliopo vijijini ambao hawakupata maarifa ya mtandao huu watanufaika wote," alisema Boaz.

Alisema mtandao huo, ulianzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017 lengo likiwa kupanua wigo kwa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Umoja wa Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR) .

Aidha, alisema mtandao huo, umewashirikisha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa dhamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe ambapo vijana hao kupitia mtandao huo watawekwa pamoja na kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

# Pampu umwagiliaji kuwanufaisha wakulima 15,000

Na Allan Isack, ARUSHA

ZAIDI ya wakulima 15,000 wa mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Singida, wataondokana na adha ya kusubiri kilimo cha msimu wa mvua, baada ya kampuni ya IYO ya jijini Arusha, kuanza kusambaza pampu za umwagiliaji.

Pampu hizo, zitatumia nishati ya jua katika maeneo mbali mbali ya mikoa hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko na Uendeshaji wa Kampuni ya IYO Solar Pump Group, Abdul Sariko, alisema bodi ya wakurugenzi ya kampuni hiyo, imelenga zaidi kumkomboa mkulima wa hali ya chini kulima kisasa kwa kutumia pampu za jua kumwagilia mazao mashambani na gharama yake ni nafuu kwa mkulima wa hali ya chini.

"Pampu hizi tumeshasambaza kwa zaidi ya wakulima 15,000. Tunaamini itakuwa njia mojawapo ya kumwondoa mkulima katika kilimo cha kizamani kwenda katika kilimo cha kisasa na kuacha kutegemea kilimo cha mvua pekee yake," alisema.

Sariko alisema uwezo wa pampu hizo ni mkubwa kwa kuwa moja ina uwezo wa kusambaza maji lita 40,000 kwa saa, hivyo kilio cha wakulima kutegemea mvua kwa sasa kitakuwa historia na nchi itakuwa na mavuno ya kutosha ya chakula katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo.

Alisema kwa sasa kampuni imejikita katika mikoa ya kaskazini, lakini lengo lao ni kusambaa mikoa mingine kama moja ya njia ya kuisaidia serikali kuboresha kilimo nchini kuwa cha kisasa.

"Tumeshasambaza pampu hizi katika wilaya za Same, Mwanga, Simanjiro, Arumeru na Singida na mahitaji ni makubwa sana na tutajitahidi kukidhi mahitaji hayo," alisema Sariko.

Obed Mawalla, alisema ameshanunua pampu hiyo na ameipeleka kijijini kwao Marangu mkoani Kilimanjaro, inafanya kazi vizuri ya kumwagilia mahindi na migomba na imestawi tofauti na awali alipokuwa akitegemea mvua.

Mawalla alisema pampu hizo ni mkombozi wa wakulima na wataacha kutegemea mvua.

"Naishukuru kampuni kwa kubuni kitu kama hiki ambacho mkulima alikuwa akiteseka katika kilimo cha kutegemea mvua na kwa hali hiyo, nchi itapata mazao mengi sana, kama mashine zitasambazwa nchi nzima," alisema Mawalla.

Elias Qorro mkazi wa Karatu, aliishauri serikali kuipa nguvu kampuni hiyo, kusambaza pampu hizo kila wilaya nchini ili ziwasaidie wakulima katika kilimo cha kisasa kuliko kutegemea mvua peke yake.

Qorro alisema amenunua pampu hiyo na ameona faida yake na iwapo wakulima nchini, watazinunua, sekta ya kilimo itainuka na serikali haitakuwa na tatizo katika suala la chakula.

Hata hivyo, alisema serikali inapaswa kutoa nguvu kwa kampuni hiyo, ili kufanikisha jukumu la kusambaza mashine za kisasa kwa wakulima vijijini.



# Mvua Siha yasababisha daraja kushindwa kupitika

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

MVUA kubwa ya msimu wa masika inayoendelea kunyesha katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro juzi, imesababisha baadhi ya wananchi wa Kata ya Donyomoruwa kushindwa kwenda kwenye nyumba za ibada kuabudu kutokana na daraja la Donyo kujaa maji na kuziba eneo la kuvukia.

Hali hiyo imewafanya wananchi hao kuiomba serikali kuwaepushia adha hiyo inayotishia uhai wao kutokana na kiwango kikubwa cha maji kujaa na kutapika kwenye kingo za mto huo.

Jana, baadhi ya wakazi wa Donyomoruwa akiwamo Ivan Losekuu ambaye ni Mwinjilisti wa Kanisa la Free Pentecostal Church of Tanzania, alisema shughuli mbalimbali zikiwamo za usafiri na uchukuzi zimekatishwa kutokana na mvua kubwa kujaza mto huo juzi.

"Wananchi wanaotumia usafiri wa umma kwa ajili ya kuwahi kwenye majukumu yao walilazimika kutembea umbali mkubwa kuzunguka, lakini kibaya zaidi huwa tunategemea kuvuka kwa miguu kwenda ng'ambo. Hali ni mbaya, tunaomba tujengwe daraja," alisema Losekuu.

Loveness Mafie alisema yeye na familia yake walishindwa kwenda kuabudu Jumapili ya juzi, kutokana na maji kujaa katika mto Donyo ambao wanautumia kuvuka kwenda upande wa pili.

Wiki iliyopita, wakazi wa kata hiyo pia walilalamikia hali hiyo kuhatarisha maisha yao, hasa kipindi hiki cha mvua za msimu wa masika kutokana na kukosa kivuko kwa zaidi ya miaka 26 sasa.

Walidai kuwa wananchi wengi wanalazimika kupita barabara ya kuzunguka vijiji jirani ambako kuna umbali mrefu na kutumia gharama kubwa za nauli.

Diwani wa Kata ya Donyomoruwa, Lwite Ndosi (CCM), alinukuliwa na gazeti hili akisema ni kweli kumekuwa na tatizo la kukosekana daraja hilo na kusababisha mahitaji yao ya msingi kukwama.

"Sisi wananchi wa Donyomoruwa tunategemea hospitali, shule pamoja na huduma zote muhimu kutoka maeneo ya jirani ya mji wa Bomang'ombe uliopo Wilaya ya Hai, na kote huko tunapaswa kuvuka mto Donyo. Niungane na wananchi kuomba Halmashauri ya Wilaya ya Siha kuyafanyia kazi kwa haraka malalamiko haya na kuja na ufumbuzi wake," alisisitiza Ndosi.

Kwa mujibu wa diwani huyo, gharama za ujenzi wa daraja hilo kwa mwaka 1993 lilikadiriwa kujengwa kwa Sh. milioni 10, huku tathmini ya ujenzi kwa mwaka huu wa fedha zikiwa zinakadiriwa kufikia Sh. milioni 500.

# Swahiba wa Komu atoa ya moyoni

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

SWAHIBA wa zamani wa kisiasa wa Mbunge wa Moshi Vijijini (Chadema), Anthony Komu, amesema uamuzi wa kiongozi huyo kuwaacha njia panda wananchi wa jimbo hilo, huku akiwa hajatekeleza ahadi zake za uchaguzi mkuu uliopita, haujawaridhisha wananchi.

Rafiki huyo ambaye kwa sasa ni kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi, Deo Mushi, alikuwa meneja wa kampeni wa Komu mwaka 2015.

"Kwa nafasi yake (Komu) katika Jimbo la Moshi Vijijini hajaridhisha wananchi, kwa sababu aliahidi mambo mengi katika ahadi zake na wananchi walitaka kuona ametekeleza na hajafanya hivyo. Lakini pia najua amehama huko kama mimi kwa kukosa ushirikiano. Tunamtakia kila la kheri kwa safari yake aliyoianza," alisema.

Katika mitandao ya kijamii jana, baadhi ya wananchi wa Moshi Vijijini, walikuwa wakieleza mtazamo wao kuhusu uamuzi wa Komu, baadhi wakionyesha hisia zao kuwa jambo hilo pia huenda linatokana na kukata tamaa kutokana na uhusiano mbaya kati yake na wapigakura.

Juzi, Komu alitangaza uamuzi wake wa kuondoka Chadema kutokana na kukatishwa tamaa na tuhuma za usaliti zinazomkabili kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Komu alisema ataondoka rasmi Chadema, baada ya kumaliza muda wake wa ubunge kwa kuwa bado atahitaji ushirikiano wa chama hicho jimboni, kabla ya kumaliza muda wake.

Alisema amechukua uamuzi huo baada ya uongozi wa chama hicho kutosahihisha au kufafanua tuhuma za usaliti zilizosababisha mbegu ya chuki kukomaa ndani ya chama hicho.

Komu aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa Chadema Taifa, kwa kipindi cha miaka 15 hadi alipong'atuka mwaka 2016, baada ya kushinda ubunge wa Moshi Vijijini kwa kumwangusha mpinzani wake mkubwa, Dk. Cyril Chami (CCM).



Baadhi ya wananchi wakiwa kwenye foleni ya kupimwa joto, kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa corona, ili waingie katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kuona na kusalimia wagonjwa waliolazwa katika hospitali hiyo, jana. **PICHA: NDALIKE SONDA**

# Wafanyakazi shamba la Lerongo 'njia panda'

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

WAFANYAKAZI wa shamba la Lerongo lililopo Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wamebaki 'njia panda' wakiwa hawajui hatima ya ajira yao baada ya mwekezaji wa shamba hilo kudaiwa kuzuiwa kuendelea shughuli za uzalishaji.

Taarifa zaidi zinasema, mwekezaji huyo anadaiwa kuzuiwa kuendelea na shughuli za uzalishaji katika shamba hilo na Chama Kikuu cha Ushirika wa Kahawa mkoani Kilimanjaro (KNCU).

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyakazi wa shamba hilo walilieleza Nipashe kuwa hawajui hatima yao kutokana na mgogoro huo unaodaiwa kusababishwa na malimbikizo ya kodi.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Agness Minde, alisema hawajui hatima yao baada ya mwekezaji wa shamba hilo kuzuiwa kuendelea na shughuli za uzalishaji kutokana na deni kati ya mwekezaji na mmiliki wa shamba hilo.

"Mwishoni mwa mwaka jana walikuja hapa (Lerongo), watu kutoka KNCU na kueleza kwamba tusiendelee na shughuli yoyote ya uzalishaji kwenye shamba hili. Sababu ya kusitisha shughuli hizo walitueleza ni kutokana na mwekezaji kushindwa kuwalipa kodi yao.

"Kimsingi, shughuli zimesimama na tunaona kabisa dalili zote kwamba shamba linarudi mikononi mwao KNCU. Sisi tunachoomba ni tulipwe stahiki zetu."

Kwa mujibu wa Minde, tangu kusimama kwa shughuli za uzalishaji mwezi Desemba mwaka jana hadi kufikia sasa, wafanyakazi wa shamba hilo hawajalipwa mishahara yao.

Mfanyakazi mwingine, Shaibu Monko, alisema licha ya mwekezaji huyo kuwaahidi wasiwe na wasiwasi, lakini wanashangazwa na ujio wa kampuni moja ya udalali kutoka mkoani Arusha kuingia katika eneo hilo na kuuza mali mbalimbali kwa njia ya mnada.

Alipotafutwa kuzungumzia sakata hilo, mwekezaji huyo Mary Otaru, alisema hawezi kuzungumzia jambo hilo kwa kuwa liko katika ngazi ya mahakama.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa KNCU, Godfrey Massawe, alisema walifikia uamuzi huo kutokana na deni la zaidi ya Sh. milioni 250 wanazodai tangu mwaka 2015.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 31, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 17

## CORONA WIKI ILIYOPITA Wamarekani 100,000 waambukizwa



Ukurasa 15

## Ufundi stadi mwarobaini kuibua fursa za kujiajiri



Ukurasa 18

## Virusi matata, tishio duniani?



TEKNOLOJIA

# Grace na Nancy wabunifu wanaofanya maajabu ujenzi

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Majukumu ya polisi



Polisi wana majukumu mengi japo kubwa ni la ulinzi na usalama wa raia na mali zao, pia wanashiriki kwenye masuala mengine kama kushiriki gwaride wakiwa moja ya vikosi vya ulinzi na usalama. **PICHA ZOTE: MTANDAO**





Aidha, wanakuwapo kwenye makaribisho ya viongozi wa kimataifa, kushiriki gwaride kama inavyoonekana, Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnangagwa, akikagua kikosi cha polisi wakati wa gwaride la makaribisho, alipozuru Tanzania mwaka jana.

JIELIMISHE

# Ndizo faida za chungwa jekundu



WATU wengi wana hakika machungwa yaliyoiva ni machungwa tu na huenda wengi hawafahamu kuhusu mekundu.

Machungwa mekundu yalitokea wapi? Yanakuwaje na yana faida gani kiafya? Historia inaeleza kuwa yalitokea Kusini Mashariki mwa kisiwa cha Sisili nchini Italia, kwa hivyo, jina la kawaida la machungwa kama hilo ni Sicilia.

Rangi nyekundu ina 'carotene' kwa wingi na kwa asili hupandwa katika ukanda wa joto wa kama Morocco, kusini mwa Italia, Uhispania, Marekani hasa maeneo ya Florida na California.

Aidha, yemapandwa nchini China kwa miaka mingi na huko Ulaya kwa karne tano. Matunda haya mekundu yamejulikana kwa karne nyingi hufanana kwa muundo, lakini hutofautiana katika ladha, harufu na rangi.

Faida zake kwa lishe nyingi kwani yamejaa vitamini: A, B (1, 2, 9), C, P;) madini ya kalshamu, chuma, sodiamu, potasiamu, seleniamu, magnesiamu, fosforasi.

Yana nyuzi nyingi na viondoa sumu mwilini 'antioxidants' na chungwa jekundu lina protini, mafuta na wanga huliwa kama machungwa mengine.

Yana ubora zaidi kiafya kwani huimarisha kinga, huongeza chemba nyekundu ili kuzalisha damu 'haemoglobin' huimarisha , ngozi; huimarisha uoni, kuzia gauti ni tiba mfumo wa hewa, ni afya kwa mifupa, nywele, meno na  kucha zinaimarishwa.

Ni dawa kwani husaidia  njia ya chakula na kuboresha mfumo wa kusaga chakula. Pia huondoa msongo wa mawazo na magonjwa yanayoambatana na msongo wa mawazo.



ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ufundi stadi mwarobaini kuibua fursa za kujiajiri

HOFU ya wanafunzi wanaohitimu sekondari na taasisi nyingine za elimu, kukosa ajira hasa katika sekta rasmi, inazidi kuongezeka hasa kwenye mataifa yanayoendelea ikiwamo Tanzania.

Hata hivyo, wataalamu na wanataaluma katika sekta za elimu na maendeleo ya vijana, mara kwa mara wanashauri njia mbadala za kukabiliana na changamoto hiyo, ili kupata suluhu itakayowaondoa kutoka katika mkwamo huo.

Mratibu wa Baraza la Ujuzi la Kisekta (SSCs), Jane Gonsalves, ni mmoja wa wanataaluma wanaojadili changamoto hiyo, akiwashauri wahitimu kujiunga katika vyuo vya ufundi stadi na ufundi ili kujiongezea ujuzi na ubunifu utakaowawezesha kujiajiri, badala ya kutegemea ajira rasmi. Gonsalves anayefanya kazi katika Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), anasema wahitumu wanapaswa kuondokana na dhana ya usomi unaolenga kutunukiwa vyeti vya kitaaluma kama njia pekee ya kupata ajira kwenye taasisi za umma na binafsi.

"Nawasihi mwondokane na dhana hiyo iliyojengeka miongoni mwa wahitimu nchini na kwingineko. Waweza kupata daraja la kwanza katika masomo yako na bado ukachagua kwenda kujiunga na vyuo vya ufundi stadi na ufundi, ili tu upate ujuzi utakaokuwezesha kupata ajira kwa haraka au kujiajiri," anasema Gonsalves.

Anasema, ni muhimu vijana walio miongoni mwa wahitimu wengi, wapate elimu itakayowawezesha kubuni miradi na huduma mbazo zitasaidia kutatua changamoto mbalimbali katika jamii, huku zikiwanufaisha kwa kipato cha kukidhi mahitaji yao. Gonsalves anakumbusha kuwa kwa hali hiyo, vijana wanastahili kuchagua kozi zitakazowafanya waajirike kirahisi au kujiajiri, na kwamba sehemu kubwa ya kozi hizo zinapatikana katika Vyuo vya Ufundi Stadi na Ufundi, ambavyo vinatoa ujuzi wa ufundi wa mikono.

Pia, mtaaluma huyo anatoa wito kwa wazazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla kubadili mtazamo wao juu ya elimu ya ufundi stadi na ufundi, kwani kwa sasa, mathalani hapa nchini, kunajengeka dhana ya kwamba mtu anayekwenda kusoma vyuo vya ufundi stadi mfano VETA, ni yule ambaye hana uwezo darasani.

"Dhana hiyo ni tofauti sana na ilivyo kwa wenzetu hasa waliokuwa kundi la nchi masikini, lakini wakapiga hatua kubwa za maendeleo kama vile China, Singapore nakadhalika," anasema.

Gonsalves anasema ufanisi katika eneo hilo utapatikana kupitia uwekezaji mkubwa wa rasilimali,



Wadau mbalimbali wa masuala ya ajira: **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> " Dhana hiyo ni tofauti sana na ilivyo kwa wenzetu hasa waliokuwa kundi la nchi masikini, lakini wakapiga hatua kubwa za maendeleo kama vile China, Singapore nakadhalika.



Jane Gonsalves, akizungumza na wadau hao wa masuala ya ajira.

kama inavyofanyika sasa nchini kupitia uratibu wa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli.

Anaitaja miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa uwekezaji unaosaidia kuiinua sekta ya ufundi stadi ni katika miundombinu na miradi inayolenga kuifikia nchi katika kiwango cha uchumi wa kati unaotegemea viwanda.

Pia anasema, ili kufikia hali hiyo, nchi inapaswa kuwa na nguvukazi yenye ujuzi yenye kupatikana kwa njia tofauti, ikiwamo mkakati wa taifa wa kukuza ujuzi (NSDS-2015/16-205/26). Kwa mujibu wa Gonsalves, mkakati huo unatekelezwa kwa kupitia programu ya kukuza ujuzi (ESPJ) inayosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia vipengele vitatu muhimu.

Anavitaja vipaumbele hivyo kuwa ni mabaraza ya ujuzi ya kisekta (SSCs), mfuko wa maendeleo wa ujuzi (SDF) na vocha ujuzi.

Kwa Tanzania, takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya vijana 800,000 wanahitimu katika vyuo mbalimbali nchini, lakini kati ya hao ni asilimia 10 tu ndio wanaweza kupata ajira kwenye sekta rasmi inayotengeneza ajira zisizozidi 80,000 kila mwaka.

Ni jambo la kawaida kuona vijana wakizunguka na bahasha kusaka ajira. Na hali ya ukosefu wa kazi hujidhihirisha zaidi pale kampuni inapotangaza nafasi za ajira, ni mamia ya vijana hujitokeza kuomba nafasi chache zinazotangazwa.

Vilevile ni kawaida kusikia waajiri wakiendelea kulalamika kwamba hata hao vijana wanoajiriwa bado hawana ujuzi stahiki.

Kutokana na hali hiyo, jitihada kama zile za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya kazi bega kwa bega na TPSF na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) zinapaswa kuungwa mkono.

Pia, kupitia mabaraza ya ujuzi ya kisekta, vijana wataweza kujengewa uwezo kwa kupata nafasi kujifunza katika mahala za kazi kupitia programu za uanajenzi na ile ya wanahitimu tarajali.

Gonsalves anasema kwa vijana ambao hawakupata elimu kupitia mfumo rasmi, wanaweza kufanyiwa tathmini na ujuzi wao kutambulika ili kuwa miongoni mwa wanufaika wa fursa hizo wasioachwa kando.

Hata hivyo, anasema mabaraza ya ujuzi ya kisekta yanaona upo umuhimu wa kutathmini tena mfumo wa elimu wa kitaifa.

Miongoni mwa maswali yanayohitaji kuibua mjadala kwenye jamii ni je, mfumo wa elimu unaandaa wahitimu kuajiriwa tu, ama mfumo huo hauwasaidii watu hasa vijana kufikia hatua hiyo. Gonsalves anasema mfumo wa elimu uliopo ni mzuri, japo kuna changamoto hasa zinazotokana na dhana potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii na wahitimu kwa ujumla juu ya elimu ya ufundi stadi na ufundi.

Anasema wakati umefika sasa kwa watu katika ngazi zote za kijamii wakiwamo wanasiasa, watunga sera, vijana, wanataaluma kama walimu na taasisi za elimu, kubadili mtazamo huo ili elimu hiyo itambuliwe inavyostahili.

***Maoni: 0754691540***

TEKNOLOJIA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Grace na Nancy wabunifu wanaofanya maajabu ujenzi

## • Wabuni matofali, vigae vya plastiki

LENGO namba tano la maendeleo endelevu (SDGs) ya Umoja wa Mataifa (UN), ni usawa wa kijinsia, linalokusudia kuondoa kila aina ya vikwazo, vigingi, uonevu na vizuizi vinavyowakwamisha wanawake na wasichana kusonga mbele kwenye nyanja zote za maendeleo.

Lengo hilo ni muhimu kuviondoa vikwazo ili kufikia maendeleo endelevu yanayohusisha matumizi ya sayansi na teknolojia ambayo inalenga kuondoa au kuziba pengo la kiteknolojia kati ya wanawake na wanaume duniani.

UN inapobainisha lengo hilo, ni bayana kuwa ni kwa nadra kuwaona wanawake wakitajwa sana na kuibuka kwenye masuala ya ubunifu na ugunduzi, ndiyo maana hilo lengo la tano limewekwa mahsusi ili kuwaona wanawake wakiwa wabunifu, watafutaji na wajasiriamali wanaotumia sayansi na teknolojia na kuondokana na 'upofu, uziwi na umbumbumbu' wa matumizi ya teknolojia.

Licha ya wengi kudhani kuwa lengo hilo halitambuliwi na wasichana ukweli ni kwamba licha ya ukweli kuwa ni kwa nadra kuwaona mabinti hasa wasiokuwa na historia ya sayansi kuwa wabunifu wanaofanya mambo kiteknolojia, wanawake wapo na wanafanya mambo makubwa ambayo yanahitaji kupewa msukumo ili wasonge mbele.

Hivi karibuni Nipashe inakutana na wasomi wawili wanaovunja mwiko wa wanawake kubaki nyuma kiubunifu, wawili hawa Nancy Tarimo na Grace Meena wote wakiwa marafiki tena wenye umri sawa wa miaka 25 wamejikita kwenye urejelezaji unatunza mazingira na kupunguza makali ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Grace na Nancy licha ya kusoma masomo ya sanaa wamevunja ukimya na sasa ni wabunifu wanaotamani kufikia viwango vya juu kwenye kutengeneza matofali ambayo ni nyenzo muhimu katika sekta ya ujenzi.

Wawili hawa wanasema katika mahojiano na Nipashe kuwa zama hizi mafanikio ya nchi kiuchumi, kiafya na kitaaluma yanategemea matumizi ya sayansi na teknolojia pamoja na utafiti wa kuleta ufumbuzi wa changamoto za kijamii zinazokwamisha maendeleo.

Nancy anasema hakuna maendeleo bila kuwa na ugunduzi na ubunifu kwenye kilimo kinachoathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa, wadudu waharibifu wa mazao, kadhalika ni ndoto kutokomeza maradhi ya watu na mifugo bila kutumia teknolojia ya kisasa inayoleta, chanjo na tiba kwa maradhi yanayoibuka kila siku kuanzia virusi vya corona hadi homa ya dengue.



Nancy Tarimo (kushoto) akielezea namna wanavyotengeneza matofali ya mchanganyiko wa plastiki na mchanga. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Kwanza tunaomba kama serikali au wahisani hata wawekezaji wakashirikiana nasi kupata mashine ya kukatakata plastiki ili ziwe vipande vidogo ambavyo ni rahisi kuyeyushwa.

Lakini, mbali na hayo ubunifu ni muhimu ili kuanzisha ajira, kupunguza athari za taka mitaani na pia kuilinda Tanzania kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Wabunifu Nancy na Grace ambao wanaanzia elimu yao kwenye kozi za sanaa (arts) wanaamini wameandika historia ya ubunifu. Nancy amesoma Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira na kupata shahada ya ualimu, wakati Grace ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Jordan (Jordan University College) huko amepata shahada ya uzamili katika ualimu akijifunza masomo ya sanaa.

Baada ya kuhitimu masomo yao, mwaka 2018 alianza kwa kuwaingiza kwenye mchakato wa kujiajiri wenyewe na wakaamua kujikita kwenye kufundisha wakianzisha shule ya watoto wadogo na kuanza kutoa elimu ya awali.

Wakiwa kazini kufundisha watoto hawakuishia kushika chaki na kusahihisha kazi za wanafunzi pekee bali walijibidiisha kujifunza kwenye mitandao ya masuala ya teknolojia na kuzungumza na wadau mbalimbali hatimaye wakaibuka na ubunifu wa kuzalisha matofali kwa kutumia mchanga na plastiki.



Nancy na Grace wakiyeyusha plastiki kwa ajili ya kutengeneza matofali. Picha ndogo juu kuli; Grace akifafanua kuwa matofali hayo. Chini; Ukuta wa majaribio uliojengwa kwa kutumia matofali ya plastiki. **PICHA ZOTE: GAUDENSIA MNGUMI**

Wameanza ujasiriamali huo mwaka 2019 wakijikita kwenye kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye mto jirani na makazi yao unaochafuliwa na plastiki zinazozagaa mtoni na uwanda wote jirani.

Wanatumia plastiki hizo pamoja na mchanga kutengeneza matofali ya kuweka chini au pavings, pia wanazalisha ya kujengea nyumba na vigae vya kuezekea.

### HISTORIA YAO

Wasichana hawa licha ya kuhitimu katika vyuo tofauti, wameunganishwa na upendo wao kwenye mazingira wakitengeneza bidhaa muhimu za ujenzi matofali ya aina mbalimbali na vigae.

Katika mahojiano wanasisitiza kuwa wanaamini katika dunia safi na salama, isiyochafuliwa na plastiki wakianza na kuzikusanya na kuziondoa zilizotupwa ili zisichafue maji ya Mto Mpiji eneo la Tegeta Msichoke wanapoishi.

Wanachofanya ni urejelezaji (recycling) wa taka hasa plastiki kuanzia vyombo vya nyumbani na vifungashio vya aina mbalimbali hasa mifuko ya plastiki ambayo hutupwa mtoni humo.

### WALIPOJIKITA

Wakizungumza na Nipashe wabunifu hawa wanasema wanatengeneza matofali na vigae vya kuezekea kwa kutumia mchanganyiko wa uji unaotokana na kuyeyuka plastiki na mchanga kutengeneza vigae au tofali hizo.

"Kinachofanyika ni utaalamu na ubunifu wetu, tukishakusanya plastiki tunazisafisha na kuzipika. Hatuna mitambo hivyo tunatumia pipa la kawaida la bati na kuna kukoleza moto unaoziyeyusha.

Tunakadiria uzito wa plastiki kwa uwiano wa mchanga. Mfano tunatumia mifuko ya plastiki 200 ikishayeyushwa tunaichanganya na nusu kilo ya mchanga kuzalisha tofali 20."

Wanasema wanaendelea kufanya utafiti wa kiuwiano kutengeneza matofali makubwa. Na kwa upande wa vigae wamefaulu kuandaa mchanganyiko, lakini imara lakini wanachokosa ni mashine ya kukandamiza vigae hivyo ili viwe vigumu na imara zaidi.

Wakizungumzia teknolojia wanayotumia ili kuyeyusha plastiki wanasema wanatumia kuni wanazozikusanya mtoni pamoja na mabaki ya taka za mbao ili 'kupika' plastiki. Wanakiri kuwa moshi huo huathiri mazingira pamoja na afya za watu lakini, mwanzo mgumu na wanaamini kuwa enzi za kuni zitakwisha.

### SIFA ZA MATOFALI

Wabunifu hawa wanafanyia kazi nyumbani kwao Msichoke na huko ndiko iliko karakana ya kutengeneza bidhaa zao. Wanaeleza kuwa matofali wanayozalisha ni mapya na teknolojia yake haijazoeleka nchini na wanataja baadhi ya sifa za matofali yao kuwa:

Ni mosi hayatumii sementi wala maji si katika kutengenezwa wala kukomazwa kaa yalivyo ya mchanga na sementi. Mchanganyiko wa mchanga na plastiki iliyoyeyuka ukishapoa hakuna kinachoendelea mbali na kuanza kujenga, anasema Nancy.

"Matofali hayahitaji maji ni rafiki wa mazingira. Hukomaa na kukauka haraka, hayana sababu ya kuwekwa juani, wala hayaharibiwi na mvua kama ya sementi ambayo yakinyeshewa yana hatari ya kumomonyoka," anaongeza.

Anayasifia kuwa yanapotumiwa kwenye ujenzi wa kuta na majengo mengine ni 'sound proof' hivyo huzuia sauti na kelele kupenya na kusikika upande mwingine. Lakini pia hayapitishi maji hivyo kisifa kingine ni 'water proof.'

Wanaeleza kuwa licha ya kwamba hawajapata ushauri wa kitaalamu kutoka taasisi za umma zinazoendeleza wabunifu, wamewasiliana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costec) na kuwapatia matofali na vigae kwa ajili ya uchunguzi na kutoa mapendekezo yao.

Pia wamefikisha maombi Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (Sido), kwa ajili ya kupewa nafasi za utafiti na kusimamiwa na wataalamu.

### KINACHOWAKWAMISHA

Nancy na Grace wanaeleza kuwa wanachofanya ni kazi ya kuendeleza teknolojia ya urejelezaji wa bidhaa za plastiki, kusafisha mto na mazingira lakini pia kueneza elimu na ujuzi kwa vijana wenzao.

Wanasema hawajapata mafunzo kutoka mahali popote mbali na kujisomea na kuwasiliana na kusikiliza ushauri wa watu mbalimbali kuhusu ubunifu wao huo. Aidha, wapo na vijana wengine wawili wanaowafundisha kuzalisha matofali na vigae hivyo, hivyo ili wasongembele wanasema:

"Tunahitaji mashine na utaalamu. Kwanza tunaomba kama serikali au wahisani hata wawekezaji wakashirikiana nasi kupata mashine ya kukatakata plastiki ili ziwe vipande vidogo ambavyo ni rahisi kuyeyushwa," anasema Grace.

Anaongeza: "Aidha, tungefanikiwa zaidi kwenye mradi wetu kama tungepata mashine ya kuyeyusha nailoni ili tuachane na kutumia jiko la kuni na pipa. Kadhalika kwa upande wa vigae vya kuezekea tunahitaji roof tiles machine yenye uwezo wa kuvikandamiza ili viwe vigumu na imara zaidi."

Anaeleza kuwa wamefanya mchanganuo na kwamba gharama za kupata mashine hizo ni karibu Sh. milioni 15 na iwapo watafanikiwa kuzipata uzalishaji wa matufali utaongezeka kwa vile kwa kukosa vitendea kazi wanazalisha matofali 20 kwa siku.

> Mikopo inayotolewa ni midogo kuja na maombi ya Shilingi milioni 15 ni fedha nyingi ambazo si rahisi kuzipata.

Grace anaeleza kuwa licha ya watu kufurahishwa na bidhaa zao wanashindwa kuzalisha na kuuza kwa wingi kwa vile hawana vitendea kazi wala miundombinu ya kisasa.

Wanaomba pia taasisi za kuendeleza wabunifu kama Sido, Costec, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Vyuo Vikuu vya Teknolojia kuwasaidia kutimiza azma yao.

Aidha, wanasema wanahitaji pia kupata eneo la kujenga kiwanda, kukusanya na kusafisha taka za plastiki na sehemu ya kuhifadhi matofali.

### KUSAKA FEDHA

Wabunifu hawa wanapoulizwa iwapo wametumia fursa ya kuomba fedha zinazotolewa na hazina za halmashauri kuendeleza vijana, wanawake na wenye ulemavu, wanasema walizifuatilia fedha, lakini vigezo na masharti viliwakwamisha.

"Moja ya masharti ni vijana kujiunga kwenye kikundi cha uzalishaji mali chenye wanachama 10. Tukakwama kwani sisi hatuzalishi mali ni wabunifu. Tunatakiwa tuwe tumeshafanyabiashara na kutengeneza mapato. Hatujafikia ngazi hiyo. Mikopo inayotolewa ni midogo kuja na maombi ya Shilingi milioni 15 ni fedha nyingi ambazo si rahisi kuzipata," anaeleza Grace.

Wabunifu hawa wanaomba kuwasaidia kwa kuwasiliana nao kwa mitandao ya kijamii kupitia simu.

RIPOTI

CORONA WIKI ILIYOPITA

# Wamarekani 100,000 waambukizwa



Mazishi ya waliokufa kwa corona nchini Italia. **PICHA: DW**

WIKI imemalizika kwa corona kuongeza hofu zaidi, kwa upande wa Marekani madaktari na wauguzi wanaopambana na janga la virusi vya corona wameomba vifaa zaidi vya kujikinga ili kutibu idadi kubwa ya wagonjwa wanaotarajiwa kuongezeka.

Hospitali katika miji ya New York, New Orleans, Detroit na maeneo mengine yaliyoathirika zaidi na virusi hivyo pia zimeelezea wasiwasi kutokana na uhaba wa dawa, vifaa vya matibabu na wahudumu wa afya wakati idadi ya watu waliothibitishwa kuambukizwa hadi mwisho wa wiki walikuwa zaidi ya 100,000.

Baada ya siku kadhaa za malumbano, Bunge la Marekani mwishoni mwa wiki liliidhinisha mpango wa msaada wa ndani wa dola trilioni 2.2, na kuutuma kwa Rais Trump ambaye aliusaini mara moja kuwa sheria.

Mbali na kuzisaidia hospitali, mpango huo utazipa fedha kampuni na wafanyakazi wasio na ajira wanaoathirika na hatua za kusalia majumbani.

Barani Ulaya, Italia imerekodi idadi kubwa ya vifo kuwahi kutokea katika kipindi cha saa 24, ambapo watu 969 waliripotiwa kufariki na kufikisha jumla ya vifo 9,134, nchini humo na zaidi ya watu 86,000 wameambukizwa, na kuizidi China ikimaanisha kuwa ndiyo nchi ya pili duniani yenye maambukizi mengi baada ya Marekani. Rais wa Italia Sergio Mattarella aliita habari hizo kuwa ni "ukurasa wa huzuni katika historia ya nchi."

Uhispania, ni ya nne duniani na idadi kubwa ya maambukizi, imeripoti watu 7,800 kuambikizwa na kufikisha jumla ya zaidi ya watu 64,000. Nchi hiyo imesema wahudumu wa afya wanajumuisha asilimia 15 ya waliambukizwa. Idadi ya vifo ilipanda na kuzidi watu 4,900 na ikiwa ni idadi ya pili kubwa duniani baada ya Italia.

Barani Afrika, Afrika Kusini ilitangaza kifo chake cha kwanza kutokana na virusi vya corona huku jumla ya idadi ya watu walioambukizwa ikizidi 1,000 hata hivyo imeanza kutekeleza amri ya kufungwa shughuli zote isipokuwa zile zenye umuhimu mkubwa, kwa kipindi cha wiki tatu.

Katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kisa cha kwanza cha virusi vya corona kuripotiwa nje ya mji mkuu Kinshasa kimeripotiwa mkoa wa mashariki wa Ituri, ambao pia uliathirika na janga la ebola. Congo ina visa 54, ambapo watu wanne wamefariki dunia, kwa mujibu wa mratibu wa janga hilo nchini humo Jean-Jaques Muyembe.

Shughuli katika mji mkuu Kinshasa zilitarajiwa kusitishwa kuanzia Jumamosi iliyopita kwa siku nne, lakini maofisa mjini humo walichelewesha baada ya tangazo hilo kusababisha ongezeko la bei za bidhaa za msingi na wasiwasi wa kuzuka ghasia.

Afrika Mashariki, polisi nchini Uganda wamesema watu wawili wamelazwa hospitalini baada ya kupigwa risasi kwa kukiuka vizuizi vya usafiri vilivyowekwa kwa ajili ya kudhibiti virusi hivyo. Nchini Kenya, polisi wamekabiliana na wananchi mwishoni mwa wiki katika siku za kuanza kutekelezwa amri ya kutotoka ndani usiku.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, mwishoni mwa wiki alitangaza kusitishwa shughuli kote nchini humo kwa kipindi cha siku 21. **DW**

JE, WAJUA?

# Virusi matata, tishio duniani?



Mwathirika wa ndui, kirusi kilichotikisa dunia na kusababisha takribani vifo milioni 300. **PICHA: MTANDAO.**

MWAKA 2020 umeanza na hofu ya virusi hatari vya COVID 19 vinavyosambaza homa ya corona. Awali vilionekana kama tatizo la China, lakini leo ni janga la dunia likiua watu takribani 34,000 na zaidi ya 700,000 wakiambukizwa dunia nzima.

Janga la virusi si jipya, lakini linapoikumba dunia madhara yake ni makubwa, mathalani hivi ni baadhi ya virusi vilivyoitikisa dunia miaka ya karibuni na kuzua vifo na taharuki kubwa.

Ipo jamii ya Marburg, hawa ni virusi hatari namba moja vinavyosababisha maradhi ya kuvuja damu kwa wingi.

Kirusi hiki kiligundulika mwaka 1967 nchini Ujerumani wakati wanasayansi walipodhuriwa na kirusi hicho kinachoelezwa kutoka kwenye kima wanaodhaniwa kuwa wana asili ya Uganda.

Marburg ni kama ebola kwani husababisha homa kali na kuvuja damu kila sehemu yenye uwazi mwilini na kusababisha kifo.

Idadi ya vifo ni asilimia 80 kwa maana kuwa katika kila watu 100 walioambukizwa 80 hufariki. Nchi za Congo na Angola zilishapata tatizo la virusi hivyo.

### EBOLA

Mlipuko wa kirusi cha ebola ambacho ni hatari uliripotiwa Sudan na Congo kwa mara ya kwanza 1976.

Kirusi hiki huenea kupitia majimaji ya mwili hasa damu, mate, mkojo na hata machozi kupitia kwa mtu aliye na maradhi.

Ebola ni hatari kwani husababisha homa kali na kuvuja damu kila mahali kama ilivyo kwa virusi vya marburg. Kuna jamii mbili za ebola reston, kirusi kisicho na athari kubwa lakini bundibugyo ni hatari huua kwa zaidi ya asilimia 50 mpaka 71 kwa watakaoshambuliwa kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

### RABIES

Licha ya kuwa na chanjo, kirusi hiki husababisha ugonjwa kichaa cha mbwa. Kirusi hiki kiligundulika mwaka 1920. Kuwapo kwa chanjo hiyo kumetokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa huko Ulaya, lakini ukabakia kuwa tatizo India na sehemu nyingine za Afrika.

"Virusi hivi huharibu ubongo na kusababisha ushindwe kung'amua au kufanya majukumu yake ni hatari mno na huambukizwa kupitia kuumwa na mwenye kirusi hicho." Inasema WHO lakini iwapo hutatibiwa kwa asilimia 100 unakufa.

### HIV/VVU

VVU ni kirusi hatari na hata sasa kinaua mamilioni duniani, hakina tiba wala chanjo ili kuna na dawa za kufubaza nguvu ya VVU.

Inakadiriwa kuwa watu milioni 32 wamekufa na VVU tangu ugonjwa huo ulipogundulika mwanzoni mwa miaka ya 1980.

### NDUI –SMALLPOX

Mwaka 1980 WHO ilitangaza kutokomeza ndui duniani ni baada ya kupata chanjo na kuidhibiti. Lakini kilikuwa kirusi hatari mno kilichoangamiza watu milioni 300 duniani na hata wale waliopona walibakiwa na makovu ya kuchimbika ngozi, uoni hafifu na hata ulemavu.

Inakisiwa kuwa asilimia 90 ya watu wa Amerika wenye asili ya taifa hilo walikufa kwa ndui iliyofikishwa kwao na wapelelezi wa Ulaya mwanzoni mwa karne ya 20 na kwamba takribani watu milioni 300 waliangamia na ndui.

### INFLUENZA

Hiki ni kirusi cha mafua fluu na inakadiriwa kuwa pengine watu 500,000 kwa dunia nzima waliuawa na ugonjwa huu, WHO inasema. Kirusi cha mafua au fluu kinaitwa Spanish flu, kilichoanza mwaka 1918 na kuangamiza karibu watu milioni 50.

### DENGUE

Kirusi hiki huambukizwa kupitia mbu anayemuua mwanadamu, kwa mara ya kwanza viligundulika mwaka 1950 nchini Filipino na Thailand na kuanzia hapo, dengue hushambulia watu kuanzia milioni 50 mpaka 100 kila mwaka duniani kote kwa mujibu wa WHO.

Japo haiui kama ebola na wastani wa vifo ni asilimia 2.5 wanaoshambuliwa na virusi hufa.

### SARS

Ni kirusi kinachosababisha kushindwa kupumua na mwaka 2002 kililipuka kwa mara ya kwanza huko Guangdong jimbo la kusini la China, kwa mujibu wa WHO.

Maradhi hayo yanahofiwa kuibuka kutoka kwenye popo na wanyama wengine wanaojitokeza usiku waitwao civets.

SARS ilisambaa katika mataifa 26 duniani na kuambukiza watu 8,000 na kusababisha vifo vya wagonjwa 770.

Virusi hivyo husababisha homa kali, nimonia kali na baadaye mapafu hujaa usaha na kifo chake ni asilimia 9.6 na hakuna chanjo wala dawa.

## NYUMBA YETU

# Namna ya kujenga jengo imara kwenye mfinyanzi

UJENZI wa nyumba zama hizi ni jambo linalotatiza wengi kwa vile ni vigumu kupata ardhi hasa mijini. Kwa vile kila mmoja anatamani kupata nyumba wapo baadhi wanashawishika kununua popote hata kwenye maeneo yenye ardhi inayosumbua kujenga. Huku ni kwenye mabonde pamoja na sehemu zenye udongo wa mfinyanzi.

Sumu ya ujenzi ni udongo wa mfinyanzi na tatizo linakuwa kubwa kama hakuna fedha za kutosha kudhibiti changamoto.

Blogi ya Nyumba yako, Maisha yako", inaainisha udongo huo na kueleza namna ya kuutambua, pamoja namna bora ya kujenga kwenye udongo wa mfinyanzi.

Inasema unapotaka kufanya ujenzi kitu cha kwanza na cha muhimu ni kutambua aina ya udongo uliopo kwenye eneo lako la ujenzi. Utambuzi huu utakusaidia kujua namna ya kufanya ujenzi ili kuepuka changamoto za kufanya marekebisho mengi baada ya ujenzi kutokamilika.

Endapo huzifahamu aina za udongo ni vyema ukawasiliana na mtaalamu wa ujenzi akueleze kwa kina kuhusu aina na tabia za udongo kulingana na mahali ulipo.

### KUTAMBUA MFINYANZI

Udongo wa mfinyanzi una tabia ya kusinyaa na kutanuka. Kukiwa na unyevu au ukilowana hutanuka na endapo unyevu utapungua au kukauka ufinyanzi husinyaa na kuacha nyufa zinazotokana na kupasuka.

Tabia hii husababisha nguvu ya msukumo inayokinzana ambayo itasababisha madhara endapo utaenda kwenye udongo huu bila kuzingatia kanuni za ujenzi kwenye mfinyanzi.

Njia rahisi ya kutambua udongo wa mfinyanzi ni kuangalia alama za mipasuko kwenye ardhi ambayo hutokea hasa kipindi cha kiangazi, ambapo udongo huu unasinyaa sana kutokana na kutokuwa na unyevunyevu.

### ATHARI

Udongo wa mfinyanzi unaposinyaa unakuwa na hatari zaidi kwenye nyumba yako kuliko unapopasuka. Unaposinyaa unakuwa na mipasuko inayoacha nafasi hali inayosababisha nguvu kubwa ya mvutano kwenye msingi wa nyumba. Hali hii inapotokea nyumba itapata nyufa au mipasuko kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye msingi, kuta, nguzo, sakafu, marumaru pamoja na maeneo mengine. Hali hii ya mipasuko huharibu taswira ya jengo na kulifanya liwe hatari kwa matumizi.

Nyumba yenye shida hii litahitaji marekebisho ya mara kwa mara ili kuziba nyufa na kubadili sehemu zilizoharibika na wakati mwingine inakuwa vigumu kuishi kwenye nyumba ya namna hii kitu ambacho ni hasara kubwa kwa mmiliki wa jengo.

### CHA KUFANYA

Kuna njia mbalimali za kufanya ujenzi kwenye mfinyanzi, lakini njia kuu mbili zinazoweza kutumiwa kukabiliana na udongo wa aina hii ni kama hizo:

Mosi kuondoa udongo wote wa mfinyanzi kwenye eneo utakalojenga msingi. Unachimba na kuuondoa wote na kisha kuweka mchanga.

Mbinu hii inatumika ili kuhakikisha msingi haugusani na udongo wa mfinyanzi. Ukishaondoa udongo wa mfinyanzi unaleta udongo mwingine mpya na kuuweka kwenye eneo husika ambapo utajenga msingi huo. Njia hii inaweza ikaonekana ina gharama kubwa wakati unaanza ujenzi, lakini ni mbinu ya uhakika kuhakikisha hukutani na changamoto za mipasuko na nyufa baada ya kumaliza kujenga.



Mfinyanzi ni udongo unaoumiza majengo pamoja na mazao hasa unapokauka. **PICHA: MTANDAO.**

UCHAMBUZI
NA MICHAEL ENEZA

# Mwelekeo corona kuamua hatima masomo mtandaoni

MJADALA umeanza kusikika hapa na pale baada ya baadhi ya shule za binafsi kuunganisha wanafunzi wao kwa njia ya mtandao, ili waendelee na masomo nyakati hizi ambako shule zimefungwa kote nchini kutokana na tishio la kuenea kwa homa ya mapafu ya corona.

Wanafunzi wanaosoma nchini jirani kama Kenya na Uganda ambao wamerudi nyumbani pamoja na wengine wanaendelea na masomo kwa njia ya mtandao.

Wakati wazazi wenye watoto shule binafsi wamepongeza juhudi hizo na kuzitaka shule za serikali kuiga mfano huo, wako wenye wasiwasi na hatua hiyo, kuwa itawapa watoto wa shule binafsi nyenzo za ziada.

Ni kama wanahofia wataachwa nyuma kimasomo, hasa katika mitihani ya mwisho.

Inawezekana taarifa iliyotolewa haikufafanua nini hasa kinatazamiwa kufanyika, halafu kuna mazingira ya wasiwasi kuhusu muda wa kufunga shule na nini hasa cha kufanya katika kipindi hicho.

Ilipotoa tangazo la kufunga shule kuelekea katikati ya mwezi, serikali ilitazamia kuwa hali hiyo itadumu kwa mwezi mmoja, lakini kinachotokea kwingineko bara la Afrika kinaleta wasiwasi.

Mwisho wa wiki ya tatu ya mwezi Machi, jumla ya maambukizi barani Afrika ilikuwa 1,000 na huku Afrika Kusini pekee ikiwa na wagonjwa 200, hadi kufikia Ijumaa Machi wiki iliyopita hali ilikuwa tofauti, wagonjwa kufika 3,030 na Afrika Kusini 500, hapa Tanzania waliripotiwa 13.

Kwa njia hiyo kulikuwa na ishara kuwa nchi za Afrika zingeingia katika kasi ya kiwango fulani ya maambukizi kwani kwa jumla yalikuwa yanaongezeka, licha ya juhudi za nchi tofauti kuchukua hatua.

Kwa njia hiyo kukosekana kwa masomo siyo ajabu kuendelea kwa muda mrefu zaidi ya mwezi mmoja, na endapo janga halisi la homa ya corona, hata hao wanaojaribu kutumia muda huu vyema ni wazi watakuwa hawana uwezo wa kuendelea.

Ni pale tu mazingira yakiwa ya kitu kama likizo ndipo mpangilio huo unaweza kutumika, na siyo inapogeuka janga la kitaifa.

Kwanza jambo la awali ni kuhusu mpangilio wa kinachotakiwa kufundishwa au kuwahishwa kwa wanafunzi majumbani kwao kupitia mtandao. Mtaala hauwezi kuanza tu kupelekwa majumbani au mtandaoni bila kujipanga utafanya hivyo kwa muda gani, na ni kwa kiwango gani wanafunzi watakuwa tayari kupokea masomo. Hata wanaolipiwa shule za binafsi



Katika mazingira haya ya kujisomea hata bila ya corona ni vigumu wanafunzi na walimu kutumia mitandao kwa vile hakuna miundombinu. **PICHA: MTANDAO.**

> "Ndicho ambacho sote tulitazamia na ndilo jambo ambalo wengi wanaliombea, lakini dalili za majirani zetu hasa mataifa mengine ya Afrika kuna wasiwasi.

wana tofauti za kina katika makazi, utayari wao, kwani si kila kaya yenye mtoto shule binafsi ina miundombinu ya kutumia mtandao.

Kwa maana hiyo tatizo la utayari wa wanafunzi au mlingano wao kimasomo wakati shule zinafunguliwa siyo tu kati ya shule binafsi na zile za serikali ila hata kati ya shule binafsi zenyewe.

Waalimu hawawezi kuhakikisha kuwa wanafunzi wapo katika sehemu husika kwa wakati na hisia zao ziko katika masomo, labda kama homa ya corona itakuwa ni gumzo tu la mtaani au hotuba za viongozi. Yanapoanza matukio ya vifo watoto wakaanza kuyasikia, mtaala utafikia mwisho.

Unaweza kusema jitihada hii ya kuweka mtaala wa mtandaoni wakati wa kufunga shule ni wazo lililoendana na hisia za awali kuwa janga la corona kimsingi ni la nchi zenye baridi, na siyo joto kama hapa, au Afrika Mashariki kwa jumla. Bado hisia hiyo haijaondoka kwani idadi ya maambukizi ya ndani ilikuwa ndogo, zaidi ni watu waliongia nchini kutoka nje, wawe raia au wageni halisi.

Ila urahisi wa wao kuambuzikwa wakiwa ng'ambo na kuwepo kwa ubaridi wa kutosha kupata mafua hata hapa, au kuenea kwa homa hiyo Afrika Kusini ni kielelezo kuwa hata sisi hatuna kinga, labda kuwe na mazingira tu ya baraka fulani taifa lisipatwe na janga hilo.

Kumbe hakuna mshindi katika 'mkwaju ngoma' huo kwani walio na nafasi ya kusoma nyumbani hawatakuwa na muda wa kufanya hivyo, kwani kwa njia hii au ile mazingira yatabadilika. Endapo mwezi mmoja umeisha hakuna maambukizi mapya na waliopatwa na homa hiyo awali wanapona, shule zitafunguliwa na hiyo 'tuisheni' ya wiki mbili au tatu kama itakuwa imeanza mapema haitabadili kitu.

Ila endapo kutakuwa na mazingira ya janga hilo kuingia nchini siyo rahisi kuona walimu au wanafunzi wakiweka akili zao sawa na kuendelea na masomo katika utulivu wa kawaida, endapo vifo vitaanza kugusa watu mitaa yote.

Ndiyo eneo ambalo halielekei kuwa waliobuni suala la kusoma mtandaoni wakati wa kufunga shule inaelekea hawakuangalia, kwani waliona kana kwamba wanafunzi wanaenda livu. Ukweli ni kuwa vifo vikitokea itakuwa wazi kutakuwa na taharuki na ni vigumu kuwa tuisheni.

Bado hatujafikia huko, lakini endapo waalimu wa shule za binafsi wana njia za kuwasiliana na wanafunzi wao, ni wazi kuwa wangetanguliza elimu ya kujilinda na ugonjwa huo na siyo kupenyeza masomo. Waongee nao kuhusu wanavyojilinda na kuchunga kutoka na kuingia nyumbani, wawape matumaini na kuwajengea imani.

Ni jambo jema kuwapongeza waliobuni mkakati huo kwani walionyesha kuwajali wanafunzi kuhusu masomo yao na siku zinazoelekea kupotea bila kusoma.

Japo nia ni njema walijitahidi kufikia njia hiyo, lakini ni kama hawakuelewa undani wa suala lililopo mezani, wanajenga mpango wao wa masomo ya ziada kupitia kompyuta wanafunzi wakiwa nyumbani, kwa matazamio kuwa hali ya utulivu na ugonjwa huo kusikika kwa mbali ingedumu muda mfupi, halafu ipite.

Ndicho ambacho sote tulitazamia na ndilo jambo ambalo wengi wanaliombea, lakini dalili za majirani zetu hasa mataifa mengine ya Afrika kuna wasiwasi.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Makundirika yanaweza kuchangia kuwafanya watoto kukutana na vishawishi chanya au hasi toka kwa marafiki zao. Je, wazazi na walezi wanatakiwa kujua marafiki wa watoto wao? Wadau wanajadili.



### ZAINABU MSALAMA (MKAZI WA JIJIJNI DAR ES SALAAM)

MAKUNDIRIKA ni hatari sana katika jamii, hayana mafunzo yoyote ya kimaadili kwa wakubwa na wadogo zao, yametawaliwa na jaziba, hasira, chuki majivuno na dharau kutunushiana misuli mizozo isiyokua na tija, fujo, subira imepotea kabisa.

Umaarufu ndiyo ngao ya maisha yao, kudai haki bila kufanya kazi, hawajui wajibu wao siyo kwa wao wenyewe kwa familia zao wala kwa jamii zao.

Mweleke potevu kwa makundi rika haya ni kutokana na utandawazi ambao umesababisha a kulega na kupotea kwa mafunzo ya asili ya jando na unyago na kutekwa kwa kiasi kikubwa na tamaduni za kimagharibi, hivyo kujishughulisha zaidi na mambo ya kuiga na kushindwa kufanya mambo yao ya ubunifu na kusahau kabisa tamaduni zao katika suala zima la malezi na kujishughulisha na mambo, ambayo hayana tija katika maisha ya baadaye.

Ni wakati wa kila mmoja wetu kuamka na kujua ni wapi alipo mtoto wake na anafanya nini, iwe ni shuleni au sehemu yoyote ile. Ikumbukwe hata shuleni mtoto anaweza akajifunza tabia mbaya kulingana na makundi ya wanafunzi wenzake anaokutana nao. Wanaweza kuwa ni wale wasiotaka shule kabisa.

Watoto, wavuta bangi, na wenye tabia ya udokozi, hivyo iwapo wazazi na walezi watazembea bila kufuatilia ili kujua marafiki wa watoto wao, watarajie kwamba ipo siku wanaweza kukumbana na mambo mageni kutoka kwa watoto wao ambayo si mema, ingawa pia wapo wanaopata marafiki wema.



### MWASITI RAJABU (MKAZI WA MJINI MOROGORO)

SUALA la mzazi kujua marafiki wa mtoto wake akiwa shuleni ni la msingi sana, kwa sababu linasaidia hata kujua kama anaelekea kubaya au kuzuri, kwani unaweza kujua kupitia kwa hao marafiki zake kuwa ni wema au wabaya.

Vilevile wazazi wajenge ukaribu na walimu na majirani ili kuweza kujua tabia zinazojitokeza kwa watoto wetu wakiwa nje ya nyumbani. Kwa mzazi mwenye mtoto kuanzia umri wa miaka sita hadi tisa, wanaweza kuwaalika marafiki wa mtoto wao ili wacheze pamoja nyumbani, kwani hatua hiyo inaweza kusaidia kujua tabia zao na mambo gani wanashawishiana. Iwapo mzazi utabaini kwamba kuna jambo haliko sawa, basi hiyo ni fursa ya kuwapa mwongozo mzuri.

Kwa wale wenye watoto wa miaka 10 hadi 15. Hawa wako kwenye hatari kubwa ya kujiingiza katika vishawishi vya makundi rika ni dhahiri na vigumu kwa mtoto kujiepusha nayo hata kwa yule mwenye uwezo wa kukwepa vishawishi.

Umri huu ni changamoto kwa mzazi kumshawishi mtoto kubadilisha maamuzi kwa kuwa kipindi hiki anapata dhana ya kujitegemea hasa kimaamuzi.

Hivyo ili kulisaidia kundi hili, ni vyema kujadili nalo kuhusu changamoto za vishawishi ambavyo linakumbana navyo linapokuwa shuleni na hata mitaani.

Kikubwa zaidi ni mzazi kuwa mpole na mvumilivu kwani watoto wenye umri kama huo mara nyingi huweza kufanya mambo bila kujali matokeo kama yatakuwa ni ya hatari au la.



### FRANK EMMANUEL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

MIMI ninaamini kwamba kuna uwezekano wa kupunguza watoto kuharibikiwa kutokana na msukumo wa makundi-rika, hasa kwa kumzuia kujihusisha nayo, kutokana na ukweli kwamba katika makundi hayo kuna hasi na chanya na mara nyingi watoto wengi huangukia kwenye hasi na hivyo kuharibikiwa.

Unaweza kukuta kama mtoto wako alikuwa na na uwezo mzuri shuleni, unaanza kushuka, utoro shuleni na wakati mwingine anaaga kwamba anakwenda shule na kumbe anaishia kwenye vijiwe vya watoto wa kihuni, na nyumbani tabia zake zinabadilika, anaweza kuwa mkorofi au kufanya jambo lolote hata baya.

Kwa hiyo suala la mzazi au mlezi kujua marafiki wa mtoto wake iwe shuleni au wapi ni jambo la msingi sana ili kama itagundulika kuwa siyo wema, basi mtoto akanywe mapema na kuachana nao.

Kwa ujumla ni kwamba makundirika mara nyingi huwa siyo mazuri, yanaharibu sana vijana wa kiume na wa kike na kujikuta wakijiingiza kwenye matendo maovu.

Lingine ni kwaba wazazi na walezi wasiwe wakali, wawafanye watoto kuwa marafiki, kwani wakati mwingine watoto wanaweza kutafuta marafiki wabaya kutokana na jinsi wanavyosikilizwa na hivyo kudhani kwamba kwenye vijiwe ndiko kuna watu wanaoweza kuwashauri vizuri na kumbe wanaharibikiwa.



### DEBORAH MASANGURA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UTAWAZI imekuja na mambo mengi sana na umesababisha baadhi ya wazazi kudhani kwamba suala la kulea watoto ni sawa na kupoteza muda wao, kwa vile wana majukumu mengi na wanaona suala na malezi ya watoto kama kupoteza muda. Wanaona ni bora wawe na majukumu mengi kazini.

Wanasahau kwamba malezi kwa watoto ni moja ya mambo ya msingi. Malezi haya hayaishii nyumbani tu bali mzazi anatakiwa kujua hata marafiki wa watoto wake shuleni kama wanafaa au hawafai ili hatimaye kama atabaini kuwa hawafai amzuie mtoto wake kuwa nao karibu. Lakini jambo hili wakiachiwa walimu tu utakuwa ni mzigo mkubwa kwao.

Hivyo kila mzazi atimize wajibu wake wa malezi kwa mtoto inavyotakiwa, kwani ndiyo njia bora ya mwongozo utakaomfanya aweze kuwa mwema kuliko kumwacha afanye anavyotaka na kujikuta akikumbwa na makundirika na kuiga tabia hasi ambayo inaweza kusababisha akatishe masomo na kujiunga kwenye makundi maovu na hata kuhatarisha maisha yake.

Kutokana na utandawazi, hata jirani akiona mtoto wa mwenzake anafanya jambo baya hawezi kumkea. Yaani kwa sasa mtoto siyo tena mali ya jamii, mtoto anajilea mwenyewe bila kujua mwenendo wa maadili mema. Kwa hiyo Kila mzazi afanye sehemu yake katika malezi kuanzia nyumbani na pia shuleni ili kubaini ni nani marafiki wa mtoto wake na ni wa aina gani.



### IBRAHIM MPWAPWA (MKAZI WA MJINI SINGIDA)

UMRI wa kuanzia miaka 16 hadi 18 una changamoto nyingi na ndiyo unakutana na makundirika na bahati mbaya ni kwamba umri huu ndiyo watoto wanadhani eti wamkuwa watu wazima na kuamini kuwa wanaweza kujisimamia wenyewe na husukumwa kutaka kujua kila aina ya kilevu kuanzia kwenye, sigara, bangi, dawa za kulevya na hata mambo ya kujamiiana.

Kundi lenye umri kama huo, mara nyingi huamini marafiki kuliko wazazi au walezi. Yawezekana mzazi au mlezi akajitahidi kushauri kwa kila njia ili kumrudisha mtoto kwenye mstari lakini akashindwa. Njia nzuri ambayo inaweza kusaidia kumuweka mtoto sawa ni kujua mapema rafiki zake shuleni na pia kukaa naye kwa karibu kila mara na kumshauri mambo mazuri kwa ajili ya maisha yake ya baadaye na kumtia moyo ili akazane kwenye masomo. Lakini mzazi akizembea katika hilo, mtoto atafundishwa na watu wengine na mwisho wa siku ni kulalamika tu kwamba 'mtoto huyu ni mkorofi hanisikilizi' na kumbe kosa umelifanya mwenyewe.

Katika malezi kuna njia nyingi za kuweza kumfanya mtoto akawa rafiki na siyo lazima kutumia vitisho, ambavyo kwa kweli vinaweza kumfanya mtoto akawa mwoga. Badala yake iwapo ataonekana amebadilika tabia na kuwa mbovu, hiyo ni nafasi kwa mzazi au mlezi kumwambia kumwelezea tabia zinanzokubalika ndani ya jamii na kumuonyesha mifano ya watoto wema na wenye mafanikio katika jamii.



**HABARI MBEYA**

# DC aridhishwa maandalizi ya kukabili corona

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbarali, imeelezea kuridhishwa na maandalizi ya kutenga eneo maalum kwa ajili ya kuwahudumia washukiwa na maambukizi ya corona.

Kamati hiyo chini ya Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune, ilifika eneo la Kitongoji cha Mpunga Relini mahali ambapo hospitali mpya ya wilaya inajengwa kuangalia maendeleo ya ujenzi wa jengo maalum la kuwahudumia wanaohisiwa kuwa na ugonjwa huo.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa jengo hilo mwishoni mwa wiki, Mfune alisema maandalizi yamefikia hatua nzuri na mtu yeyote atakayeshukiwa atapata huduma zote muhimu za afya.

"Baada ya tamko la Waziri wa Afya (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), Ummy Mwalimu, kuziagiza halmashauri zote nchi kutenga maeneo maalum kuwahudumia washukiwa wa maambukizi ya corona, tulitenga jengo moja kutoka hospitali mpya ya wilaya ili tuwahudumie na tayari maandalizi yamekamilika na tuko tayari kuwahudumia wale wote watakaobainika," alisema Mfune.

Aidha, Mfune alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wenye lengo kuhakikisha mazingira na huduma itakazotolewa zitakuwa rafiki kwa wagonjwa na watoa huduma.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema miongoni mwa maeneo ambayo wameyapa kipaumbele kwenye ujenzi wa jengo hilo ni kutenga chumba maalum cha kupumzikia wagonjwa.

Alisema chumba hicho maalum kitakuwa na hewa ya kutosha na miundombinu mingine ambayo haitaruhusu mwingiliano ambao utaongeza maambukizi kwa njia ya hewa.

Naye Msangi aliwaomba wananchi wa Mbarali kutoa ushirikiano pindi wanapohisi kuna mshukiwa wa maambukizi ya corona kwenye maeneo yao.

Aliwataka kuzingatia kanuni bora za afya zinazoelekeza kunawa maji safi na salama yanayotiririka kwa kutumia vitakasa kabla na baada ya kutoka chooni sambamba na kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima hasa kwenye magulio ya soko.

# Wadai kuchangia maji na wanyama

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Kijiji cha Usoha Muungano katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwapelekea huduma ya maji ya bomba kwa madai kuwa wanatumia maji machafu ambayo pia wanachangia na wanyama wakiwamo mbwa na ng'ombe.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Sebastian Mwangaya, alisema hayo jana kuwa kijiji hicho chenye wakazi 1,563 hakijawahi kupata maji ya bomba hali inayowalazimu kutumia maji ya Mto Bangalala ambayo si salama kwa afya zao.

Alisema mto huo unaotegemewa na wananchi, uko mbali na makazi yao hali inayosababisha kutoelewana kati ya wanandoa na wakati mwingine kusababisha baadhi ya ndoa hizo kuvunjika.

"Kipindi cha Desemba, mwaka jana, nilipokea kesi tano za wanandoa kutokana na changamoto ya umbali mrefu kufuata huduma ya maji. Baadhi ya wanaume huwapiga wake zao kisa kuchelewa kufuata maji na wakati mwingine wanaume hao hao hudhani wake zao wanachepuka wanapokuwa mtoni kuchota maji," alisema Mwangaya.

Aidha, msimu huu wa mvua kuna nafuu kidogo kwa kuwa wananchi hupata maji ya mvua, lakini hofu yao ni baada ya kipindi cha masika kwisha watarudi kwenye adha ya kutumia maji yasiyo safi na salama.

Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, Veronica Ibrahim, alisema muda mwingine hulazimika kusubiri wanyama kama ng'ombe kunywa maji mtoni hapo kisha wao wapate huduma huku maji hayo yakiwa machafu.

Naye Modest Martin, alisema kipindi hiki cha msimu wa mvua hapata unafuu wa huduma ya maji yakiwamo ya mvua na ya mtoni, kulinganisha na msimu wa kiangazi ambao maji ya mto huo hukauka.

Martin alisema kipindi cha kampeni katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Diwani wa Kata ya Maendeleo, Yohana Nyamwale, aliahidi kuanza na kero ya maji pindi akipata nafasi hiyo.

Nyamwale kwa upande wake alisema anafahamu kero ya maji katika kijiji hicho kwa kuwa makazi yake yako hapo lakini alidai kuwa katika bajeti ya fedha ya mwaka 2019/20, halmashauri ilielekeza fedha za kujenga mradi mkubwa wa maji katika Kijiji cha Ikoho ambako kuna Sekondari na Kituo cha Afya.

Alisema suala la kutatua changamoto ya maji katika kijiji cha Usoha Muungano linategemea bajeti ya halmashauri na kwamba yeye kazi yake ni kuikumbusha serikali katika vikao na mabaraza ya madiwani.



Baadhi ya madereva wa bodaboda wa Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakizoa taka baada ya kufanya usafi kwenye moja ya mitaro iliyopo nje ya stendi ya mabasi ya mji huo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mfumo dume bado kikwazo kwa wanawake

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASILIMIA 60 ya wanawake wanaoishi katika kijiji cha Simambwe, wilayani Mbeya, wanadaiwa kunyanyaswa na familia zao katika masuala ya umiliki wa ardhi pamoja na mgawanyo wa mali.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Clemence Bulaya, alibainisha hayo jana wakati wa mahojiano na Nipashe, huku akisema kiwango cha matukio ya wanawake kunyanyaswa katika umiliki wa ardhi na mgawanyo wa rasilimali kimekuwa kikubwa kutokana na wanawake wenyewe kutokuwa na uelewa na haki za kumiliki mali.

Bulaya alisema uwapo wa idadi kubwa ya wanawake kunyanyaswa katika familia umesababisha jamii kuendelea kuamini kuwa mwanamke hastahili kumiliki mali, hivyo kuendelea kukandamizwa.

Aidha, Bulaya alibainisha kuwa katika familia, mawifi wamekuwa mstari wa mbele kuchochea ukandamizaji wa mwanamke katika umiliki wa mali pindi kaka yao anapofariki dunia kutokana na kutoa lugha za kejeli.

"Suala la kunyanyaswa wanawake katika umiliki wa ardhi pamoja na mali katika familia mara nyingine huchochewa na mwanamke mwenyewe. Baadhi yao hawakubali mwanamke mwenzao kumiliki mali au ardhi, hivyo ni lazima wanawake wenyewe kwanza wajitambue na wawe na sauti ya pamoja," alisema Bulaya.

Katika mapambano ya kupinga ukatili wa umiliki mali dhidi ya wanawake, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umesema vita dhidi ya ukatili huo vinaendelea, ambapo mpaka sasa wameweza kutoa elimu ya namna ya kumkomboa mwanamke kiuchumi.

Mwezeshaji wa Masuala ya Jinsia kutoka TGNP, Rehema Mwateba, alisema watahakikisha wanatoa elimu ya uziduaji ambayo inahusiana na sekta ya uchimbaji madini kwa wanawake ili kuwanufaisha zaidi wanawake kuliko wanaume.

Alisema ili sekta ya uchimbaji madini (uziduaji) imnufaishe mwanamke, serikali haina budi kutoa kipaumbele cha fursa za ajira pamoja na maeneo kwa ajili ya kufanyia shughuli hiyo.

Mmoja wa wanawake waliozungumzia suala hilo, Suzana Tenesi, alisema watahakikisha wanawake katika Kijiji cha Simbambwe, wanapata haki za kumiliki ardhi na mali katika familia.

Tenesi alisema wamekuwa wakitoa elimu ya umuhimu wa mwanamke kumiliki mali sambamba na kukemea vitendo mbalimbali vya kikatili vinavyotokea katika jamii ikiwamo ubakaji.





# Pinda ataja mwarobaini wa kutokomeza udumavu

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameishauri jamii kujikita kwenye kilimo cha mboga ili kuimarisha afya ya mwili na kuondokana na utapiamlo na udumavu nchini.

Rai hiyo aliitoa jana alipokuwa akikabidhiwa vitalu nyumba 12 kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo hicho na vilivyogharimu takribani Sh. milioni 100 vilivyotengenezwa na Kampuni ya Daymo Trading Company LTD ya jijini Arusha.

Alieleza kuwa hali ya utapiamlo ipo juu na inatokana na watu kutozingatia vyakula vya kujenga mwili ikiwamo mboga kwa mujibu wa viwango vinavyotolewa na wataalamu wa afya.

"Kumekuwa na dhana potofu miongoni mwa jamii kwamba wanaotumia mboga za majani kwa wingi ni maskini na watu wasiokuwa na uwezo, si kweli hiyo ni dhana potofu tu, mboga za majani ni muhimu sana katika kujenga mwili na kuimarisha afya," alisema.

Alibainisha kuwa tangu amestaafu amejikita katika shughuli mbalimbali za kilimo katika eneo la Zuzu na imesaidia wanafunzi wa vyuo vikuu vya ndani na nje ya mkoa wa Dodoma kujifunza shughuli za kilimo na ufugaji.

"Naendesha shughuli hizi kwa fedha ambazo nakopa benki mbalimbali... Watanzania msiogope kukopa maana hakuna tajiri yeyote duniani anayefanikiwa bila kukopa," alisema Pinda.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, aliwataka vijana kujifunza kutoka kwa kiongozi huyo katika uendeshaji wa miradi ya kilimo na ufugaji.

"Vijana lazima tuchukue mfano huu, tusiogope kukope ili mradi tuwe na wazo na baada ya kufanikiwa kupata mkopo tuitumie kwa malengo yaliyokusudiwa, tutafanikiwa na tutaweza kurejesha marejesho kwa wakati," alisema.

Naye Ofisa Masoko wa Kampuni hiyo, Dativa Koyanga, aliwashauri Watanzania na hasa vijana kutumia fursa hiyo ya vitalu nyumba kulima kilimo cha kisasa na kupata faida kubwa.

"Vitalu nyumba ni kiimo cha kisasa ambacho kina faida kubwa, mtu yeyote atakayekitumia atafanikiwa, na kukuza uchumi na kujipatia kipato," alisema.



Wachuuzi wa karanga wakisubiri wateja katika eneo la Mji Mpya, jijini Dodoma jana, huku wakionekana kutochukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, kutokana na kutoweka maji ya kunawa na sabuni au kitakasa mikono kwa ajili yao na wateja wao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC acharukia madereva wa malori kuwa chanzo cha ajali

Na Renatha Msungu, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ametoa siku saba kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo (OCD), kufanya msako wa madereva wa malori yanayobeba madini ujenzi, ambao wamekuwa wakisababisha ajali kwa uzembe.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katambi alisema hivi karibuni kumekuwa na ajali mbalimbali wilayani Dodoma zinazosababishwa na madereva wa malori, ambao wengi wao inasemekana hawana leseni, hivyo kusababisha vifo vya watu kila wakati.

"Nasema nimechoka kuona maiti za watoto wanaogongwa na madereva wa malori, siku za hivi karibuni nimeshuhudia ajali nyingi za watoto wa shule wanaofariki kutokana na kugongwa na magari hayo yanayobeba madini ujenzi kama vile mchanga na kokoto," alisema Katambi.

Aidha, Mkuu wa Wilaya hiyo alisema kuna madereva wanaendesha bila tahadhari yoyote.

"Namtaka OCD kufanya ukaguzi wa magari mabovu na madereva wasiokuwa na leseni ili wachukuliwe hatua kali za kisheria," alisema na kuongeza:

"Watoto wetu wanagongwa sana, tena wakivuka katika alama za vivuko, hivyo inaonesha madereva hawana mafunzo halali."

Alizitaka mamlaka husika kuangalia adhabu kali kwa madereva wanaofanya uzembe kama huo barabarani kwa kuwa adhabu iliyopo ya kulipa faini hawaiogopi.

Katambi alisema maeneo ambayo madereva hao wamekuwa wakiendesha bila kufuata sheria ni pamoja na barabara iliyopo maeneo ya Emmaus kuelekea Mlimwa, ambapo zimekuwa zikitokea ajali za mara kwa mara zinazosababishwa na madereva hao.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya alisema wanatarajia kuanza operesheni usalama kwa ajili ya kudhibiti wahalifu kama vibaka, watumia kilevi cha gundi na vijana wanaozagaa zagaa ovyo Dodoma.

"Siku hizi Dodoma kuna wimbi la wahalifu, ambao wamekuwa kikwazo kwa wananchi wanaofanya shughuli zao kwa matukio ya ukabaji, uporaji vimekithiri sana, hivyo tutaanza msako ili kudhibiti hali hii," alisema Katambi.

Aliwaonya vijana wazururaji waache mara moja tabia hiyo kwa kuwa wakikamatwa, sheria itachukua mkondo wake.

## Mafundi cherehani wapewa tahadhari mlipuko wa corona

Na Peter Mkwavila, DODOMA

MAFUNDI cherehani wametakiwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Umoja wa Mafundi Cherehani Mkoa wa Dodoma (Umachedo), Khalid Zoya, alisema kuwa kutokana na mafundi hao kukutana kila wakati na wateja, ni muhimu wakachukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo.

Zoya alisema ni vyema kila fundi mahali pa kazi alipo akahakikisha anakuwa na vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo, ikiwamo vitakatisa mikono.

Alisema kuwa ametoa maagizo kwa mafundi wote wa cherehani kuhakikisha pia wanatoa elimu kwa wateja wao juu ya kujikinga na maambukizi hayo kwa malengo ya kuimarisha afya zao na kwa wateja wanaowahudumia.

"Sisi mafundi cherehani tunakutana na watu wengi na wa aina mbalimbali kutokana na hali hiyo tunatakiwa kuwa na tahadhari kubwa ya kujikinga na maambukizi.


"Lakini si hilo tu nimewaagiza mafundi wote wa cherehani ambao ni wanachama kuhakikisha wanakuwa na vitakatisha mikono katika maeneo yao ya kazi ili kuweza kutekeleza agizo la serikali la kujikinga na virusi hivyo," alisema.

Sambamba na hilo, mwenyekiti huyo alitoa maagizo kwa viongozi wa chama hicho waliopo wilayani kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii inayowazunguka pamoja na mafundi wenyewe.

"Huko wilayani hususani vijijini nimewaelekeza viongozi wangu kuhakikisha wanawatembelea mafundi cherehani na kutoa elimu juu ya kujikinga na gonjwa hili hatari," alisema.

Aliongeza: "Wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya serikali kwa kuzingatia usafi wa kunawa mikono, kutokusalimiana kwa kushikana mikono wala kukohoa wala kupiga chafya bila kuziba mdomo."

**"Lakini si hilo tu nimewaagiza mafundi wote wa cherehani ambao ni wanachama kuhakikisha wanakuwa na vitakatisha mikono katika maeneo yao ya kazi ili kuweza kutekeleza agizo la serikali la kujikinga na virusi hivyo," alisema.**



# Anglikana yafuta mahubiri marefu, kwaya, kubusu msalaba Ijumaa Kuu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, amesema kanisa hilo litatumia sehemu kubwa ya ibada ya Pasaka kwa ajili ya kuliombea Taifa kupambana na janga la corona.

Alisema hayo Mjini Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari akielezea utaratibu wa ibada utakavyoendeshwa katika kipindi cha Pasaka.

Alisema kanisa linaunga mkono kauli zilizotolewa na viongozi wakuu wa nchi juu ya mikakati ya kupambana na ugonjwa wa corona, ikiwamo kupunguza mikusanyiko mikubwa inayowakutanisha watu mbalimbali kwa wakati mmoja.

Askofu Hafidh alisema ibada zote zitafupishwa na mahubiri yasizidi dakika kumi, ambapo pia ibada hazitakuwa na kwaya.

Aidha, alisema baadhi ya shughuli zimesitishwa kabisa katika kipindi hiki kuelekea katika sherehe za Pasaka ikiwamo mazoezi ya kwaya, madarasa ya kipaimara pamoja na mikesha ya aina zote na tafrija.

Alieleza kuwa ibada ya Ijumaa Kuu hakutakuwa na njia ya msalaba pamoja na utaratibu wa kubusu msalaba bali waumini wanatakiwa kutafakari na kuendelea kutoa sadaka.



Mkuu wa Kitengo cha Vipodozi wa ZFDA, Salim Hamad Kassim, akiwaonyesha waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, dawa ya kutakasa mikono (sanitizer) ambayo haina kiwango iliyotengenezwa na Kiwanda cha Oil Cam kilichopo Kiembesamaki, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaokaidi kutoa ushahidi mahakamani kupewa kibano

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Othman Khamis, ameitaka serikali kuwachukulia hatua watumishi wake ambao wanakataa kutoa ushahidi mahakamani na kusababisha baadhi ya kesi hizo kufutwa.

Aliyasema hayo akipokea taarifa ya matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika Mkoa wa Kaskazini ambapo taarifa inaonyesha baadhi ya kesi zimelazimika kufutwa baada ya kukosa ushahidi.

Alisema inasikitisha kuona kwamba mtendaji wa serikali anakataa kutoa ushahidi kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kulazimika kesi hizo kufutwa.

Alieleza kuwa kitendo cha jamii kukataa kutoa ushahidi maana yake kuwapa nguvu wahalifu wa matukio hayo kuendelea kutekeleza uovu na jamii kuathirika.

"Nimesikitishwa na tabia ya baadhi ya watendaji wa serikali kukataa kutoa ushahidi mbele ya mahakama kwa matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia,'" alisema.

Aidha, aliziomba taasisi za wafanyakazi ambao wamekataa kutoa ushahidi mahakamani kupelekewa majina yao ili yafikishwe mbele ya wizara husika.

Naye Ofisa Mipango wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto, Fatma Ali Kombo, alisema kuanzia Julai hadi Desemba mwaka 2019, jumla ya matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia yapatayo 150 yameripotiwa huku matukio 10 yakihusisha ulawiti.

Aidha, alisema matukio 12 yaliyoripotiwa ni mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema bado changamoto ya jamii kukataa kutoa ushahidi kwa wahusika wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ni kubwa, ikiwamo watumishi wa serikali.

"Bado jamii yetu haipo tayari kuona matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vinatokomezwa...matokeo yake kesi zinalazimika kufutwa Mahakamani," alisema.

# SMZ sasa yazuia uwindaji hifadhini

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imepiga marufuku uwindaji wa wanyama katika maeneo ya hifadhi ya taifa ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kulinda mazingira.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati akitoa gawio la Sh. milioni 400 kwa wanavijiji wanaozungukwa na msitu wa taifa wa Jozani ikiwa fedha zinazotokana na fidia za uharibifu wa mazao yao.

Mjawiri alisema serikali imechukuwa uamuzi huo kufuatia kujitokeza kwa tabia ya baadhi ya wananchi ikiwamo kusaka wanyama katika maeneo ya hifadhi ya taifa.

Alisema uwindaji wa wanyama katika maeneo ya hifadhi ya taifa kwa kiasi kikubwa husababisha uharibifu mkubwa ikiwamo kukamata wanyama ambao wanalindwa na sheria ya uhifadhi ikiwamo paa nunga.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapiga marufuku matukio ya uwindaji wa wanyama katika msitu wa hifadhi ya taifa baada ya kubainika kuwapo kwa hujuma za wanyama mbalimbali ambao baadhi wanalindwa na matukio ya hujuma,'" alisema.

Naye mwenyekiti wa umoja wa mashamba ya uhifadhi wa maendeleo ya msitu wa Jozani, Yussuf Mshenga, alisema bado yapo matukio ya uharibifu wa na uvamizi wa msitu wa hifadhi ya taifa unaofanywa na watu kwa ajili ya kukata kuni na mbao.

Alisema licha ya kuwapo kwa ulinzi katika kuingia maeneo ya situ huo, bado matukio ya uharibifu pamoja na vitendo vya wafugaji wa asali kuchoma moto na kusababisha hasara kubwa.

"Katika kipindi cha miaka miwili zaidi ya matukio ya janga la moto yameathiri msitu wa Jozani, ambao umesababisha na wafugaji wa asali," alisema.

Msitu wa Jozani umeingizwa katika orodha ya Hifadhi ya Taifa mwaka 2000 na unasifika kwa kuhifadhi viumbe vya baharini na baionuai nyingi na miti ya aina mbalimbali adimu.

**"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapiga marufuku matukio ya uwindaji wa wanyama katika msitu wa hifadhi ya taifa baada ya kubainika kuwapo kwa hujuma za wanyama mbalimbali ambao baadhi wanalindwa na matukio ya hujuma,'" alisema.**

## Mbunge azigawia shule vitabu 500

**Na Sabato Kasika**

SEKONDARI mbili za kata, Dan Mapigano Memorial na Busambara zilizopo Musoma Vijijini mkoani Mara, ambazo zilianza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu, zimepata msaada wa vitabu zaidi ya 500.

Vitabu hivyo vya masomo ya sayansi na vya Kiingereza vilitolewa wiki iliyopita na mdau wa elimu, Prof. Sospeter Muhongo, ambaye ni Mbunge wa Musoma Vijijini ili kusaidia kuinua kiwango cha elimu katika shule hizo.

Prof. Muhongo alisema ameipa kila shule maboksi 10 yenye zaidi ya vitabu 250, na kwamba idadi hiyo inatosha kwa wakati huu kwa vile ni sekondari mpya zenye kidato cha kwanza tu.

Alisema ataongeza vingine kadri itakavyowezekana, kwa kuwa elimu ni moja ya kipaumbele chake katika Jimbo la Musoma Vijijini, na kwamba ameamua kuanza na idadi hiyo ya vitabu.

Alisema amewaomba wakuu wa shule hizo kuwasiliana na mmoja wa wasaidizi wake jimboni, Fadison Masawa, ili wapate vitabu hivyo na kwenda kuvitumia katika shule zao.

"Dan Mapigano Memorial School ipo Kata ya Bugoji na Busambara Sekondari ipo Kata ya Busambara, na zote zilianza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza hivi karibuni," alisema Prof. Muhongo.

Alifafanua kuwa Musoma Vijijini kuna shule za sekondari 18 za serikali, mbili za binafsi na za msingi 111, na amekuwa akigawa vitabu katika shule zote hizo na kuhamasisha ujenzi wa maktaba.

"Sote tunajua elimu ndiyo kila kitu, hivyo ni muhimu kushirikiana na serikali katika uboreshaji wa miundombinu ya shule ili kupata wasomi wazuri wa badaye," alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Busambara, Faruku Yateri, alisema ameshawasiliana na msaidizi wa mbunge kwa ajili ya kuchukua vitabu hivyo ili vianze kutumiwa na wanafunzi wake.

"Kwanza kabisa nishukuru kwa msaada huo na pia ni kwamba wadau wa elimu wanahitajika kwa ajili ya kusaidia shule za umma kwa hali na mali ili kuinua kiwango cha elimu nchini," alisema Yateri.

Mwalimu Yateri alisema, shule hiyo bado ni changa, hivyo kupata msaada wa vitabu vya masomo ya Sayansi na lugha ya Kiingereza ni hatua nzuri na huenda wakajitokeza wadau zaidi wa kuisaidia.

# Ajinyonga mtini hadi kufa kisa wivu wa kimapenzi

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

MKAZI wa Mtaa wa Mbulu, Kata ya Mhongolo, wilayani hapa, aliyetambulika kwa jina moja la Maziku, amekutwa amefariki dunia baada ya kujinyonga juu ya mti mazingira ya nyumbani kwake karibu na kanisa.

Mwanaume huyo anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 28-30, maarufu kama baba Justine, amedaiwa kuchukua uamuzi huo kutokana na wivu wa mapenzi uliosababisha kuwapo kwa mgogoro kati yake na mke wake.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mbulu, Fikiri Gerlad, akizungumza jana na vyombo vya habari eneo la tukio, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kudai kuwa muda aliojinyonga haufahamiki isipokuwa majira ya saa mbili asubuhi alipokea taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa huo, Hamza Abdalah, kuwa kuna mwananchi amekutwa amejinyonga kwa kutumia shati lake maeneo ya nyumbani kwake huku mwili ukiwa unang'inia juu ya mti.

Alidai kuwa marehemu alikuwa ni mkazi mpya katika eneo hilo ambaye ana miezi miwili tangu ahamie na awali alikuwa akiishi katika mtaa wa Nyakato, kata ya Nyasubi mjini Kahama na kuongeza kuwa hata alipohamia katika mtaa wao hakutaka kujisajili katika kitabu cha makazi.

"Mama wa familia na watoto walikimbia kabla ya kujinyonga huyu bwana na kwenda kusikojulikana, ni vizuri watu wakafika mochwari ili kutambua mwili baada ya polisi kuupeleka mwili ili kuwafahamisha ndugu ambao mnawajua," alisema.

Awali, Mchungaji wa Kanisa la Pentecostal, Grigal Julius, alidai kuwa Maziku alikuwa muumini wake kanisani na kutaja chanzo cha mgogoro ni mwanaume kumhisi mkewe kuwa anatoka nje ya ndoa na kuchukua uamuzi mgumu wa kujitoa uhai wake.

"Mimi na katibu wangu wa kanisa tulikuwa tukisuluhisha mgogoro wa ndoa yao mara kwa mara, juzi (Jumapili) tukiendelea na suluhu hiyo mwanaume alimtuhumu mkewe kutoka nje ya ndoa huku mwanamke naye akidai yeye ni mfanyabiashara wa mahindi ya kupika hivyo mumewe alimkuta eneo la maegesho ya magari makubwa yanayokwenda Rwanda na Burundi akiwahudumia wanaume ndio chanzo cha mzozo wao," alidai.



Mchuuzi wa kahawa akiwahudumia wateja jirani na dampo la takataka katika eneo la Machinga Complex, Ilala, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kitendo ambacho ni hatari kiafya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hospitali yafunga mfumo wa maji kuikabili corona

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

KATIKA kujikinga na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga imefunga mfumo wa maji na masinki ya maji nje ya malango mkubwa wa hospitali ya halmashauri hiyo, kwa ajili ya watu wanaofika kuona wagonjwa.

Hatua hiyo itawawezesha kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka bila usumbufu wowote.

Akizungumza na wanahabari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Anderson Msumba, alisema mfumo huo umeshafungwa ambapo zaidi ya mabomba kumi yanatarajia kukamilika, na kuwa yamekamilika manne na wananchi watakuwa wanatumia masinki hayo kunawa mikono kabla na baada ya kuingia kuona wagonjwa.

Amesema kwa wanaopita na magari wameweka utaratibu wa kuwapulizia dawa mikononi na kwenye magari yao ili kuzuia maambukizi ya virusi hivyo, na kwamba wanampima joto la mwili kila mtu anayeingia hapo baada ya kunawa mikono.

Dk. Msumba alisema kuwa wameweka mtu katika lango kuu la kuingia na kuwapima joto la mwili kwa kutumia kipimia joto.

Aidha, alisema halmashauri hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo, na kuwataka wananchi kuzingatia maelekezo wanayopewa na viongozi wa serikali.

Neema Juma na Makoye Joseph, wakazi wa Kahama waliofika kuona wagonjwa katika Hospitali ya Mji wa Kahama, waliipongeza halmashauri kwa kujenga wabomba nje ya geti la hospitali, hivyo kumfanya kila mmoja aweze kunawa.

HABARI KIMATAIFA

## Raia waendelea kusubiri matokeo ya uchaguzi Mali

**BAMAKO,** Mali

TUME ya uchaguzi nchini Mali imesema kuwa zoezi la kuhesabu kura linaendelea nchini humo, ikiwa ni siku moja tu baada ya wananchi kushiriki uchaguzi wa wabunge mwishoni mwa wiki.

Uchaguzi huo, ambao kabla ulipangwa kufanyika mwaka 2018 uliahirishwa mara mbili kwa sababu ya kuongezeka machafuko kwenye majimbo ya kati na Kaskazini mwa nchi hiyo, ambako serikali inapambana na makundi ya itakadi kali.

Uchaguzi huo unafanyika licha ya taifa hilo la Afrika Magharibi kukabiliwa na changamoto ya usalama, kiongozi wa upinzani kutekwa na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Wachambuzi wa masuala ya siasa nchini humo wanasema uchaguzi huo ni muhimu kwa sababu utasaidia kukabiliana na machafuko na kuleta suluhu ya kisiasa katika maeneo yaliyoathiriwa. **RFI**

## Afghanistan yatangaza timu ya mazungumzo na Taliban

**KABUL,** Afghanistan

SERIKALI ya Afghanistan imetangaza timu ya wajumbe 21 itakayoshiriki mazungumzo na Taliban, katika kile kinachotajwa kama ishara ya matumaini ya mazungumyo ya amani yanayosimamiwa na Marekani.

Timu hiyo iliyotangazwa mwishoni mwa wiki na taasisi maalumu ya kitaifa inayoshughulikia amani, inaongozwa na mfuasi wa Rais Ashraf Ghani, Masoom Stanekzai na imejumuisha wanasiasa, maofisa wa zamani, wawakilishi wa vyama vya kiraia. Watano miongoni mwao ni wanawake.

Haikujulikana mara moja iwapo mpinzani wa kisiasa wa Rais Ghani, Abdullah Abdullah pia atataja timu ya wajumbe walioteuliwa, ambayo wanadiplomasia wamesema itakuwa muhimu kwa kuzingatia ushawishi wa upande wake katika sehemu kubwa ya kaskazini na magharibi mwa nchi hiyo. **DW**

# Walioambukizwa corona Rwanda wafikia 70

**KIGALI,** Rwanda

**Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Rwanda ilitangaza kufunga mipaka yote ya nchi hiyo na watu kuamrishwa kusalia majumbani mwao katika juhudi za kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.**

WIZARA ya Afya nchini Rwanda imethibitisha maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona kwa watu 10 zaidi siku ya Jumapili na kufikisha idadi ya watu 70.

Akilihutubia taifa usiku wa Ijumaa, Rais Paul Kagame alisema idadi hiyo itaendelea kuongezeka kwa sababu wale waliochanganyika na waathirika wanaendelea kutafutwa.

Taarifa iliyotolewa na wizara ya afya nchini humo ilieleza kuwa katika matukio ya hivi karibuni watu sita walitokea Dubai, wawili Afrika Kusini, mmoja kutoka Nigeria na mwingine alikuwa amesafiri maeneo ya Afrika Mashariki. Ilieleza taarifa ya Wizara ya Afya nchini humo.

Rwanda kwa sasa ina jumla ya wagonjwa 70 wa corona, 32 kati ya hao waliwasili kutoka Dubai.

Wiki iliyopita Waziri wa Afya wa Rwanda alikiambia kituo cha televisheni cha Rwanda kwamba hali hiyo ya maambukizi ilitokea baada ya wafanyabiashara wengi wa Rwanda kurejea nyumbani kutoka Dubai, serikali ilipotangaza kuwa itafunga mipaka yote ya nchi.

Rwanda inaongoza kwa visa vya maambukizi ya ugonjwa wa corona katika ukanda wa Afrika Mashariki ikiwa na wagonjwa 70, ikifuatiwa na Kenya 42, Uganda 33, Tanzania 14, huku Burundi na Sudan Kusini zikiwa hazijarekodi visa vyovyote vya maambukizi.

Jumapili Rwanda ilianza wiki ya pili ya kukaa nyumbani ili kudhibiti kuenea kwa virusi.

Katika hotuba yake kwa taifa, Rais Kagame alisema serikali inatoa msaada wa chakula kwa familia zisizojiweza na ambazo zimeathiriwa na amri ya kukaa nyumbani.

Mamlaka nchini humo Jumamosi zilianza shughuli ya kugawa chakula mjini Kigali kwa kuzitambua familia maskini zinazojikimu kutokana na shughuli za kila siku.

Maelfu ya familia zinatarajiwa kupokea vyakula vya msaada kutoka kwa serikali mchakato wa utambuzi utakapokamilika.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Rwanda ilitangaza kufunga mipaka yote ya nchi hiyo na watu kuamrishwa kusalia majumbani mwao katika juhudi za kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Hatua zingine zilizochukuliwa ni pamoja na watumishi wote wa serikali na sekta binafsi kufanyia kazi nyumbani na safari za kwenda mikoani kusitishwa kwa wiki mbili kukiwa na uwezekano wa muda huo kuongezwa.

Vilabu vya pombe na maduka yasiyo ya chakula pia yamefungwa huku usafiri wa bodabobda ukisitishwa.

Hatua hiyo ilichukuliwa siku moja baada ya Wizara ya Afya ya Rwanda kutangaza kuwa watu wengine sita wameambukizwa virusi vya corona miongoni mwao mtoto mchanga wa miezi 10. **BBC**



Rais Donald Trump akiongea na waandishi wa habari kabla ya kuondoka kuelekea Norfolk, Virginia. **PICHA: REUTERS**

# Trump: Hakuna kuanzisha karantini New York

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amebadilisha kauli yake ya kufikiria kuanzisha karantini kudhibiti maradhi yanayotokana na virusi vya corona katika maeneo yaliyoathiriwa zaidi ya New York, New Jersey na Connecticut.

Badala yake ameamrisha umakini uongezwe zaidi kwa wasafiri ili kuzuia kuenea kwa mlipuko huo.

Makamu wa Rais, Mike Pence, alituma ujumbe katika mtandao wa kijamii wa Twitter akisema Kituo cha Kuzuia Maradhi (CDC) kinataka wakazi wote wa majimbo hayo matatu kutofanya safari ambazo siyo muhimu kwa kipindi cha siku 14 zijazo.

Fikra ya karantini ilikuwa imehamasishwa na magavana kadhaa, akiwamo Ron DeSantis wa Florida ambaye alitaka kuzuia wasafiri kutoka maeneo yaliyoathirika zaidi kuingia katika majimbo yao.

Lakini hilo lilikosolewa mara moja na viongozi wa majimbo hayo yanayojadiliwa, ambao walitahadharisha itasababisha wasiwasi katika jamii ambayo tayari inaadhibika kutokana na virusi hivyo.

Rais Trump alitangaza kufikia uamuzi huo baada ya kushauriana na kikundi kazi cha White House kinachoongoza harakati za serikali kuu za kukabiliana na mlipuko wa corona na magavana wa majimbo hayo matatu.

Alisema amewaagiza CDC kutoa ushauri makini wa kusafiri utakaosimamiwa na magavana, wakishauriana na serikali kuu huku akisisitiza kuwa karantini haitahitajika.

Gavana Andrew Cuomo wa New York, ambaye alikosoa serikali kuu inavyokabiliana na maradhi hayo wakati jimbo lake likiwa ni chimbuko la maambukizi alisema kuyatenga majimbo itakuwa sawa na serikali kuu kutangaza vita.

Alisema suala la uwezekano wa kuwapo karantini hazikujadiliwa wakati wa mazungumzo yake na Rais Trump mwishoni mwa wiki akiongeza kuwa anaamini itakuwa ni kinyume cha sheria, balaa la kiuchumi, upuuzi na upeo mdogo wakati maeneo mengine ya Marekani yanashuhudia kuongezeka kwa maambukizi hayo.

Alisema kuyatenga makao makuu ya kiuchumi ya taifa (New York) utaleta mtikisiko katika soko la hisa na kudhoofisha uchumi wakati ambao Rais Trump alieleza anahangaika kurejesha hali ya uchumi mahali pake.

Rais Trump alitoa kauli yake ya awali alipokuwa yuko njiani kuelekea mji wa Norfolk, Virginia, kushuhudia kuondoka kwa meli ya jeshi la majini ambayo ni hospitali ikielekea jijini New York kusaidia kukabiliana na mlipuko wa janga la corona.

Katika tukio hilo, alizungumza na kundi dogo lililokuwa katika kituo hicho cha kijeshi na kuwatahadharisha kuchukua hatua za kujikinga. **VOA**

# Mjasiriamali zana za chuma aundiwa kamati ya kumsaidia

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

TIMU ya wataalamu tisa kutoka wizara nne imeundwa kumsaidia mjasiriamali kutoka Ludewa mkoani Njombe, Reuben Mtitu (60), maarufu kama Mzee Kisangani, ili kutimiza ndoto yake ya kuwa bilionea baada ya kubuni kiwanda kinachotengeneza zana zinazotokana na madini ya chuma.

Wataalamu hao wanatoka Wizara ya Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Kamati hiyo ilitangazwa kuundwa jana na mawaziri Doto Biteko (Madini) na Mussa Zungu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na naibu mawaziri Mwita Waitara (Tamisemi) na Mhandisi Stella Manyanya wa Viwanda na Biashara.

Mawaziri hao walitangaza kamati hiyo katika kikao kilichofanyika ukumbi wa mikutano Wizara ya Madini jijini Dodoma. Wengine waliohudhuria ni kutoka Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na wataalamu kutoka Wizara ya Madini na Tume ya Madini.

Akifungua kikao hicho, Waziri Biteko aliwaeleza wajumbe hao kuwa lengo ni kujadili namna ya kumsaidia Mzee Kisangani kwenye kila hatua kutoka mahali alipo hadi kufikia ndoto yake ya kuwa bilionea.

"Mzee Kisangani hajui kusoma wala kuandika, lakini ameonyesha kitu ambacho serikali inahitaji kumsaidia kwa kila hatua anayohitaji," alisema Biteko.

Biteko alisema alipokuwa ziarani Njombe kuanzia Machi 13 hadi 16, mwaka huu, alitembelea kiwanda chake ambacho kwa namna kilivyo kinatengeneza zana mbalimbali za chuma kama vile mapanga, mafyekeo, visu na majembe huku akiwa amewaajiri watu 30.

Kutokana na uthubutu na juhudi alizo nazo. Biteko aliahidi kukutana na mawaziri wote wanaohusiana na shughuli zake ili kujadili namna ya kumsaidia.

Kwa upande wake, Zungu alisema Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia NEMC, itahitaji andiko la kibiashara kwamba wataalamu wa eneo hilo watasimama ipasavyo kumsaidia kufikia ndoto yake.

Wakati Zungu akihitaji andiko, Biteko alisema tayari Chuo Kikuu cha Mzumbe walishajitolea kumwaandalia andiko la biashara ya kiwanda chake.

Naye Waitara alisema kila mkoa ulipewa agizo la kuandaa maeneo ya uwekezaji, hivyo Mkuu wa Mkoa wa Njombe atatoa eneo maalum kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda cha Kisangani kwenye eneo lililotengwa.

Manyanya kwa upande wake alisema kumekuwa na changamoto nyingi za kuwasaidia watu wenye ubunifu hususani kutokana na vipengele vilivyowekwa kisheria suala ambalo huwakatisha tamaa.

Alisema wizara yake kupitia Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) na lile la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda (Tirdo) kila moja litatoa mtaalamu kwa ajili ya kumsaidia mjasiriamali huyo ili afikie malengo yake.

Mkurugenzi Mkuu wa NDC, Prof. Damian Gabagambi, alisema mara baada ya kusoma taarifa za ziara ya Waziri Biteko kupitia vyombo vya habari, alituma wataalamu kwenda kiwandani hapo na kuona namna ya kumsaidia ili kuzalisha chuma na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa bidhaa.

Walioteuliwa kuunda kamati hiyo na taasisi wanazotoka kwenye mabano ni Wilfred Machumu (Tume ya Madini), Issa Mtuwa (Wizara ya Madini), Abbas Mruma (GST), Prof. Silvester Mpanduji (Sido), Prof. Madundo Mkumbukwa (Tirdo), Dk. Yohana Mtoni (NDC), Anorld Mapinduzi (NEMC), Leo Mavuka (Tamisemi) na Dk. Hellen wa Chuo Kikuu Mzumbe.



Diwani wa Kata ya Mtoni, Benard Mwakyembe (wa pili kushoto), akipata maelezo ya ujenzi wa soko la muda kutoka kwa Kaimu Ofisa Mtendaji Kata ya Mtoni, Sepeku Mhina (kushoto), wakati alipokagua ujenzi wa soko hilo, wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima wailalamikia Amcos kuwalangua dawa

**Na Anthony Gervas,** MAGU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, wamevilalamikia vyama vya msingi vya ushirika na mazao (Amcos), kuwauzia bei kubwa wakulima wa zao la pamba dawa ya kuua wadudu.

Diwani wa Kata ya Ng'haya, Gelrad Robert, alitoa malalamiko hayo yaliyoungwa mkono na madiwani wengine, mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, kilichofanyika mjini humo.

"Inasikitisha vyama vya msingi vya ushirika na mazao kuwauzia wakulima wa pamba dawa za kuua wadudu kwa bei kubwa, wakati dawa ile ile katika maduka binafsi ya pembejeo za kilimo inauzwa lita moja Sh. 15,000, lakini wao wanawauzia Sh. 22,500," alisema Robert.

Alitoa angalizo kuwa Amcos na serikali wanatakiwa kuwasaidia wakulima badala ya kuwaumiza kwa kuwa msimu ujao wakulima wengi wanaweza kukata tamaa kuendelea na kilimo hicho na kuhamia kwenye mpunga.

Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Philimon Sengati, alisema serikali itahakikisha inalisimamia suala hilo badala ya kuachia dawa hiyo kuuzwa kiholela na kufuata taratibu miongozo na sheria hata kama ni soko huria.

"Serikali tutachukua hatua za kuhakikisha tunadhibiti uuzwaji holela wa dawa hizo katika maduka binafsi ya pembejeo za kilimo, hata kama ni soko huria, haiwezekani soko likajiendesha lenyewe bila usimamizi," alisema Sengati.

Kadhalika, Sengati alisema kazi kubwa ya serikali ni kusimamia shughuli zote za maendeleo ya wananchi, ikiwamo kutatua kero zao, kuboresha miundombinu mbalimbali ya kijamii, kilimo cha mazao ya kimkakati na yasiyokuwa yakimkakati kama vile, soya, dengu, choroko, mbaazi na ufuta.

# Wamachinga wahakikishiwa soko lao Samunge

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewahakikishia wamachinga kuendelea kufanyabiashara kwenye soko la Samunge, Halmashauri ya Jiji la Arusha, lililoungua moto juzi na kuwaondolea hofu ya uvumi wa kuwapo mpango wa kuwaondoa.

Akiongea jana katika soko hilo na wafanyabiashara zaidi ya 3,000, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, aliiagiza Halmashauri ya Jiji la Arusha kuharakisha ujenzi wa miundombinu ya soko hilo, ili kuwapa nafasi wafanyabiashara kuendelea na shughuli zao.

Alisema hakuna mfanyabiashara yeyote aliyekuwa anafanyabiashara katika soko hilo atakayeondolewa bali serikali inahitaji kuweka sawa hali ya ufanyaji wa biashara ndani ya soko hilo.

"Niwatoe hofu hakuna mtu atakayeondolewa ndani ya soko hili, kama maneno yanavyopita chini chini msiyasikilize kwa kuwa serikali inahitaji kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji wa biashara na ndani ya siku saba itakuwa teyari," alisema Daqarro.

Alisema, halmashauri itaendelea kufanya tathmini ya miundombinu rafiki kwa majanga, ili kuondoa changamoto iliyojitokea wakati wa kuzima moto ikiwamo kuweka nafasi za kupita kwa magari ndani ya soko hilo.

Katika hatua nyingine Daqarro ameagiza kufungwa kwa barabara mojawapo iliyo kando ya soko hilo, ili kutoa fursa kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao bidhaa zao hazikuunguliwa na moto kuendelea na biashara zao hadi miundombinu ya soko hilo itakapokuwa tayari.

Aliwataka wafanyabiashara waliounguliwa kufanya usafi na kutoa mabaki ya mabati na bidhaa, ili kupisha soko hilo kufanyiwa marekebisho haraka.

Naye Mwenyekiti wa wamachinga Mkoa wa Arusha, Amina Njoka, aliishukuru serikali kwa kuwaruhusu kuendelea kufanya biashara katika soko hilo, kwa kuwa walikuwa hawajui hatima yao.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**SIMBA LOGISTIC EQUIPMENT SUPPLY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 179 DNC TRUCK** HORSE, yenye Chassis namba **LZZ5CLSB4JD400313.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 101 DMU TRAILER,** yenye chassis namba **NP9GA02W3JK025004.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/266572/2020.**

115684702


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GUNDOGAN: SINA TATIZO LIVER KUPEWA UBINGWA

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Ilkay Gundogan hatakuwa na tatizo lolote kama Liverpool watapewa ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu huu, baada ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa ubingwa wa corona.

Mechi zote za Ligi Kuu ya England zimesimamishwa hadi angalau Aprili 30 mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya COVID-19 vinavyosababisha corona, huku pia ikitarajiwa ligi hiyo kuendelea tena kwa kuchezwa bila mashabiki uwanjani.

Wakati ligi hiyo imesimama, Liverpool wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi Liverpool 25 kileleni.

Kutokana na gepu hilo kubwa la pointi, wachambuzi wa soka wanaona kama Liverpool ipewe taji la Ligi Kuu na kiungo huyo wa City ambao ni mabingwa watetezi, hana tatizo na hilo.

"Itakuwa poa tu kwa upande wangu (kama Liverpool watapewa taji), unatakiwa kuwa mwanamichezo," amesema Gundogan akiiambia ZDF.

Sio tu Ligi Kuu ya England ambayo imelazimika kusimamishwa, pia ligi za nchi zote tano kubwa za Ulaya pamoja na ligi ya madaraja ya chini.

# Jovic anajiharibia mwenyewe – Kocha

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Luka Jovic anafanya kila kitu anachoweza "kuharibu kazi yake", kwa mujibu wa kocha wa zamani wa Eintracht Frankfurt na raia mwenzake wa Serbia, Dragoslav Stepanovic.

Jovic amekuwa na mwanzo mgumu katika msimu wake wa kwanza kwa miamba hao wa soka la Hispania, baada ya kutua hapo akitokea Eintracht, akifunga mabao mawili tu katika mechi 24 kwenye mashindano yote.

Aliingia kweye matatizo mapema mwezi huu baada ya kuvunja amri ya kujitenga kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Jovic, ambaye amerudi nchini kwake Serbia baada ya msimu wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kusimamishwa kutokana na corona, alilaumiwa kwa kutozingatia maelekezo.

Stepanovic, ambaye aliinoa Bayer Leverkusen na Athletic Bilbao, hafurahishwi na tabia ya Jovic na amesema anahitaji kubadilika ili kuendelea kufurahia kipaji chake.

"Ni yeye mwenyewe ambaye anafanya kila kitu kuharibu kipaji chake," amesema kocha huyo akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Jovic anajimaliza mwenyewe. Alikuwa na bahati kwamba Adi Hutter (kocha mkuu wa Eintracht) alimpa nafasi pale Eintracht na halafu akafanya usajili mkubwa kwenye historia ya Serbia na kutua Rea Madrid. Nashindwa kuelewa kijana kile anachofanya.

"Nilisoma kwenye vyombo vya habari vya Serbia na najua maisha gani aliyoishi wakati akiwa mtoto, alilala kwenye gari na baba yake kusubiri treni hadi asubuhi. Sasa sijui kwanini anataa kuharibu maisha yake mwenyewe.

"Sijui kwanini, Luka hajifikirii kuhusu yeye mwenyewe na kule alikotoka."





# Petit amtaka Guardiola ajiondokee Man City

**LONDON,** England

EMMANUEL Petit amesema kwamba, kufungiwa kwa miaka miwili kwa Manchester City kutoshiriki michuano ya Ulaya kunaweza kumpa kocha Pep Guardiola 'nafasi ya kuachia ngazi.'

City walipigwa marafuku ya miaka miwili ya kutoshiriki mashindano yanayoandaliwa na Uefa Januari kwa kuvunja sheria ya usawa wa manunuzi, hata hivyo, wamekata rufani kwa mahakama ya usuluhishi wa michezo.

Na sasa kiungo wa zamani wa Arsenal na Chelsea, Petit anaamini kifungo hicho kinaweza kumpa Guardiola nafasi ya kuondoka kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu, sawa na wakati alipokuwa anaondoka Barcelona mwaka 2012.

"Nafikiri hii inaweza kuwa nafasi kwa upande wake kuondoka City kipindi cha majira ya joto kwa sababu ya kufungiwa kutocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya," amesema Petit akinukuliwa na gazeti la The Mirror.

"Inaweza kuwa nafasi kwa upande wake kuachia ngazi na kuwa na mapumziko. Kuna wakati aliondoka na kuamua kupumzika katika nafasi ya ukocha na anaweza kufanya hivyo sasa."

Guardiola alichukua mwaka mmoja wa mapumziko baada ya kuinoa Barcelona kwa miaka minne kutoka mwaka 2008 hadi 2012, kabla ya kuchukua mikoba ya kuinoa Bayern Munich. Raia huyo wa Hispania alihamia kwa Man City mwaka 2016, na ametwaa mara mbili taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji matatu ya ligi na moja la FA.

HABARI MICHEZO

# Cavani asubiriwa kutua Boca Juniors

**BUENOS AIRES,** Argentina


MKURUGENZI wa soka wa Boca Juniors, Jorge Bermudez ana matumaini nyota wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani, atajiunga na miamba hao wa soka la Argentina "haraka sana".

Cavani atamaliza mkataba wake Juni mwaka huu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale PSG baada ya kushindikana kwa usajili wa kutua Atletico Madrid wakati wa dirisha dogo la Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 mfungaji wa wakati wote wa PSG – pia ameripotiwa kuhusishwa na mpango wa kutua kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, katika Klabu ya Inter Miami.

Lakini Bermudez anaamini Boca, ambako kwa sasa gwiji wake, Juan Roman Riquelme ndiye makamu wa rais, anaweza kumvuta fowadi huyo kwenye jiji hilo la Buenos Aires.

"Kwa kumjua Riquelme na ukaribu wa mchezaji wa zamani wa Uruguay, Diego Forlan, wote wakiwa wanamjua vizuri Cavani, natumaini atajiunga nasi haraka sana," amesema Bermudez akiiambia redio Cooperative.






# BENZEMA AKATAA KABISA KULINGANISHWA NA GIROUD

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Karim Benzema amesema "ni sawa na kulinganisha magari ya Formula One na yale ya mota" wakati akikataa kulinganishwa na mshambuliaji mwenzake wa Ufaransa, Olivier Giroud.

Benzema hajaichezea Ufaransa tangu Oktoba 2015, baada ya kocha, Didier Deschamps kukataa kumuita nyota huyo wa Madrid, badala yake akamgeukia fowadi wa Chelsea, Giroud.

Alipoulizwa kuhusu kulinganishwa kwake na Giroud katika kipindi cha maswali na majibu kwenye mtandao wa Instagram, Benzema alitumia mfano wa mbio za magari za Formula One na magari yanayotumia mota ambayo hayana kasi kubwa.

"Usilinganishe Formula One na magari ya mota," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kupitia kwenye Instagram. "Najua kwamba mimi ni Formula 1.

"Ana maisha yake, anafanya kile anachokifanya, anafunga mabao anayoyataka. Yupo kwenye mstari wake, mimi nipo kwenye mstari wangu, sifikirii kuhusu yeye.

"Kwa upande mwingine anaichezea timu ya taifa. Anafanya vizuri kwa sababu yuko pale.

"Yupo vizuri kwa sababu kuna wachezaji kama Mbappé au Griezmann ambao wana kasi na wanaweza kucheza sehemu zao kwa ufanisi mkubwa."

# *Manchester United yaongeza kasi kumtwaa Niguez*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United 'wameongeza imani kwamba wanaweza kumsajili Saul Niguez kwa ada itakayoweka rekodi ya klabuni hapo ya pauni milioni 135' wakati wakitafuta mbadala wa Paul Pogba.

Klabu hiyo inayotumia dimba la Old Trafford kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na kumuwania kiungo huyo wa Atletico Madrid na walituma maskauti kumwangalia Niguez wakati akisaidia kuwatupa nje Liverpool katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema mwezi huu.

Na kwa mujibu wa gazeti la The Daily Star, Ole Gunnar Solskjaer amepokea ripoti nzuri, ikithibitisha kwamba Niguez ndio kipaumbele chao cha kwanza kwenye dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

Wakati Pogba akitarajiwa kuondoka ndani ya miezi inayokuja, Real Madrid inatajwa kumuwania kiungo huyo wa Ufaransa mwenye thamani ya pauni milioni 100, na United watawekeza fedha hizo kwa ajili ya kumsajili nyota wa Hispania Niguez mwenye umri wa miaka 25.


Niguez ana kipengele kwenye mkataba wake wa miaka tisa na Atletico, kwamba atauzwa kwa pauni milioni 135 na United wanajiandaa kufikia bei hiyo, na kuvunja rekodi ya pauni milioni 89 waliyomnunulia Pogba kutoka Juventus mwaka 2016.

Atafiti kwenye daraja la wachezaji wakubwa duniani, lakini bado kijana na mwenye kipaji na hivyo utakuwa wakati mzuri kwa Solskjaer kukijenga kikosi chake vizuri zaidi.

Niguez anaweza kufiti kwenye safu ya kiungo ya United sambamba na Bruno Fernandes raia wa Ureno, ambaye ameanza vizuri maisha yake pale Old Trafford baada ya kusajiliwa kutoka Sporting Lisbon Januari.

Mchezaji huyo alisaini mkataba mnono na Atletico mwaka 2017 ambao unamalizika mwaka 2026.

Saul amefunga mabao manne katika mechi 37 alizoichezea Atletico msimu huu, likiwamo bao la kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya Liverpool.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE SASA AANZA KUAGA TOTTENHAM

Mimi ni mchezaji mwenye tamaa, nataka kushinda makombe mapema badala ya baadaye...

**LONDON,** England

HARRY Kane, ambaye bado ana mkataba na Spurs hadi mwaka 2024, amesema anaweza kuondoka klabuni hapo kama timu hiyo haitasonga mbele kwa sababu anataka kushinda makombe "mapema badala ya baadaye".

Tottenham imetolewa nje kwenye michuano yote msimu huu na ipo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England kabla ya mechi za ligi hiyo kuahirishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19). Na taji la mwisho kwa klabu hiyo lilikuwa ni Kombe la Ligi mwaka 2008.

**"Mimi ni mchezaji mwenye tamaa, ninataka kujizatiti na kuwa bora," aliongeza Kane ambaye hadi sasa amefunga mabao 11 msimu huu. "Ninataka kuwa mchezaji wa kiwango cha juu, juu kabisa.**

"Si dhahiri: 'Nitaendelea kubaki pale milele.' Lakini si 'hapana' pia.

"Mara zote naipenda Spurs, lakini ni moja kati ya vitu hivyo. Mara zote ninasema kama sioni tunapoendelea mbele kama timu ama kwenda katika mwelekeo sahihi, mimi si mmoja wa kubaki pale kwa sababu yao tu."

Katika hatua nyingine mshambuliaji huyo wa England, Kane amesema msimu wa Ligi Kuu England unapaswa kufutwa kama hautaweza kumalizika Juni mwaka huu.

Michuano yote mikubwa ya soka nchini England imeahirishwa angalau hadi Aprili 30, mwaka huu kwa sababu ya mlipuko wa janga la virusi vya corona.

"Ninajua Ligi Kuu England itafanya kila linalowezekana kumaliza msimu," alisema mshambuliaji huyo wa Tottenham, Kane.

"Kunahitajika kuwa na pointi ambayo inatosha. Labda kikomo kwangu ni mwishoni mwa Juni."

## ZISIKUPITE

### MANE AU AUBAMEYANG REAL

REAL Madrid inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30, lakini ni kama tu itashindwa kuipata saini ya straika Mnorway Erling Braut Haaland, 19, kutoka Borussia Dortmund ama mshambuliaji wa kimataifa wa Senegal, Sadio Mane, 27, kutoka Liverpool. ***(Express)***

### UPAMECANO AVUTA VIGOGO

REAL Madrid inajiandaa kuingia vitani na Arsenal, Barcelona na Bayern Munich kuisaka saini ya beki wa RB Leipzig, Dayot Upamecano majira haya ya joto. ***(Daily Mail)***

### RAMSEY, POGBA KUPISHANA

AARON Ramsey anajiandaa kujiunga na Manchester United katika mpango utakamhusisha Paul Pogba kuelekea upande wa pili wakati huu Ole Gunnar Solskjaer akielezwa kuwa shabiki mkubwa wa nyota huyo wa Juventus. ***(The Sun)***

### GOMES AWINDWA MADRID

REAL madrid inataka kumsajili kiungo Mbrazili Igor Gomes, 21, ambaye anaweza kuigharimu pauni milioni 45 kutoka pale Sao Paolo. ***(AS - in Spanish)***

### SANCHO AIKUBALIA UNITED

WINGA wa Borussia Dortmund, Jason Sancho, 20, rasmi atajiunga na Manchester United, na wakati nyota huyo wa kimataifa wa England akitarajiwa kuigharimu pauni milioni 116. ***(Irish Independent)***

### NEWCASTLE, BRADY, HENDRICK

NEWCASTLE United ipo tayari kuwasajili kwa uhamisho huru viungo wawili wa Burnley, Robbie Brady na Jeff Hendrick, kila mmoja akiwa na umri wa miaka 28. Wachezaji hao wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland watamaliza mikataba yao hapo Turf Moor katika majira ya joto. ***(Newcastle Chronicle)***

### MKHITARYAN KUJIFUNGA

KIUNGO wa Arsenal, Henrikh Mkhitaryan anatumai kuubadili mkataba wake wa mkopo hapo Roma kuwa wa kudumu katika dirisha la usajili la majira ya joto. Arsenal inataka pauni milioni 18 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Armenia mwenye umri wa miaka 31, lakini miamba hiyo ya Italia inataka kutoa pauni milioni 10 tu. ***(Mail)***

### XAVI ATAKA KAZI LALIGA

NGULI wa Barcelona na Hispania, Xavi amesema yupo tayari kuinoa klabu ya La Liga lakini akasisitiza hakuwezi kuwa na "sumu" yoyote katika chumba cha kubadilishia. ***(La Vanguardia - in Spanish)***

### NIGUEZ KUWEKA REKODI UTD

MANCHESTER United imeongeza kujiamini kuwa itamsajili kiungo wa Hispania na Atletico Madrid, Saul Niguez, 25, kwa ada itakayoweka rekodi klabuni hapo kiasi cha pauni milioni 135. ***(Daily Star)***

### EVERTON NA UWANJA MPYA

EVERTON bado inamatumaini ya kupata ruhusu ya mapendekezo yao ya uwanja mpya majira haya ya joto licha ya kuwapo kwa janga la virusi vya corona. ***(Liverpool Echo)***

HABARI MICHEZO

## Corona yakalia rufani ya U-17

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema rufani iliyokatwa kupinga Uganda kuchezesha wachezaji 'vijeba' katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa Wasichana wa umri chini ya miaka 17, imechelewa kusikilizwa kutokana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19).

Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF, Oscar Milambo (pichani), aliliambia gazeti hili kuwa rufani hiyo bado haijasikilizwa kutokana na changamoto ya kiafya iliyopo tangu mlipuko wa virusi vya corona.



Milambo alisema anaamini hali itakapotengemaa, mabosi katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), watakutana na hatimaye uamuzi kuhusiana na malalamiko hayo yatatolewa.

"Ninaamini bado tuna nafasi, kama yale malalamiko yetu yataangaliwa vizuri, kama Uganda haijachezesha wachezaji wakubwa, basi wachezaji hao watakuwa na uzoefu mkubwa, maana baadhi yao wameanza kuitumikia timu ya Taifa ya Uganda (She-Cranes), tangu mwaka 2017," alisema Milambo.

Tanzania ilitolewa katika mashindano hayo baada ya kufungwa mabao 5-0, na matokeo ya jumla yakawa 6-2.

## KVZ yamrejesha Shekha kikosini

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa KVZ FC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar imetangaza kumrejesha kocha wake wa zamani, Shekha Khamis ili iweze kufanya vizuri katika ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katibu Msaidizi wa timu hiyo, Khamis Abdulhamid, alisema wameamua kumrejesha Shekha kwa sababu anaifahamu vema timu hiyo na msimu wa 2018/19 aliiongoza kumaliza katika nafasi ya pili.

Kiongozi huyo alisema mipango ya KVZ pamoja na kocha huyo ni kuhakikisha timu hiyo inachukua ubingwa au inamaliza katika nafasi tano za juu.

"Mipango yetu pia ni kuhakikisha hatushuki daraja, tupo katika harakati za kuhakikisha timu inabaki kwenye Ligi Kuu, tumeshazungumza na wachezaji pamoja na walimu wetu na kuwaambia jitihada zaidi zinahitajika ili tukamilishe mpango huu ingawa ni mgumu," alisema kiongozi huyo.

KVZ ambayo imecheza michezo 23 na kushinda mechi nane, sare nane na kufungwa michezo saba, iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16.

# NAMUNGO KUTOSAJILI NYOTA SIMBA, YANGA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Namungo FC umesema mikakati yao ya usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara hautaangalia nyota wanaotemwa kutoka katika klabu kongwe za Simba na Yanga.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu alisema wachezaji kutoka Simba au Yanga hawatapa nafasi katika kikosi chao kutokana na kutojituma ipasavyo.**

Zidadu alisema uongozi wa klabu hiyo umeamua kutoa kipaumbele cha kusajili wachezaji ambao wanatoka katika timu nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara au Ligi Daraja la Kwanza.

Kiongozi huyo alisema mambo mawili wanayoyakwepa kuwasajili wachezaji wanaotemwa na timu hizo kubwa ni baadhi yao kutofikia matarajio na hivyo klabu kuathirika na mchango mdogo wanaotoa.

"Huku kwetu hakuna posho kama ilivyo kwa timu hizo wanaposhinda, hivyo wanapokuja huku wanacheza ili mradi yupo katika kazi, hivyo hatutegemei zaidi hawa wachezaji kutoka Simba na Yanga maana hawatakuwa kitu tunachotaka, anapokuwa katika hizi timu za chini hucheza 'kifadha'," alisema Zidadu.

Aliongeza wanaposajili wachezaji kutoka timu nyingine, nyota hao hujituma na kuipa timu kile kilichotarajiwa kwa sababu wanahitaji kuonekana na hatimaye kusajiliwa na vigogo hao au klabu nyingine za nje ya Tanzania.

"Niwe mkweli kwa upande wetu tumekuwa waathirika wakubwa wa wachezaji hawa, baada ya mwanzoni mwa msimu huu kuwachukua kwa mkopo wachezaji kutoka Simba," Zidadu aliweka wazi.

Namungo FC inayotumia Uwanja wa Kassim Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi, ni moja ya timu zilizoonyesha ushindani katika msimu huu ikiwa imepanga kwa mara ya kwanza, ambapo kwa sasa inashika nafasi ya nne ikiwa na alama 50 baada ya mechi 28.




Mkurugenzi wa Udhibiti na Utawala wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, ndoo maalumu za kuhifadhia maji ya kunawa mikono ikiwa ni sehemu ya kuiunga serikali mkono katika jitihada zake za utoaji elimu kwa vitendo namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *SportPesa yaiunga mkono serikali mapambano dhidi ya corona*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kuzuia kuenea kwa virusi vya corona (COVID-19), Kampuni ya SportPesa Tanzania imetoa vifaa na dawa kwa Wilaya ya Kinondoni ili kupambana na kasi ya maambukizi hayo.

Mchakato huo wa ugawaji vifaa umepokelewa kwa mkono miwili na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo ofisini kwake jana.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, Mwenyekiti ambaye ni Mkurugenzi wa Udhibiti na Utawala wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema wanaungana na serikali katika kuongeza jitihada na utoaji elimu kwa vitendo namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Tarimba alisema: "Tunaungana na serikali katika kupiga vita maambukizi ya virusi vya corona hapa nchini. Katika kutambua hilo, kama SportPesa tumeona ni vema kugawa vifaa muhimu kama ndoo na sabuni za kunawia mikono kwa ofisi za serikali za mitaa zinazohudumia wananchi kwa karibu zaidi kila siku, tukianza na wilaya ya Kinondoni.

"Hivyo mkuu wa wilaya pokea vifaa na tunaamini vitawasilishwa kwa walengwa ambao ni takriban zaidi ya ofisi 130 kwa niaba yetu."

SportPesa imekuwa mbele katika kuunga mkono shughuli mbalimbali za kijamii nchini ikiwa ni pamoja na kuwawezesha Watanzania kuweza 'kutoka' kimaisha kwa kubashiriri matokeo ya mechi kupitia kampuni hiyo.

Tofauti na kampuni nyingine za kubashiri matokeo nchini ambazo mshindi huambulia kitita cha fedha pekee, SportPesa mbali na fedha, kwa nyakati tofauti imekuwa ikiambatanisha ubashiri huo na zawadi mbalimbali zikiwamo bajaji, smartphone na gari.

Aidha, ni kampuni pekee ya kubashiri matokeo nchini inayoongoza kwa kudhamini klabu nyingi za soka, zikiwamo Simba, Yanga, Singida United na Namungo FC.

# Michezo

Jumanne Machi 31, 2020

Nipashe



Kane sasa aanza kuaga Spurs

UKURASA 30

ANAWIKA...



Hassan Dilunga (mbele) akishangilia pamoja na Meddie Kagere, moja kati ya mabao sita aliyoifungia Simba msimu huu. Licha ya Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime kusema Simba na Yanga zinaua vipaji vya chipuzi wanaowasajili, Dilunga huu ni msimu wa pili tangu atue Simba akitokea Mtibwa Sugar na amekuwa katika kiwango bora huku akiwaweka mastaa kibao benchi katika kikosi hicho. **PICHA: MAKTABA**

## Eymael aanza kuisuka Yanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema tayari umeshaanza kupitia na kufanyia kazi kimya kimya ripoti waliyokabidhiwa na benchi la ufundi linaloongozwa na kocha Mbelgiji Luc Eymael ambayo inaeleza mahitaji ya kikosi chake kwa msimu ujao.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, ameliambia Nipashe kwamba tayari wameshaanza mikakati ya usajili kwa wachezaji ambao wamependekezwa na Eymael.

"Ripoti ipo mezani, hivyo kamati husika inafanya kazi yake, mashabiki na wanachama wetu wanatakiwa kutulia na kusubiri muda utakapofika kila kitu kitawekwa wazi hasa suala zima la usajili," alisema.

Mwakalebela alisema kuna wachezaji wengi ambao wamekuwa wakitajwa kusajiliwa na klabu yao, na kwamba kamati imekuwa karibu na kocha kuhakikisha wanasajili mtu sahihi ambaye atakuja kufanya kazi.

"Suala la usajili ni jukumu la kamati husika ambayo wajumbe wake waliteuliwa kwa ajili ya kazi hiyo, hawafanyi kazi pekee yao bali wamemshirikisha kocha mwenyewe ambaye analeta mchezaji anaona anafaa na kusajili," alisema.

Alisema katika ripoti hiyo imeainisha sehemu nyingi ya usajili huku kocha akihitaji zaidi washambuliaji wawili kulingana na upungufu wa kikosi chake kwa msimu huu kwa safu hiyo kuwa na mabao machache.

Kocha huyo aliwahi kusema kwamba akipata nafasi ya kupendekeza wachezaji atahakikisha analeta nyota wazuri wenye kiwango bora kama ilivyo kwa kiungo mshambuliaji wao Bernard Morrison ambaye anafanya vizuri.

# Simba, Yanga zaonywa usajili

**Na Somoe Ng'itu**

● ● ● Ni kwa kusajili nyota wanaowika na kuua vipaji vyao, wanaokimbilia huko watahadharishwa kuwa...

WAKATI dirisha la usajili likiwa bado halijafunguliwa rasmi, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, ameweka wazi Simba na Yanga zinachangia kwa kiasi kikubwa 'kuua' vipaji vya wachezaji ambao walikuwa wanafanya vizuri kabla ya kujiunga na vigogo hao wa soka nchini.

**Hata hivyo, tayari klabu mbalimbali hapa nchini zimeanza kuboresha mikataba ya wachezaji wao inaowamiliki na kuzungumza na nyota wapya ambao wanamaliza mikataba na timu zao.**

Pia wako baadhi ya wachezaji ambao wametangaza wako huru na wanazikaribisha klabu nyingine kufanya mazungumzo kutokana na kanuni kuwaruhusu kufanya hivyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Maxime alisema klabu hizo kongwe nchini na zenye mashabiki wengi zaidi, zinachangia kurudisha nyuma viwango vya wachezaji kwa kushindwa kuwatumia vema baada ya kuwasajili na hivyo kuwapoteza katika ramani ya soka.

Beki huyo wa zamani Mtibwa Sugar ya Manungu, Morogoro alisema ili kumaliza tatizo hilo, makocha wa klabu nyingine wamekuwa na jukumu la kufufua vipaji vipya, lakini mara wanaposajiliwa na klabu hizo za Dar es Salaam, hali hubadilika na ndoto zao kupotea.

Maxime alisema ili kumaliza tatizo hilo, klabu hizo zinatakiwa kuhakikisha zinasajili wachezaji ambao zitawatumia kwa sababu "kuozea" benchi kunarudisha nyuma maendeleo ya wachezaji hao chipukizi iliyowasajili.

"Simba na Yanga zimekuwa ni mabingwa wa kuua vipaji, mabingwa wa kupoteza vijana, wanasajili wachezaji tuliowaibua na wanaong'ara kwetu, lakini wakifika kwa vigogo hao wanapotea, waache hii tabia," Maxime alisema.

Katika hatua nyingine, kocha huyo alisema kwake anajivunia kufanya kazi hapa nchini kwa sababu hakuna timu ya nje ambayo imewahi kumwahidi kumlipa mshahara mnono zaidi ya anaopata katika klabu yake hiyo ya mkoani Kagera.

"Siwezi kukubali kwenda nje tu ili nionekane ninafundisha nje ya nchi, hapa nilipo napata maslahi mazuri sana na ninaridhika, itakapotokea ofa nzuri nitaifikiria kabla ya kufanya uamuzi," Maxime, nahodha huyo wa zamani wa timu ya Taifa (Taifa Stars) na Mtibwa Sugar, alisema.

Aliongeza hata uamuzi wa kutosajili wachezaji wageni katika kikosi chake anauona si wa lazima kwa sababu nyota wa hapa nchini anaowatumia wana uwezo wa kufanya vizuri na kutoa ushindani katika mechi zote wanazocheza wakipambana na klabu zenye wachezaji mchanganyiko.

Mara kadhaa Maxime ametajwa kutua Yanga, lakini mara zote mchakato wa kujiunga na klabu hiyo ya Mtaa wa Twiga na Jangwani ukishindwa kukamilika, kwa sababu ya kutofikia dau analotaka.

Kocha huyo aliwahi kuliambia Nipashe kuwa anao mkataba aliopewa na viongozi wa klabu hiyo, lakini hajausaini na anaendelea kufanya kazi Kagera Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >